

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 4 Julai, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA PAMOJA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na (Utwala Bora) kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA,
SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na Utawala Bora, kwa Mwaka 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA
FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu, kwa Mwaka 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

MHE. SUZAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, PAMOJA NA UTAWALA BORA:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) pamoja na (Utwala Bora) Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. MCH. ISRAEL YOHANA NATSE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA RAIS, UHUSIANO NA URATIBU:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu, Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu na kufuatana na utaratibu wa Serikali *The most Senior Minister* ndiye anachukua nafasi ya kusimamia Shughuli za Serikali hapa Bungeni naye ni Mheshimiwa Samuel Sitta, ndiye atafanya kazi hiyo kwa muda wa wiki moja. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 165

Kero ya Maji Katika Mji Mdogo wa Ngudu

MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. MANSOOR SHANIF HIRANI) aliuliza:-

Mji mdogo wa Ngudu ambao ndio Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, una wakazi wengi na taasisi mbalimbali zinazotoa huduma za kijamii na kiuchumi lakini una matatizo makubwa ya maji ambayo hutokana na uchakavu wa pampu mbili za kuvuna maji na *pump* moja ya kusukuma na kusambaza maji kutoka kwenye vyanzo vya maji vilivyo eneo la Kilyaboya. Gharama za *pump* hizo kwa pamoja hazizidi shilingi milioni hamsini za Kitanzania.

Je, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha tatizo hili la maji linamalizika kwa wakati ili kuondoa kero hiyo iliyopo kwa muda mrefu sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mansoor Shanif Hirani Mbunge wa Kwimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Ngudu una wakazi 18,715 wanaohudumiwa na mradi wa maji chini ya mamala ya Maji Mji Mdogo wa Ngudu. Chanzo cha maji katika Mji Mdogo wa Ngudu na visima vya kati sita (6) vilivyochimbwa ambapo na kati ya hivyo visima 4 vina mitambo ya kuvutia maji kupeleka katika sampa ni tanki la kukusanya maji kutoka katika visima. Vipo visima viwili (2) mitambo yake imeharibika na havifanyi kazi kwa sasa. Aidha, jumla ya visima vitatu (3) vinahitaji kusafishwa ili kuhuisha uwezo wake wa uzalishaji maji. Kutoka kwenye sampo ya kukusanya maji kuna mitambo miwili (2) ambayo husukuma maji katika matanki ya usambazaji yaliyopo katika maeneo mawili ya Mjini. Mtambo mmoja umeharibika na unahitaji kununuliwa mtambo mpya.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na matatizo ya maji Mji Mdogo wa Ngudu, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, kupitia Bajeti yake ya mwaka 2011/2012 imetenga kiasi cha shilingi milioni 100.

Fedha hizo ni kwa ajili ya kununua mtambo mmoja wa kusukuma maji kutoka katika sampa hadi matanki ya usambazaji maji pale mjini. Vile vile pampu tatu za kuvuta maji katika visima ili kuongeza kiwango cha maji kitakachokusanya. Mamlaka ya Maji Mji Mdogo wa Ngudu, nayo katika Bajeti yake ya mwaka 2011/2012 imetenga kiasi cha shilingi milioni 6 kwa ajili ya kusafisha visima vitatu ili kuongeza kiwango cha maji katika visima hivyo.

Mheshimiwa Spika, kupitia mradi wa maji na usafi wa mazingira unaoteklezwa chini ya programu ya maji na usafi wa mazingira kitaifa (*WSSDP*), Mhandisi Mshauri *Don Consult Ltd.* Anaendelea kufanya upembezi yakinifu. Baada ya usanifu na kuandaa *tender document* ndipo shughuli za kutafuta mkandarasi zitafanyaika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, inashauriwa kuendelea kuzingatia katika vipaumbele vyake na kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji ili kuwaondolea adha wananchi wa maeneo hayo.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, kwa sababu maji ni uhai na maji hayawezi kusubiri. Je, Serikali sasa kutokana na ufinyu wa fedha ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, inazo Serikali inaweza mpango mkakati wa kuyatoa maji katika Kijiji Maro ambapo ni kilomita 70 kutoka Maro kwenda Ngudu maji ya Ziwa Victoria ili maji hayo sasa yaweze kusaidia Mji wa Ngudu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali imeshachukua hatua ndio maana imemwajiri na Mshauri ili aweze kufanya usanifu wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria. Lakini kwa muda wa matokeo ya haraka tumefanya utafiti pia wa kuweza

kuongeza visima na kusafisha vile vilivyopo ili wakati tunasubiri huu mradi angalau wananchi wa Magu waweze kupata maji.

MHE. MWIGULU L. MCHEMBA MADELU: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la pampu kuharibika hata Iramba lipo na gharama ya kusafisha pampu na kuhuisha visima vya Songambele, Kibaya, Misuna, Makunda na Kisharita ni dogo kuliko la kuchimba visima vipyta.

Je, Serikali inatoa kauli gani ili kuvihuisha visima hivyo ambavyo sasa wananchi wanapata tabu sana katika vijiji hivyo na vingine? (*Makofii*)

SPIKA: Mambo ya kusafisha visima yanatosha TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu kwenye jibu la msingi ya kwamba huduma za maji kwa jamii yetu linaona kwanza na jamii husika na kule tuna mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ambako kuna Baraza la Madiwani, Baraza la Madiwani linao uwezo sasa kubaini kuwa tatizo lililopo katika eneo hilo na kutenga Bajeti kuitia fedha ambazo zipo.

Pia niweze kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kuitisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo tumeikamilisha juzi na sasa suala la kupeleka fedha kwenye Halmashauri zetu sasa linaanza mara moja na kwa hiyo, sasa kama kunahitaji kuchimba visima vivyo hivyo, kuhuisha visima vilivyopo, kununua pampu ni maamuzi ya Halmashauri yenye ili kuweza kutoa huduma ya maji kwa jamii husika. (*Makofii*)

Na. 166

Uanzishwaji wa Kidato cha Tano na Sita katika Kila Tarafa Nchini

MHE. KAIKA SANING’O TELELE aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Nne katika sekta ya Elimu inahamasisha Uanzishwaji wa Kidato cha Tano na cha Sita katika kila Tarafa hapa nchini:-

Je, Serikali itasaidia vipi Tarafa ya Ngorongoro ambayo ni hifadhi mseto kupata kibali cha tathmini ya mazingira *Environmental Impact Assessment (EIA)* toka Baraza la Taifa la Mazingira (*NEMC*) haraka ili ujenzi na uanzishwaji wa vidato hivyo uweze kuanza kama ilivyo kwenye maeneo mengine nje ya Hifadhi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning’o Telele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tarafa ya Ngorongoro, ina hifadhi mseto na kwa kuwa kibali kinachoombwa kinatolewa na Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) nashauri Halmashauri husika iwasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Mazingira ili waiandikie *NEMC* barua ya kuomba eneo husika kufanyiwa *Environmental Impact Assessment (EIA)* ili kuona uwezekano wa kujenga shule hiyo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa EIA ni itifaki ya Kimataifa na kwa kuwa ripoti itakayotolewa itahusisha mambo ya usalama wa wanafunzi katika hifadhi mseto Halmashauri ikubaliane na ushauri utakaotolewa na *NEMC* na kuona uwezekano wa kujenga shule hiyo katika eneo jingine endapo eneo hilo walilochagua litaonekana halifai.

Mheshimiwa Spika, baada ya kibali hicho kupatikana, Wizara yangu itatoa kibali cha kuanza ujenzi wa shule kwa kuzingatia taratibu na vigezo vilivvopo vyta kuanzisha shule yenye kidato cha Tano na Sita. Aidha, Wizara yangu itakuwa tayari kusajili shule hiyo haraka baada ya kukamilisha ujenzi kwani azma ya Serikali ni kuwa na shule yenye kidato cha 5 na 6 kwa kila tarafa hapa nchini ili kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

MHE. KAIKA SANING’O TELELE: Mheshimiwa Spika, naona upatikanaji wa kibali kutoka Baraza la Taifa la Mazingira ina mlolongo mrefu.

(a) Je, Serikail haiwezi kupandisha hadhi Sekondari ambayo iko katika Tarafa ya Ngorongoro ya *O’level* ili iwe na kidato cha Tano na Sita?

(b) Kama hilo litafanyika na kwa sababu tulikuwa tumeshaanza maandalizi. Je, Serikali iko tayari kutoa kibali hata mwishoni mwa mwaka huu tuanze Februari mwaka kesho?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, kama nilivyosema ni Hifadhi Mseto na kama Mheshimiwa Mbunge, mwenyewe alivyogundua kwamba utaratibu wa hawa wa kuwaandikia *NEMC* barua ni taratibu ndefu.

Lakini kwa vile vile agizo la Mheshimiwa Rais tunataka angalau kila tarafa iwe na sekondari ya *A- level*, mimi nawashauri Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro waweze kufikiri namna ya kutafuta vigezo vyta kupandisha hadhi katika shule moja zilizopo kwenye Halmashauri sisi Wizara ya Elimu hatuna matatizo kabisa, tutatuma wakaguzi watakuja kukagua Kanda ya Kaskazini, kule Arusha watakapokuwa tayari tutatoa kibali cha kuanzisha shule moja iwe *A- level* katika Halmashauri hiyo. (*Makofit*)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tarafa ya Ngorongoro ni Tanzania na ukisema itajengwa shule kwa kila kata na Ngorongoro wanaishi watu kwa hiyo, wana kata hizo, Je, ni sheria gani inazuia Kata za Ngorongoro zisipate shule za Kata?

SPIKA: Sijui kama amekuelewa naona kama anapata tabu hata namna ya kusimama.

MHE. KAIKA SANING’O TELELE: Mheshimiwa Spika, ni kwamba Ngorongoro ni Tarafa na ina kata kama Mikoa mingine, kama eneo lingine la Tanzania. Lakini wao wananyimwa wasijenge shule kwenye kata zao kwa hizi shule za kata. Je, ni sheria gani ambayo inawanyima baadhi ya Watanzania wasiwe na shule kwenye kata zao? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naona sasa umeelewa vizuri swali lenyewe.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza historia ya *nature* ya Wilaya ya Ngorongoro iko tofauti kabisa na Halmashauri zingine hapa nchini na ndio maana lile eneo nasema hivi linaitwa Hifadhi Mseto maana yake kuna wanyama, kuna mifugo mingine ya Wamasai kule na watu wanaishi katika eneo lile. Kwa hiyo, nilichosema hapa ni kwamba hawanyimi haki ya watoto kusoma pale. Kinachotakiwa Mheshimiwa Mbunge, awasiliane na Halmashauri yake atuandikie barua wateue shule moja ambayo itakuwa ina vigezo vya kuanzisha kidato cha Tano na Sita sisi Wizara ya Elimu hatuna matatizo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali. Kwa bahati nzuri Wilaya ya Serengeti, iko bega kwa bega na maelekezo ya Serikali kila tarafa iweze kuwa na Sekondari ya *A’ level*. Hivi karibuni Wizara ya Elimu na Mafunzo walifanya ukaguzi Sekondari mbili ikiwemo ya Ngoreme pamoja na ya Ikoma zimeweza kukidhi vigezo lakini kwa masharti madogo. Wizara ya Elimu na Mafunzo ina mpango gani kuungana na juhudhi hizi za Jimbo la Serengeti kuhakikisha kwamba suala zima la mazingira linaangaliwa kwenye Sekondari hizi mbili pamoja na umeme? Naomba nipate jibu.

SPIKA: Naona hilo ni swali jipya Waziri hana hakika ni wapi unaposemea. Haya Naibu Waziri mijibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kutoa jibu fupi tu kwa Mheshimiwa Dkt. Kebwe, mbunge wa Serengeti.

Nadhani hata Mheshimiwa Spika amegundua swali hili ni jipya, lakini nadhani Mheshimiwa Mbunge alikuwa anahitaji huduma za umeme na maji kwa Wilaya ile, nadhani tutashirikiana nao tu kadiri ya taratibu zilivyo na bado kuna waraka wa sheria ya mazingira kwenye mashule, naomba Mheshimiwa Mbunge hata tukitoka hapa, nikienda pale Ofisi ndogo ya Wizara ya Elimu niweze kukupatia waraka wa mazingira mashulenii, tunashirikiana na vigezo viro, tutakwenda pamoja. (*Makofi*)

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y. MHE. LUCY F. OWENYA) aliuliza:-

(a) Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2004-2010 ni maombi mangapi ya mikopo kwa wanafunzi ilitolewa na Bodi ya Mikopo na kwa wanafunzi wangapi kwa kutaja idadi, aina ya madaraja na asilimia?

(b) Kati ya mikopo iliyotolewa, ni mawafunzi wangapi walipata mikopo kati ya hao wapo vyuo vya nje, kwa kutaja nchi na idadi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mhehsimiwa Spika, Bodi ya wanafunzi wa elimu ya juu ilianza kutoa mikopo mwaka 2005/2006 na jumla ya wanafunzi waliokopeshwa na kiasi cha mkopo kilichotolewa kwa miaka hiyo mitano ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2005/2006 idadi ya wanafunzi walikuwa 42, 729 na fedha iliyotolewa ni shilinmgi 56.11, mwaka 2006/2007 idadi ya wanafunzi ilipanda kufikia 47,554....

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hilo swalii kwa mujibu wa kanuni zetu, yaani akitusomea hapa hesabu mwaka hadi mwaka haiwezekani, naomba usome mwaka wa kwanza na wa mwisho ulioko current na mwaka wa mwisho halafu yeye atapewa jibu kwa maandishi, kwa sababu ni data tupu hili swalii zima, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tulijibu kama Mbunge alivyokuwa ameomba lakini kwa masharti hayo naomba nisome kwa mwaka wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010 idadi ya wanafunzi waliopata mkopo ni elfu 72,035 na jumla ya fedha ilikuwa ni bilioni 186,484,719,680.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa mgawanyo wa mikopo katika madaraja na asilimia ni kama ifuatavyo; sasa na hapa napo kuna mlolongo wa takwimu kubwa, lakini kwa asilimia mia moja wanapata daraja la A, asilimia 90 wanapata daraja la B, asilimia 80 wanapata daraja la C, asilimia 70 wanapata daraja la D, asilimia 60 ni daraja la E, asilimia 50 ni daraja la F, asilimia 40 daraja la G, asilimia ya 30 ya mkopo wanapata daraja la H, asilimia 20 wanapata daraja na I na asilimia 10 wanapa daraja la J. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mikopo iliyotolewa katika kipindi cha 2005/2006 hadi 2009/2010 kwa wanafunzi wanaosoma katika Vyuo Vikuu nje ya nchi ni kama ifuatavyo:-

Wanafunzi 920 wanaosoma vyuo vikuu nje ya nchi walionufaika, Algeria wanafunzi 250, China wanafunzi 145, Cuba wanafunzi 67, Urusi wanafunzi 223, Poland wanafunzi 17, Rwanda mwanafunzi 1, Nchi ya Czech wanafunzi 3, Afrika Kusini wanafunzi 22, Uganda wanafunzi 68, Ukraine wanafunzi 87, Msumbuji wanafunzi 33, Malasyia mwanafunzi 1, India wanafunzi 2 na Ururuki mwanafunzi mmoja (1). (*Makofit*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kutokana na majibu ya Naibu Waziri nina swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Hivi karibuni kwenye vyombo vyahabari kumejitokeza taarifa za maagizo ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wakisema kwamba wanafunzi warudishwe vyuoni wakifuata wale wa CCM na mikopo itolewe kiubaguzi.

Vilevile kuna dokezo sabili ambalo limetolewa na Waziri wa Elimu kwenda kwa Katibu Mkuu kuelekeza kwamba Bodi ya Mikopo kutokana na mgomo wa *UDOM* itoe mkopo kwa maagizo maalum kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM*, ningependa kupata kauli ya Serikali kuhusu taarifa hizo zenyenye muelekeo wa kiubaguzi kwenye utoaji wa mikopo ya elimu ya juu inayotokana na fedha za Umma?

(b) Kwa kuwa matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ya ndani na nje yanaendelea ikiwemo hivi sasa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Lumumba walioko Urusi ambao wamecheleweshewa pesa kwa miezi tisa na wamepewa pesa pungufu na wako kwenye hali mbaya.

Je, Serikali haioni sasa pamoja na kuundwa kwa Tume iliyochunguza masuala ya mikopo ambayo bado taarifa yake hajatolewa, haino sasa imefika wakati wa kuivunja Bodi ya Mikopo na kuunda chombo kingine kitakachosimamia vizuri mfumo wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Kiunfundi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyika, lakini kwa niaba ya Mheshimiwa Lucy Owenya kama ifuatavyo:-

SPIKA: Hapana haya ni ya Mnyika mwenyewe haya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Mhehsimiwa Mnyika mwenyewe, ahsante sana. suala alilosema kwamba Mheshimiwa Waziri ameandika dokezo kwenda UDOM kwa ajili ya masuala ya ada au yanayohusu Bodi ya Mikopo nadhani ni mwendelezo mzima wa masharti ambayo yametolewa ili wale wanafunzi waweze kurudi katika hali ya vigezo ambavyo tunaona

kwamba wanafunzi waliokuwa wamefanya mgomo, tusingeweza kuwarudisha kwa mtindo tu wa kwamba nitangaze tu kwamba wanafunzi rudi, ni moja ya masharti ambayo tunasema kwamba ili wanafunzi warudi wawe wamekamilisha maagizo mengine ambayo ni pamoja na ada za wanafunzi. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hawa wanafunzi wa Urusi ambao wamecheleweshewa mikopo yao, nadhani kama unavyojuwa Mheshimiwa Mnyika kwamba Serikali yetu miaka yetu ya fedha inayoanza tarehe 1, Julai na fedha yetu inaenda kwa *quarterly*, kwa hiyo yawezekana kule Urusi mwaka wao wa fedha labda unaanza Febrauri au Januari au unaanza Aprili na ndiyo maana hizo fedha hazikuwa zimeenda kwa wakati huwo zikaonekana labda kwamba zimechelewa. Lakini nakuhakikishia Mheshimiwa Mnyika kwamba nadhani tukitoka hapa tuangalie hili suala likoje na tuone kama kweli mpaka sasa hivi wale wanafunzi wana matatizo ili tuweze kuwatumia fedha huko waliko.

Mhehsimiwa Spika, kuhusu kuvunja Tume ya hii Bodi ya Mikopo. Nadhani ni kama tunavyoeleza kila siku kwamba Mhehsimiwa Rais ameunda Tume na Tume hiyo imeshamaliza kazi, kinachosubiriwa ni utaratibu mdogo tu ifike kule kwenye Baraza la Mawaziri, tuweze kuona vile vigezo na tutaleta hapa Bungeni, tutajadili tuone uwezekano wa namna gani tumeboresha vile vigezo. Suala si kuvunja Bodi ya Mikopo, suala ni kuangalia tumerekebisha vipi mfumo mzima wa utoaji wa Bodi ya Mikopo.

SPIKA: Ili suala la Urusi hata mimi nina *e-mail*, nitakuleteeni ya hao wanafunzi. Nina *e-mail* yao kwa hiyo ntakuletea ili kusudi muweze kuangalia.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali fupi la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu. Ni kweli au si kweli kwamba Serikali imeagiza Chuo Kikuu cha Dodoma kirudishe wanafunzi kwa kufuata kadi zao za vyama, uwanchama wa vyama vyao vyaa siasa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu Tundu Lissu kama ifuatavyo:-

Mimi nasema hivi kwa niaba ya Serikali, si kweli kwamba serikali inaweza ikafanya jambo kama hilo, hali tukitambua kwamba Serikali ya Tanzania ilikubali mfumo wa vyama vingi na wale wanafunzi wanapochaguliwa pale huwa hatufuati dini, rangi, ukabila wala hatufauti Chama. Natamka wazi kwamba si kweli na kama Mhehsimiwa Tundu Lissu ana ushaidi, basi tukitoka hapa tuonane aniambie ni wanafunzi wanagapi ambao tumewafanyia jambo kama hilo ili tuweze kulifutilia. (*Makofifi*)

Na. 168

**Gawio la Faida ya Uwanja wa Sabasaba Katika Halmashauri
ya Wilaya ya Temeke**

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Uwanja wa maonesho ya sabasaba uko katika Wilaya ya Temeke-Dar es Salaam na ukarabati ambao umefanyika katika uwanja huo umesabbisa kuingiza watu wengi sana wakati wa maonesho na kuiletea faida kubwa kwa Serikali:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani wa kutoa gawio la faida hiyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke ili isaidie katika shughuli ya maendeleo?

(b) Je, ni kiasi gani cha faida kilichopatikana katika uwanja huo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na maonesho ya saba saba hukatwa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) na pia hukatwa kodi ya majengo (*property tax*) ambazo huchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya nchi ikiwemo Wilaya ya Temeke. Aidha, faida inayotokana na maonesho hayo, hutumika katika kuendeleza na kuboresha maonesho ya Kimataifa ya biashara, sambamba na kuendeleza biashara ya ndani ya nchi na biashara ya nje ya nchi kama yalivyo majukumu ya mamlaka ya maendelo ya biashara Tanzania (*Tan Trade*).

(b) Mheshimiwa Spika, *Tan Trade* imekusanya fedha kutokana na kiingilio wakati wa maonesho ya biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Naomba kama ulivyo elekeza nitoe takwimu za mwaka wa kwanza na mwaka wa mwisho. Kipindi cha mwaka 2005/2006 mapato yalikuwa shilingi bilioni 1.02 wakati matumizi yalikuwa shilingi milioni 461 na kubakiwa na ziada ya shilingi milioni 560. Mwaka 2009/2010 mapato yalikuwa shilingi bilioni 1.8 na matumizi yalikuwa 1.3 na kubakiwa na shilingi milioni 547 kwa matumizi ya kawaida na uwekezaji.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa maonesho ya saba saba ni biashara, kwa maana hiyo huwa ni mradi na mradi ule unatuzwa kwa asilimia kubwa na wananchi wa Wilaya ya Temeke.

Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wananchi wa Wilaya ya Temeke kuwapa angalau gawio kidogo katika shughuli za Maendeleo hata kuchangia madawati kwa shule za msingi? (*Makofii*)

(b) Kwa kuwa uwaja wa sabasaba uko katika Mkoa wa Dar es Salaam na hakuna uwezekano labda wa kupata gawio, lakini kwa kuwa pia Temeke imepata na

tatizo la vifo vya watoto wakati wa shughuli za sikuku kama vile *Eid* na Krismasi. Kwa mfano Wilaya ya Temeke watoto walikufa kwenye ukumbi wa *Luxury Pub* kwa kukosa eneo la kuchezza.

Je, Serikali itakuwa tayari kukutana na wananchi wa Wilaya ya Temeke na Mkoa mzima Dar es Salaam kusaidia angalau kufungua uwanja ule nao watoto wa Temeke wachezee katika siku za sikuku za *Eid* na Krismasi nao wafaidike na mali yao? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali inafanya kila linalowezekana kuyaendeleza maonesho haya na katika kipindi chote cha maonesho ajira ambayo inapatikana ya muda kwa Wanatemeke na wananchi wa Jiji la Dar es Salaam imeendelea sana kuwafaidisha wananchi hao na kuwaongezea kipato.

Jambo la pili, maonesho haya ya Kimataifa yanayofanyika katika Wilaya ya Temeke yameendelea kuwa maarufu na yameendelea kwa uhakika kabisa kuliongezea Taifa kipato kwa maana ya kutangaza biashara yetu ya ndani na biashara ya nje na faida hasa inayopatikana ni baada ya maonesho yale kupita katika mwaka mzima unaofuata kabla ya maonesho mengine.

Kwa hiyo, tunatumaini kwamba wananchi wataendelea kuchukua fursa hii, wataendelea kujitokeza katika biashara mbalimbali na tunatumaini kwamba wana Temeke kama walivyo wana Dar es Salaam na wananchi kwa ujumla wataendelea kufaidi.

(b)Vifoo na matatizo mengine yanayotokana kutohuna na msongamani wakati wa maonesho, yameendelea kupatiwa ufumbuzi ya uwekezaji ambao umeendelea kufanywa na *Tan Trade*. Kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, kati ya mwaka 2005 hadi sasa hivi *Tan Trade* imekuwa ikiwekeza uwanja huu umeboreka hadi kufikia mwaka huu umetajwa kuwa mionganini mwa maonyesho yaliyofikia hadhi ya Kimataifa na hivyo kupunguza kabisa uwezekano wa matatizo yanayoweza kujitokeza, lakini *Tan Trade* pamoja na Wizara yangu tutaendelea kuangalia uwezekano wa jinsi gani viwanja hivi vinaweza vikafunguliwa wakati maonesho hayafanyiki.

Na. 169

**Msaada kwa Wazazi Wanaojifungua zaidi ya
Watoto Wawili**

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Imejitokeza mara nyingi katika Mikoa mbalimbali nchini wanawake wakijifungua zaidi ya watoto wawili kwa mpigo hali inayosababisha mzigo mzito kwa wazazi na walezi wao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa msaada kwa wazazi hao ili kuwapunguzia mzigo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mfuko wa msaada wa Rais kwa kina mama wanaojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mpigo imekuwa ikiwasaidia akina mama hao fedha kwa ajili ya kusaidia kuboresha lishe ya watoto. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imekuwa ikiratibu mfuko huo. Katika kipindi cha mwaka 1985-2010, jumla ya akina mama 632 wamesaidiwa na mfuko huo. Aidha, kiasi cha fedha ambazo hupewa mama anayejifungua watoto zaidi ya wawili (2) kwa mpigo, kimekuwa kikibadilika kulingana na mabadiliko ya thamani ya fedha yetu na hali ya uchumi. Mwaka 1985-1988 walikuwa wanalipwa Tshs. 10,125/=, mwaka 1989-2002 walikuwa wanalipwa Tshs. 32,184/=, mwaka 2003 mpaka sasa wanalipwa Tshs. 150,000/=.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu umekuwa ukiwanufaisha walengwa kutoka katika Mikoa mbalimbali nchini, ambapo maombi yao hupitia katika Ofisi za Ustawi wa Jamii za Mikoa na katika Halmashauri mbalimbali kisha kupelekwa katika Idara ya ustawi wa Jamii Makao Makuu kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Fedha zinapokuwa yayari hutumwa katika ofisi za Mikoa au Halmashauri husika kwa njia ya “*Warrant of Fund*” ambapo kina mama walioomba huenda kuzichukua katika ofisi hizo. Hata hivyo katika Halmashauri ambazo hakuna Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii wamekuwa wakituma maombi hayo kwenda Idara ya Ustawi wa Jamii Makao Makuu kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi hutolewa mara moja tu na akina mama hao hushauriwa kuzitumia kuanzisha na kuendesha miradi midogo midogo itakayowawezesha kuwa na uhakika wa lishe kwa watoto wao kwa kipindi kirefu. Mfano biashara ya genge, kilimo cha mbogamboga au ufugaji wa kuku. Faida wanayoipata itawasaidia kuwapatia watoto wao lishe ya uhakika.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba nimwulize maswli mawili tu ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa wanawake wengine wanajifungulia majumbani na ni vijijini ambako hakuna Ofisi za Ustawi wa Jamii na wazazi wengi wala hawajui haki hiyo.

Je, haki yao hiyo wataipataje au wataijuaje?

(b) Kwa kuwa kulingana na ugumu wa maisha kwa sasa hivi, kiasi hiki ni kidogo na utolewa mara moja tu. Je, Serikali ina mpango wowote wa kutoa zaidi ya mara moja?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna akina mama wanaojifungulia majumbani na wanazalishwa na wakunga wa jadi, lakini naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Vijiji vyetu kuna Serikali na kwenye hizo Serikali kuna Kamati za Afya na kwenye kila Kata kuna Afisa Maendeleo ya Jamii.

Basi ningependa kuchukua fursa hii niwaeleza wananchi wote kwamba panapotokea tukio kwamba kuna mama anajifungua zaidi ya watoto wawili, ninaomba Maafisa Maendeleo ya Jamii na Viongozi wetu wa Vijiji watoe taarifa ili na wao waweze kusaidiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hiki kiasi tunachokitoa ni kidogo na kinafuatana na kifungu ambacho tunachokipata, mwaka jana tulipata shilingi milioni 5 tu, mwaka huu tumeomba milioni 7 na laki 7 (7,700,000/=). (*Makofi*)

Lakini mimi naomba nitoe wito kwamba katika Halmashauri zetu wana uwezo wa kuweza kuwasaidia hawa akina mama kwenye mafungu ambayo wanapewa kwa ajili ya makundi maalum.

Ni kweli wanahitaji msaada lakini naomba nitoe wito kwenye Halmashauri kwamba na wao waangalie namna ya kuwasaidia kutokana na fedha ambazo wanazipata za kusaidia wale mavu na wale ambao wana matatizo maalum. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa sababu hili swali linaonekana la hisani na ndiyo sababu wakati pesa zikiombwa zinapelekwa kidogo sana. Kwa nini lisiwe la kisheria ili Serikali iwajibike kuhakikisha kwamba hizi pesa zinapatikana ili hawa wanawake wanaojifungua watoto zaidi ya mmoja waweze kufaidika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hili suala ni gumu kidogo kwa wananchi wetu ambao kwa bahati nzuri mimi nasema bahati nzuri wanazaa watoto zaidi ya wawili.

Lakini suala la kutungia sheria ninaomba niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge avute subira na sisi tutaliangalia kama Wizara, tutaangalia na Wizara nyingine ambazo

zinahusika na hawa ambao ni Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili tuone kwamba muafaka utakuwaje na siyo lazima litungiwe sheria ila tunaweza pia tukazungumza na Wizara nyingine zinazohusika na wakapewa maelekezo wahusika wakawa wanatoa misaada, kwa sababu penye nia pana njia Mheshimiwa Spika. (*Makofî*)

Na. 170

Serikali Kusaidia Jamii Isiyojiweza

MHE. MARTHA J. UMBULLA (K.n.y. MHE. RITHA L. MLAKI) aliuliza:-

Watu wengi hapa nchini wakiwemo wanawake na watoto hawana mahitaji ya kutosha na hviyo kukosa huduma za msingi kama vile chakula, matibabu na mavazi. Aidha, kuna watu wenye uwezo wa ziada wenye lengo la kusaidia jamii lakini hawajui watawapataje.

- (a) Je, Serikali inasaidiaje *NGOs* zilizo tayari kuwaunganisha watu wenye uwezo na nia ya kusaidia jamii?
- (b) Je, Serikali inatambua ni asilimia ngapi ya watu nchini wanaishi katika maisha duni?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritha Louise Mlaki, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika maeneo ya kijamii na kiuchumi.

Kwa kuzingatia hilo, Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali ili kuwawezesha watu wenye nia ya kusaidia jamii kupitia Mashirika haya. Hii ni pamoja na kuandaa Sera ya Taifa ya *NGOs* ya mwaka 2001 na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 ambazo utekelezaji wake umesaidia sana kuweka mazingira mazuri kwa watu wenye nia ya kusaidia jamii hususani wanawake na watoto kupitia taasisi hizi.

(b) Mheshimiwa Spika, ndiyo Serikali inatambua kwamba asilimia 33.4 ya wananchi wa Tanzania Bara wanaishi katika umaskini. Hii ni kwa mujibu wa matokeo ya uchambuzi wa Savei ya Mapato na Matumzi katika Kaya kwa Tanzania Bara iliyofanyika mwaka 2007, kiwango cha umaskini kitaifa kilipungua kwa wastani wa 2.2% kutoka asilimia 35.6 mwaka 2000/2001 hadi asilimia 33.4. Kiwango cha kupungua ni kikubwa zaidi katika maeneo ya mijini ikilinganishwa na maeneo ya vijijini.

Hata hivyo, Serikali inatarajia kufanya utafiti kama huu mwakani ili kupata takwimu *current*.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika na mimi namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja nyongeza. Kwa kuwa *NGOs* nyingi hapa nchini zinajikita kwenye shughuli zao maeneo ya mijini na kuacha maeneo ya vijiji na kwa kuwa Serikali inaratibu na kujua ni *NGOs* ngapi na ziko sehemu gani.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba ni wakati muafaka sasa kuweka utaratibu mahususi na kuwaelekeza *NGOs* hapa nchini zinazoshughulika na kuondoa umaskini, kuweka utaratibu mahususi kuelekeza shughuli zaidi maeneo ya vijiji na kupunguza kujikita maeneo ya mijini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA): Mheshimiwa Spika, *NGOs* ni taasisi ambazo zinaanzishwa kwa hiari. Kwa hiyo, uhiari unategemea pia uhamashajji. Serikali inalijua hilo kwamba taasisi nyingi za namna hii ziko mijini kuliko vijiji na kupitia kwenye Bodi ya Uratibu ya Vyama hivi Serikali inaendelea kutoa mwamko kwamba kuwe na uanzishwaji wa taasisi kama hizi vijiji kama inayofanyika kwenye miji tofauti.

MHE. MATHA M. MLATA: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema wataendelea kutoa ushawishi kwa *NGOs* ziweze kusaidia hata maeneo ya vijiji.

Je, Serikali iko tayari sasa kutumia Ofisi za Makatibu Tarafa kuitia ma-WEO na ma-VEO ili kuwatambua wahitaji na kuwaunganisha na *NGOs* hizo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA): Mheshimiwa Spika, ndiyo Serikali iko tayari na inaendelea kufanya kazi hiyo kwa kutumia Baraza la Taifa la Vyama visivyokuwa vya Serikali. Inafanya ziara na kuonana na wananchi mbalimbali pamoja na vyama ili kuwashawishi na kuwahamisha waweze kushiriki vizuri katika mambo haya na kuanzisha vyama vipyta kwa matatizo au changamoto ambazo zinaonekana zipo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa hao wanawake ambao wana hali ya umaskini ni pamoja na wanawake wengi waishio vijiji ambao ni wazee na wamekuwa wakinanza watoto yatima na kutegemewa na jamii ya familia inayowazunguka na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2010 wakati akihitubia siku ya wazee duniani aliahidi sasa kuanzishwa kwa Sheria ya Sera ya Wazee ambayo itasaidia kutoa pensheni kwa watu wazee wakiwemo wanawake ili kuwasaidia kuondokana na kipato duni na umaskini.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutujibu sasa mkakati wa kuyafanya hayo yote utaanza lini rasmi ili wazee wanawake lakini na wazee wengine wote waanze kupata pensheni ili kuondokana na matatizo ya umaskini yanayowakabili? (*Makofî*)

SPIKA: Ilikuwa *NGOs* sasa Serikali. Endelea nani anajibu wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA): Mheshimiwa Spika, mchakato wa kutaka kuanzisha utaratibu wa pensheni za wazee umeshaanza. Sio utaanza lini. Serikali inalitafakari hili suala na sasa hivi inajipanga ili lianze kufanyiwa kazi kwa maana ya utekelezaji. Ni tamaa ya Serikali kwamba haitapita zaidi ya mwaka wa fedha ujao kabla halijatekelezwa. (*Makofi*)

Na. 171

Mamlaka ya Mapato Tanzania

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA aliuliza:-

(a) Je, kwa nini bidhaa zinazolipiwa ushuru wa Forodha Tanzania Zanzibar zikifishwa Dar es Salaam zinazotozwa tena kodi ya forodha?

(b) Je, hali hii haionyeshi kuwa kuna udhaifu na kasoro ndani ya Mamlaka hiyo, kwa kutoza ushuru mara mbili na kwa ubaguzi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cherles John Tizeba, Mbunge wa Buchosa, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato katika kutekeleza majukumu yake ya kukusanya na kuzuia uvujaji wa mapato ya Serikali imepewa nguvu za kisheria na inawajibika kuifuatilia kodi wakati wowote na mahali popote ilipo. Hali kadhalika, pale inapothibitika kuwa kodi haikukuysanywa kikamilifu kwa sababu yoyote ile, Mamlaka huchukua hatua za kisheria kukusanya tofauti kati ya kodi sahihi na ile iliyokusanywa awali na hii haimaanishi kutozwa tena ushuru wa Forodha.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu huu hutumika si kwa mizigo inayoingia kupitia Tanzania Zanzibar tu na kuvushwa kuja Bara bali ni kwa mizigo yote inayoingia kupitia kituo chochote cha Forodha nchini na bila ubaguzi wowote. Kinachosababisha hali hii ya ukusanyaji sio udhaifu na kasoro za *TRA* bali mara nyingi ni ama waingizaji wa mizigo wenyewe kutotoa taarifa sahihi au kwa wao kufanikiwa kuwapiga chenga maafisa wa Forodha kwenye hatua za awali za uingizaji mizigo.

Mheshimiwa Spika, kwa kulitambua hilo, ndiyo maana Mamlaka imeweka katika muundo wake wa vitengo vya *Free Anti-Smuggling Team (FAST), Post Clearance Audit* na Idara ya Upelelezi wa kodi kama ngome ya pili ya ulinzi (*Second line of Defence*).

Mheshimiwa Spika, katika juhudi zake za kupunguza kujirudia rudia kwa hali hii, Mamlaka ya Mapato imeanzisha mfumo wa kompyuta ambapo kadhia za uingizaji mizigo kupitia vituo vyote nchini zinashughulikiwa kupitia kituo kimoja tu cha (*Dar es*

Salaam Customs Service Centre). Mfumo huu ulianza karibuni mwaka mmoja uliopita kwa upande wa Bara na unaleta uwiano mkubwa wa uthamini wa bidhaa. Aidha, mamlaka inakusudia kuvunganisha vituo vyote vya forodha ikiwemo Zanzibar katika mfumo huu ili kuleta ufanisi.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa imeonekana mara nyingi sana kwamba *tendency* hii ya mtu kutozwa tena au kufuatiliwa ili alipe hiyo tofauti imekuwapo tu kwa upande wa wale wanaoingiza mizigo kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam kinyume chake hakitoki kabisa.

Je, Serikali haioni kwamba kuna udhaifu huko kwa Watendaji wa TRA Zanzibar ambao wanasababisha kero hii kwa wananchi?

Kwa kuwa pia wako Watendaji wengi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania hasa Watendaji Wakuu ambao wamekaa kwa muda mrefu sana na hatutarajii jipya kutoka kwao. Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kubadilisha Menejimenti ya TRA?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA): Mheshimiwa Spika, kwanza mafunzo yanayotolewa na TRA kwa wafanyakazi wa Zanzibar na sehemu nyingine ni sawa sawa. Tofauti inatokea kwenye ubinadamu au pengine uhalisia wa imani ya mtu katika kufanya kazi. Kwa hiyo suala la udhaifu la watendaji wa Zanzibar linaweza likawa siyo kigezo. Pengine kuna matatizo mengine ambayo tunaendelea kuyafuatalia.

Wafanyakazi wa Makao Makuu na *TRA* sehemu nyingine huwabadilisha, hii ni kazi ambayo inaendelea kila siku, huwa wanabadilishwa vituo na wengine ambao wanafanya vibaya wanaweza wakafukuzwa kuitopia Kamati ya Maadili ambayo iko ndani ya *TRA* yenye na Serikali.

MHE. ENG. MOHAED HABIB JUMA MNYAA: Nashukuru Mheshimiwa Spika kunipatia kuuliza swali moja la nyongeza. Mbali na Tanzania Bara kutoza ushuru zaidi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar hasa magari, na kwa kuwa Zanzibar gari zikitolewa pale bandarini zinapatiwa *Registration Number* ambazo zina mfumo wa kitaifa zinazoanza Z halafu kuna namba ya tarakimu tatu halafu na herufi nyingine pale sawa na upande wa Tanzania Bara walivyonavyo, ni kama vile Zanzibar walivyoanza kutumia leseni za *Smart Card* halafu na Tanzania Bara imefuata.

Lakini kwa kuwa gari zikiingia Dar es Salaam kutokea Zanzibar ambazo zina nambari tayari, zinalazimishwa lazima zifuate nambari za hapa na kubadilishwa nambari zile za Zanzibar tofauti na zinatoka Dar es Salaam zikiingia Zanzibar hazilazimishwi. Je, Waziri unaweza ukatoa tamko la Serikali sasa hivi kugomea suala hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA A. SILIMA): Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya uamuzi kwamba gari zinazokuwa *registered* zinaweza kwenda sehemu yoyote ili mradi *registration* itakuwa imewekewa kumbukumbu ya

kusafirishwa. Kwa hiyo inaonekana kuna tatizo la kiutendaji ambalo tunahitaji kulifanya kazi ili tatizo hilo lisijitokeze. (*Makofi*)

Na. 172

Hitaji la mabwawa ya umwagiliaji – Shinyanga

MHE. AZZA HILLAL HAMAD aliuliza:-

Mkoa wa Shinyanga unalima mpunga kwa wingi:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchimba mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hususan Kata za Lyabukande, Ilola na Mwakitolyo, Welezo na Solwa?

(b) Je, Serikali itatimiza lini ahadi iliyotolewa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge, ya kuchimba bwawa la umwagiliaji katika Kijiji cha Masengwa mwaka 2006-2007? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imejiwekea malengo ya kupanua eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 334,000 (2010/2011 kufikia hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2015. Aidha, dhamira ya Serikali ni kwamba ifikapo mwaka 2015, asilimia 25 ya chakula chote kitokane na Kilimo cha Umwagiliaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo, Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani hapa nchini katika mikoa yenye mito ya kudumu hususan mikoa ya Kigoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa na Mkoa wa Ruvuma. Katika mikoa kame hususan ya Dodoma, Shinyanga, Singida na Tabora umuhimu utawekwa katika kuvuna maji ya mvua kwa kujenga mabwawa madogo madogo na makubwa 33 kati ya mwaka 2010/2011 na 2015/2016. Aidha, matumizi ya maji chini ya ardhi kwa kutumia teknolojia ya Umwagiliaji kwa njia ya matone yaani (*Drip Irrigation*) yatasisitizwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi na katika Mkoa wa Pwani. (*Makofi*)

Serikali itaendelea na utaratibu wa kugharimia miradi ya Umwagiliaji kupitia Programu ya *ASDP* ambapo miradi inaibuliwa na kuwekwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) na kuombewa fedha katika Mfuko wa

Maendeleo ya Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*DIDF*) kwa miradi midogo na ngazi ya Taifa (*NEDF*) kwa miradi mikubwa.

Kwa kuzingatia ahadi iliyotolewa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa mwaka 2006/2007, Serikali imekwishaendeleza miradi minne ya Umwagiliaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Miradi iliyokwishaendelezwa ni Masengwa (450 ha), Nyida (600 ha), Nduguti (150 ha) na Butini (400 ha) ambayo yote inazalisha mpunga. Aidha, katika mwaka wa 2011/2012, Serikali imepanga kujenga bwawa la Ishololo ili kuongeza upatikanaji wa maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itatuma Wahandisi wa Umwagiliaji kwenda kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ili kuchunguza eneo linalofaa kujenga bwawa huko Lyabukande, Ilola, Mwakitalyo na maeneo mengine. Eneo litakaloonekana linafaa kitaalam litaingizwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

MHE. AZZA HILLAL HAMAD: Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuiendeleza miradi ya umwagiliaji ambayo imekuwa haina manufaa kwa wananchi kwa kuwa maji yamekuwa yakipotea bure?

Swali la pili, kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu ilikuwa ni kujenga bwawa katika mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Mwasengwa na kwa kuwa Serikali mwaka 2009/2010 iliiandikia barua Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuwa imiteitengea milioni 900 kwa ajili uchimbaji wa bwawa la Mwasengwa na mpaka hivi ninavyoongea hakuna hata shilingi moja ambayo imekwishafika katika Halmashauri ya Shinyanga.

Je, ni lini sasa pesa hizi zitafika ili bwawa liweze kuchimbwa? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji yanayopotea; kama nilivyosema, maji ambayo yanatiririka juu ya ardhi, mpango wetu ni kuyavuna kwa kujenga mabwawa. Nimesema na ninadhani pia nitakuwa ninajibu na swali la pili kwamba, tumejiwekea katika Mpango wa Maendeleo, ambao tumeupitisha wa Miaka Mitano, kujenga mabwawa 33. Katika Mpango mzima wa Kilimo, tumejipangia shilingi trilioni 2.3, alisilimia kubwa ya fedha hizi itaelekezwa katika kuvuna maji yanayotiririka juu ya ardhi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango wa kujenga bwawa hili la Masengwa utatekelezwa kama tullivyojipangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya pili, ambayo alisema fedha ambazo ziliahidiwa hazikufika, ninaomba baadaye kidogo niwasiliane nae njue ilikuwa lini. Kwa sababu, kama tuliahidi halafu fedha hazikupelekwa, hakukuwa na sababu tena ya kuanza Miradi mingine kabla hatujakamilisha ahadi; nitapeleleza njue kulikoni.

Na. 173

Kujenga Barabara na Madaraja Kondo

MHE. MOZA A. SAIDY aliuliza:-

Pamoja na juhudi za Serikali kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika maeneo mbalimbali, bado Serikali imechelewesha maendeleo katika Wilaya ya Kondo kwa kutojenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Dodoma – Kondo – Babati hadi Arusha na kutojenga madaraja muhimu ya Kolo na Munguri:-

Je, Serikali itaijenga lini Barabara hiyo kwa kiwango cha lami na changarawe na kukarabati madaraja hayo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa kifupi sana, ninaomba kuwapongeza Wananchi wa Kigoma, kwa matukio ya kihistoria mkoani mwao leo na kesho; ya ufunguzi wa barabara ya lami toka Mwandiga kwenda Manyovu, kilometra 60 na uzinduzi wa ujenzi wa barabara ya pili ndefu ya lami kutoka Kidahwe kwenda Uvinza, kilometra 76.6 na uzinduzi wa ujenzi wa Daraja la Malagarasi na barabara zake mbili, zenyet urefu wa kilometra 48 za lami na shughuli zote hizi zitasimamiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye chini yake tunadhamiria kubadilisha sura ya Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Kondo – Babati hadi Arusha, zenyet urefu wa kilometra 261 umeanza na utafanyika kwa awamu. Kwa kuanzia, tayari ujenzi wa sehemu ya Dodoma – Mayamaya, zenyet urefu wa kilometra 43 na sehemu ya Bonga – Babati zenyet urefu wa kilometra 19.2 umeanza. Katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012, Serikali imepanga kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki ya Mayamaya – Bonga, zenyet urefu wa km. 198.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Ninapenda kuuliza swalii moja la nyongeza.

Daraja la Kolo linalounganisha Dodoma na Arusha lilikatika mwaka 1998 ambalo na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wasafiri. Je, Serikali italijenga lini Daraja hilo ili kuwapunguzia usumbufu Wananchi unaowakabili? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa barabara hii, tunatarajia kujenga madaraja mapya matatu na tayari Mkandarasi ameshaanza ujenzi wa daraja la kwanza na vilevile makalavati 50 na sasa hivi tumeshajenga makalavati 38. Kwa hiyo, ategemee kwamba, kwa sababu madaraja hayo ni sehemu ya Mradi huu, yatajengwa tu.

Na. 174

Hitaji La Bumps – Uyole Kati

MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. JOSEPH O. MBILINYI) aliuliza:-

Matukio mengi ya ajali hutokea katika eneo la Uyole Kati na kona ya Barabara Kuu ya Uyole – Kyela, hivyo kusababisha vifo vya watu wengi:-

Je, ni lini Serikali itasikia kilio cha wakazi wa eneo hilo na kuweka *Road Bumps* ili kupunguza mwendo kasi wa magari makubwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Uyole Kati lipo katika Barabara Kuu ya Uyole – Kasumulu, umbali wa kilometra moja kutoka makutano ya Barabara Kuu ya *TANZAM* na Barabara Kuu ya Uyole – Kasumulu; ni kweli kuwa, katika eneo hili kuna kona na mahali hapo ajali nyingi hutokea. Hali hiyo ililazimu uchunguzi ufanyike, ambao umebaini kuwa, ajali nyingi katika eneo hilo husababishwa na madereva wasioheshimu au kuzingatia sheria na alama za barabara za kudhibiti mwendo kasi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii isiyoridhisha na upekee wa barabara hii, kwani inaunganisha nchi yetu na nchi jirani za Malawi na Zambia; hivyo kutumiwa na madereva wenye usoefu na uelewa unaopishana, Serikali kwa ushauri wa wataalamu wake, imejipanga kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la ajali eneo la Uyole katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya matuta nayo yamekuwa yakisababisha ajali na kuharibu magari; na kwa kuwa haijulikani ni chombo kipi kinasimamia uwekaji wa matuta barabarani; je, Serikali inaweza

ikaliambia Bunge kwamba ni chombo gani kinasimamia hayo matuta na hayo matuta yanapaswa yawe ni ya viwango vya namna gani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swal la msingi, Mheshimiwa Mbunge, alikuwa anaomba tujenge matuta. Kama nilivyosema, tunalifanyia kazi kwa maana ya kwamba, Serikali itafanya kile ambacho wataalamu watatushauri. Siyo lazima tujenge matuta, tunaweza kuweka *lambo strips*, tunaweza kuweka *diversion, bypass* au taa za barabarani.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nisisitize kwamba, Serikali inapoamua kujenga Barabara Kuu, haitazamii kujenga matuta kila baada ya hatua kadhaa. Kwa sababu, inapojenga barabara inaweka na alama za kumsaidia dereva au mtumiaji yeote wa barabara, kuweza kuziheshimu ili kuzuwigia ajali. Pale ambapo alama hizi zinashindikana kuepusha ajali, ndipo ambapo Serikali inafanya *intervention* inachukua hatua za ziada kujenga matuta, kuweka taa na kuweka vitu kama hivyo. Chini ya Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 na chini ya Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hiyo, zilizopitishwa mwezi Mei mwaka jana, Mamlaka ya kuamua ni wapi tuweke matuta, yapo chini ya Waziri wa Ujenzi na ambaye ataweka *specification* ya matuta hayo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kunikumbusha. Matuta yote nchini sasa yatakuwa na *specification* maalum, siyo kama sasa ambapo wengine kwa kweli ni matuta kabisa ya kupandia viazi na mengine yanatofautiana. Kwa hiyo, yatakuwa *standard*. Ahsante sana.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swal la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swal langu bado lipo kwenye swal la msingi.

Kwa kuwa Barabara Kuu ya Mbeya ndiyo inayokwenda katika nchi nyingi sana za Kusini mwa Afrika. Je, Serikali inaweza ikatoa tamko gani kama Barabara hii ya Uyole inaweza ikacheppuliwa kwa ajili ya kuepuka ajali na vifo vingi ili iweze kutokea Mbalizi; na kama ni kweli ni lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninaomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Mary Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tatizo la ajali sehemu ya Uyole – Mwanjelwa, tunalifanyia kazi na Wataalamu watatushauri tufanye nini katika Mwaka huu wa Fedha; kama ni kujenga matuta, kama ni kuweka *bypass, diversion* au taa, wao ndiyo watakaotushauri.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inajiandaa kulifanyia kazi tatizo hilo, sehemu ya Uyole, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wa Mkoa wa Mbeya, wawashauri wapiga kura wao walioko eneo la Uyole, ambao wamegeuza sehemu ya hifadhi ya barabara kuwa sehemu ya kuuzia nyanya mpaka *CD* za muziki, kwa kufanya hivyo tumefikia mahali ambapo kwa kweli sisi wenyewe tunakaribisha ajali nyingi zaidi katika hiyo barabara.

SPIKA: Ninashukuru sana. Muda umekwisha na maswali pia yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni waliokaa katika eneo la *Speaker's Gallery* na makundi. Kwanza kabisa, ninaye Mume wake Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Hawa Ghasia, jina hawakusema; lakini ni mumewe na familia; ninaomba wasimame hapo na familia. Mheshimiwa Yahya, alikuwa anafanya Ubalozi, ninafikiri amerudi na familia yake. (*Makofi*)

Nina Watendaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Ninawataja hao kwa sababu na ninyi mnatakiwa muwajue. Kwanza kabisa, yupo Katibu Mkuu, Utumishi, Ndugu George Yambesi, ndiyo Katibu Mkuu wa huko. Halafu Naibu Katibu Mkuu, Utumishi, Ndugu Habu Mkwizu; asante sana. Yupo Katibu Mkuu Ikulu, Ndugu Phanuel Mbonde na yupo Naibu Katibu Mkuu, Ikulu, Ndugu Kidata. Yupo pia Mkurugenzi wa TAKUKURU, Dokta Edward Hosea; angalau wewe tunakujuu vizuri; mshangilieni mnjamua. (*Makofi*)

Yupo Mratibu wa MKURABITA, Injia Salema; hongera kwa kufanya vizuri na kupata Award ya *United Nations* katika Afrika kwenye suala la Uratibu; mimi ndiyo Mwenyekiti wake. Haya, kuna Mkurugenzi wa TASAF, Ndugu Ladislaus Mwamanga, ahsante; hongera kwa kupata nafasi hiyo. Yupo Bi. Mpangala, Mkurugenzi wa Tume ya Utumishi wa Umma, ahsante sana na kuna Mheshimiwa Jaji Salome Kaganda, huyu mniamfahamu vizuri; mshangilieni sasa! Kwa hiyo, mwaka huu mtapeleka fomu mapema kabisa bila kukosea. Hongera sana mama, umeamsha mori na watafanya vizuri sasa. (*Makofi/Kicheko*)

Tuna wanakwaya 45 wa KKKT Usharika wa Kijenge, Arusha. Ninaomba wasimame walipo. Ahsante sana, hongera sana, karibuni.

Tuna Wanafunzi 95 wa Shule ya Msingi Mgulani, Dar es Salaam, ninadhani, wasimame walipo na walimu wao kama wapo; Asante sana. Tunashukuru walimu mmewaleta watoto kutoka Dar es Salaam kuja kuona shughuli za Bunge hapa. Halafu tuna wanafunzi 44 na walimu saba wa Shule ya Msingi Buigiri Mission, ninafikiri karibu hapa Dodoma; wako wapi hawa? Ahaa, ahsante sana, karibuni sana na walimu tunawashukuru kwa kuwaleta watoto hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna shughuli nyingine za kazi; Mheshimiwa John Mnyika, yeye ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo tarehe 4 Julai, 2011 saa tisa kamili alasiri, kutakuwa na Kikao kwenye Ukumbi Namba 231. Mkurugenzi Msaidizi wa

Shughuli za Bunge, anaomba niwatangazie kwamba, kufuatana na zoezi la... *Okay*, hii inanihusu mimi, ngoja niwatangazie kwanza hii.

Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie kwamba, Kamati ya Uongozi ya Bunge, itakuwa na Kikao leo Jumatatu, saa saba kamili mchana. Hii ni Kamati ya Uongozi; Wajumbe wake ni Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge na Makamu wao pale Wenyeekiti wanapokuwa hawapo; ni Kikao muhimu kwa sababu tunajaribu kuangalia namna ya kuingia kwenye Kamati ya Matumizi hasa tunapofikia kwenye vifungu. Kwa sababu inaonekana nia ya Wabunge wengi kuchangia wakati ule ni kubwa na muda wetu ni mdogo na kwa mtindo huu, tutakuwa tuna *guillotine* kila wakati, kitu ambacho tunaweza kuangalia utaratibu. Kwa hiyo, ninaomba Wenyeviti msikose kuhudhuria na pale Mwenyeekiti anapokuwa hayupo, basi Makamu wake.

Tangazo lingine ni kwamba, ninawashukuru Wabunge wengi mlibandika vikaratasni na vyuma kwenye majina yenu pale mnapotaka kukaa, sasa vya kudumu vimebandikwa mahali fulani. Imedhihirika kwamba, walipokuwa wanaandika huko, kuna *mistakes* za majina yenu, *spelling mistakes*, kwa wengine. Tunaomba wale ambao wanafikiria kuna *spelling mistakes* kwenye majina yao, bandikeni hapo hapo majina yenu kamili yanavyotakiwa yaandikwe ili anapopita pale aweze kuunganisha. Tutatoa ile *glue* ya kuweka. Andika jina linavyotakiwa liwe na ikiwezekana kama lilivyo kwenye *ID* yako ile ya kuingilia. Kwa sababu, usipofanya hivyo tena, unatubadilishia majina. Fanya kama ilivyo kwenye *ID* yako ya kuingilia, ubandike pale. Ambao hawana vibandiko, tunaamini kwamba ni sahihi walivyoandika majina yao. Hawa vijana wa mezani hapa watapita watawagawieni hizo kusudi mbandike tukamilishe zoezi hili. Mkishaweka majina, tunaomba mkae hapohapo kila siku, inatusaidia sisi kuwafahamu vizuri na kuwataja kwa majina yenu kwa mujibu wa taratibu zetu. Kwa hiyo, ninaomba mfanye hivyo kwa ushirikiano kusudi tuweze kuchapa orodha ya mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, ninashukuru.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika, kwa maneno niliyosema?

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, hapana.

SPIKA: Enhee, tunaongoza nini na tulikuwa *weekend*?

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), ambayo inasema: “*Halikadhalika Mbunge, anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe usafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na Majibu ya Spika yatatolewa hapohapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa.*”

SPIKA: Hili lilitokea lini; leo?

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, Ijumaa. Wakati tunaendelea na Kamati ya Bunge Zima kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu, niliomba ufanuzi na Kauli ya Serikali, kwa nini mzani unaopimia Zao la Pamba ambao ulipigwa marufuku kwenye Bunge la Tisa, ukaharamishwa na wafanyabiashara wakatakiwa wawe na mzani mwingine wa *solter*. Nikaomba ufanuzi ni kwa nini mzani huu ambao uliharamishwa tarehe 20 Juni, wakati msimu wa pamba umefunguliwa unaendelea kutumika na kuwanyonya wakulima?

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, alisema kwamba, msimu wa kununua pamba katika nchi hii bado haujaanza na kwamba, wahusika wanafundishwa mzani ili waweze kuutumia wakati msimu utakapofunguliwa. Taarifa nilizonazo, msimu wa pamba ulianza tarehe 20 mwezi Juni.

SPIKA: Mwongozo unatakiwa uwe mfupi, unataka nikwambie nini? Nifanyeje katika mazingira haya?

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, ambayo msimu ulishaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, alisema kwamba, msimu bado; nilikuwa ninaomba Mwongozo wako, nifanye nini na wakati wakulima kule wanaendelea kunyonywa na mzani ambao ni batili.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, huo Mwongozo siyo sahihi kabisa. Sasa utatumia kifungu cha 50 cha Kanuni zetu, ambapo utapata muda wa kueleza hayo. Tunapopata Mwongozo kuzungumza baada ya Spika kuahirisha Bunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 50 ama ya 28, ninafikiri (4), inabidi ulete kitu ambacho hakina ugomvi wala hakimgusi mtu. Kama hii ya kwako ungeiandika vizuri, hapo tunakupa ruhusa wakati wa *adjourning motion, una-make statement* yako.

Nimepata maombi ya namna hiyo kwa wengine, lakini unakuta anataka kuongea *during adjournment motion*, lakini hapa atadonoa huyu, atadonoa kule, atadonoa na wengine, hiyo haikubaliki. Wewe eleza tu kilichokuudhi au unachokitaka kiwe, halafu sisi tutakusikia. Kwa hiyo, hii unaweza kuifanya wakati huo. Soma vizuri, ninafikiri kifungu cha 50(1).

Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Kaimu.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI - KAIMU KIONGOZI WA SHUGHULI ZA SERIKALI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, inawezekana kuna tatizo na Serikali yetu ina utamaduni wa kuangalia hasa pale inapoonekana kwamba, kumetokea kasoro au inaathari kwa Wananchi. Ninaliambia Bunge kwamba, badala ya yeye kuhangaika na Kanuni ya 50, tutachunguza kwa haraka sana ili kama ipo kasoro kama alivyoieleza, iweze kurekebishwa mara moja. Kwa sababu

Serikali ya CCM haiwezi kusimama hapa kuruhusu wakulima wetu wanyonywe. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa walioandika majina ya kutambulisha wageni muhimu wengine waliwaacha; yupo Ndugu Jovin Kitambi, yeze ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, ninadhani yupo hapa; yupo na Prof. Semboja, yeze ndiyo Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, yuko hapa, ahsante sana, karibu sana, ninaona hatukupewa majina. Tunaendelea Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora), pamoja na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; mtoha hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA): Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bungeni lako na Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu - Fungu 20 na 30, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Fungu - 32, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma - Fungu 33, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - Fungu 67 na Tume ya Utumishi wa Umma - Fungu 94, Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitia Makadirio ya Ofisi za Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii, kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Makamu wake, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa 2011/2012, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi alioupati katika Uchaguzi Mkuu wa 2010, kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Kuchaguliwa kwake ni ishara ya imani ya Wananchi wa Tanzania kwa Uongozi wake na Chama Tawala, kwani ameiongoza nchi kwa amani, utulivu na mafanikio zaidi tangu alipochaguliwa kushika wadhifa huo. (*Makofî*)

Katika uongozi wake, ametekeleza yale aliyoahidi kwa Wananchi wakati wa uchaguzi na mengi yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Aidha, Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia na kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia na Mapambano Dhidi ya Rushwa kwa mafanikio makubwa. Mafanikio yaliyopatikana chini ya Uongozi wake, yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini na Washirika wa Maendeleo kuona haja ya kuendelea kutuunga mkono. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika Uongozi wake ili aendelee kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Billal, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais. Ninampongeza pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi, kwa kuteuliwa kwake kuendelea kuongoza shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kuteuliwa kwake, kumedhihirisha umahiri wa utendaji wake katika kipindi cha awamu iliyopita. Aidha, Hotuba aliyoitoa mbele ya Bunge lako Tukufu wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012 ni kielelezo cha uzoefu wake katika Uongozi ambao umeonesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Kilosa na Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake ambayo imeainisha misingi na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Mbunge wa Bunda na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa Hotuba yake kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikupongeze wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kwako kushika wadhifa wa Spika wa Bunge, ukiwa mwanamke wa kwanza katika Historia ya Bunge letu la Tanzania. Kuchaguliwa kwako ni ishara ya imani kubwa waliyo nayo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, utaliongoza Bunge letu Tukufu, kwa busara na hekima. Ninampongeza pia Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii, kutoa pole kwa wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, ninatoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa kufiwa na mama yako mzazi; Marehemu Emilia Tulakela Samnyuha; Mwenyezi Mungu, awape moyo wa subira na azilaze peponi roho za marehemu. *Amina.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninaomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushindi walioupata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Hii inaonesha imani kubwa kutoka kwa Wananchi waliowachagua kuwa watawawakilisha vyema katika Bunge hili. Aidha, ninaomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais; ninaamini kuwa mchango wao utaongeza ufanisi wa Bunge lako katika kuwatumikia Wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Mathias Meinrad Malome Chikawe (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuandaa na kukamilisha Hotuba hii. Aidha, ninamshukuru Bwana Phillemon Lutangilo Luhanjo, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Fanuel Eusebius Mbonde, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; na Bwana George Daniel Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma). Aidha, ninapenda kuwashukuru pia Bwana Alphayo Japani Kidata, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Ikulu); Bwana HAB Mkwizu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma); Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais; Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Taasisi zake, ambao wamefanya kazi kubwa katika kuwezesha Hotuba hii kukamilika.

Ninapenda nitumie fursa hii pia kuwashukuru Viongozi na Wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Mikoa na Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma, kwa ushirikiano na michango yao iliyowezesha kuandaa Hotuba hii. Ninawashukuru pia Wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini, ambao kwa mara nyingine wamenichagua kuwa mwakilishi wao Bungeni na pia kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo. Ninapenda kuwaahidi kwamba, sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninapenda kuzishukuru Nchi na Washirika wa Maendeleo mbalimbali, ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio mbalimbali tuliyyoyapata. Hivyo, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuzishukuru Nchi na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yafuatayo: Australia, China, Finland, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Malaysia, Misri, Norway, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Marekani, Ireland, Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japani (*Japanese Social Development Fund*), CIDA (Canada), DANIDA, DFID, JICA, NORAD, OPEC, SIDA (Sweden), UNDP, UNIDO, UNFPA, USAID, GIZ na KOICA.

Mheshimiwa Spika, Hotuba yangu itazungumzia maeneo manne ambayo ni: Mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha Miaka 50 ya Uhuru; utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha 2010/2011; Mpango wa Kazi na maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango huu kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kama wengi wetu tunavyofahamu, mwaka huu wa 2011, Tanzania Bara inatimiza miaka 50 tangu tupate Uhuru tarehe 9 Desemba, 1961. Huu ni mwaka wa kukumbukwa kwa Watanzania wote. Ikumbukwe kuwa, mara baada ya uhuru, Tanzania Bara ilikabiliwa na maadui wakuu watatu, ambao ni ujinga, umaskini na maradhi. Katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru, Serikali imepata mafanikio mengi katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya awali yalianza kuonekana pale Tanganyika ilipokuwa Jamhuri tarehe 9 Desemba, 1962, ambapo mamlaka ya uendeshaji wa nchi yaliwekwa mikononi mwa Waafrika. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikuwa Rais

wa Kwanza wa Tanganyika huru, akiwa pia Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu. Aidha, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliofanyika tarehe 26 Aprili, 1964 uliwezesha kupatikana kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano huu ni moja ya mafanikio makubwa ambayo hayawezi kusahaulika katika maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Muda ya Tanzania ya Mwaka 1965, ambayo iliandikwa upya mwaka 1977 na kuitwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na marekebisho yake yaliyofanyika mwaka 1984 ambayo yalitambua na kujumuisha Haki za Binadamu, jambo ambalo ni kati ya mafanikio ambayo yaliijengea heshima Tanzania kwa kuweka misingi bora na imara ya uendeshaji wa nchi. Katiba hii inaweka wazi utaratibu mzima wa uendeshaji wa nchi na kuwepo kwa Mihimili Mikuu ya Dola ambayo ni Serikali Kuu, Bunge na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ambayo awali ilikuwa inaongozwa kwa Mfumo wa Chama Kimoja cha Siasa, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Hata hivyo, kufuatia vuguvugu la mageuzi ya kisiasa lililosuhudiwa na dunia mwanzoni mwa miaka ya 80 na mwishoni mwa miaka ya 90, Tanzania ilifanikisha kufanya mageuzi kwa kukubali kufuata mfumo wa Vyama Vingi kwa utulivu bila umwagaji damu, tofauti na ilivyojitokeza kwa nchi nyingine hususan za Ulaya ya Mashariki na zile za Afrika. Katiba ilirekeblishwa hapo mwaka 1992, ambapo Tanzania ilitangazwa kuwa nchi yenye kufuata Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Uchaguzi wa kwanza uliohusisha Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa ulifanyika mwaka 1995 kwa amani na utulivu; utaratibu ambao umeendelea kufuatwa na hivyo kuifanya demokrasia nchini kuendelea kushamiri.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeweza kujenga Taasisi za Kidemokrasia kwa ajili ya kulinda misingi ya Utawala Bora. Kati ya Taasisi zilizoanzishwa miaka michache ya Uhuru ni Kikosi cha Kupambana na Rushwa kilichoanzishwa mwaka 1975 kwa Sheria Na.16 ya Mwaka 1971, kikiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Baadaye mwaka 1991 kilibadilishwa kuwa Taasisi ya Kupambana na Rushwa. Kutokana na Taasisi hii kujumuisha pia masuala ya kuzuia na kupambana na rushwa, Taasisi ilibadilishwa jina na kuitwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa Sheria Na.11 ya Mwaka 2007. Kwa sasa, TAKUKURU imefanikiwa kushirikisha makundi ya jamii katika mapambano dhidi ya Rushwa na inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji (NACSAP).

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398, ilitungwa ambapo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilianzishwa ili kusimamia mienendo na maadili ya Viongozi wa Umma. Katika utekelezaji wa Sheria hii, Sekretarieti ilianza kazi ya kuhakiki Matamko ya Rasilimali, Maslahi na Madeni ya Viongozi wa Umma, ambayo hujazwa kwenye Fomu za Tamko kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Baraza la Maadili lilianzishwa likiwa na jukumu la kisheria la kufanya uchambuzi wa kina wa malalamiko ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma. Hadi sasa jumla ya Viongozi wa Umma 23 wameitwa mbele ya Baraza la Maadili na kuhojiwa. Kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Maadili, kumejenga na kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na Taasisi zinazohusika na Utawala Bora ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya umaskini ni moja ya shughuli muhimu zilizofanywa na Serikali kwa mafanikio tangu Uhuru. Serikali ya Tanzania, katika jitihada za kupambana na umaskini ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), mnamo mwaka 2000 kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa kijamii na fursa za kiuchumi kwa kuzingatia viashiria vya Malengo ya Maendeleo ya Milenia kama vilivyoainishwa katika Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA). Mfuko huu umewezesha jamii kuibua na kutekeleza Miradi 11,955, yenye lengo la kupunguza umaskini na kuboresha huduma za jamii. Aidha, kuanzishwa kwa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), mwaka 2004, kinalenga kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Umiliki wa Rasilimali. Jumla ya Wananchi 13,123 wamekwishapatiwa hatimiliiki na baadhi yao wametumia kujipatia mikopo ya kibenki.

Tanzania imeendelea kujenga uhusiano na ushirikiano na Mataifa ya nje; ilikuwa mstari wa mbele katika ukombozi Kusini mwa Afrika. Ushiriki wa Tanzania katika ukombozi uliwezesha nchi zote za Kusini mwa Afrika kukombolewa kutoka mikononi mwa wakoloni na ubaguzi wa rangi. Miongoni mwa nchi hizo ni pamoja na Botswana, Namibia, Msumbiji, Angola, Afrika Kusini na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama wa Nchi ni jukumu lililotekelawa na Serikali ya Tanzania kwa ufanisi mkubwa. Aidha, umoja na mshikamano wa Watanzania, umeendelea kuimarishwa na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kuigwa kwa kuwa nchi ya amani na utulivu. Hali hii imesaidia kudumisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utumishi wa Umma, Serikali ilikuwa na jukumu la kuunda mfumo mpya wa utawala kwa kuhakikisha inaweka mikakati ya kubadilika kutoka kwenye mfumo wa Utumishi uliokuwepo wa Serikali ya Kikoloni na kuwa Utumishi mpya wa kujenga Taifa jipya la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma hii, hatua mbalimbali zilichukuliwa zikiwemo kuwakabidhi wazalendo madaraka na ajira, *Africanization*, ili waweze kuwahudumia Wananchi; kuanzishwa kwa taasisi za mafunzo ambazo ziliongeza uwezo wa watumishi waliokuwepo kazini na wapya waliokuwa wanatoka shulenii ili kupata wataalam zaidi; kuanzishwa kwa Mpango ya Rasilimali ambayo lengo lilikuwa ni kuuwezesha Utumishi wa Umma kujitosheleza kwa wataalam; kuanzisha Jeshi la Kujenga Taifa, ambalo lengo lake lilikuwa kuimarisha ukakamavu, ulinzi, ari ya ujenzi wa Taifa, umoja wa Kitaifa na uzalendo mionganii mwa Watumishi wa Umma; kumiliki njia kuu za uchumi kwa kuziweka mikononi mwa Wananchi kuititia Azimio la Arusha; na kuanzisha mageuzi ya kiuchumi na Programu za Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Programu za Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma, zililenga kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kwa kupunguza ukubwa wa Serikali na gharama za uendeshaji; kuweka mifumo ya kiutendaji na kimenejimenti ili kuwa na utendaji wenye kujali matokeo ya kazi; kuongeza uwajibikaji na usikivu wa

watumishi wa umma; kuimarisha utendaji kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mapambano dhidi ya Rushwa, kuimarisha utoaji wa huduma za jamii na usimamizi wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Programu hizi za Mabadiliko katika Utumishi wa Umma ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuwa na mfumo shirikishi wa taarifa za watumishi na orodha ya malipo ya mishahara (*Integrated Human Resource & Payroll Management System*), ambao unarahisisha usimamizi na upatikanaji wa taarifa za kiutumishi wakati wa kufanya maamuzi na unasaidia kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa ulipaji wa mishahara na kuimarisha udhibiti dhidi ya watumishi hewa;

(ii) Kuwepo kwa mifumo ya utendaji kazi katika Taasisi za Umma inayolenga kuongeza uwajibikaji na hivyo kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi. Mifumo hii ni pamoja na: matumizi ya mipango mkakati, mipango ya mwaka, mikataba ya kazi, upimaji wa wazi wa utendaji kazi (*OPRAS*), mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, mikataba ya huduma kwa mteja na mfumo wa kushughulikia malalamiko ya Wananchi;

(iii) Kuongezeka kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma. Hii imerahisisha mawasiliano na upatikanaji wa baadhi ya huduma na taarifa ndani ya Serikali kwa kuitia mifumo ya kompyuta na tovuti;

(iv) Serikali imeweza kupunguza majukumu ambayo siyo ya msingi katika utendaji wake. Hatua hii, imeifanya Serikali kuweka utaratibu wa kukabidhi majukumu hayo ili yafanywe na Sekta Binafsi au Wakala wa Serikali;

(v) Kubadili mfumo wa usimamizi wa Rasilimaliwatu kwa kupeleka madaraka ya kuajiri, maendeleo ya watumishi na kusimamia nidhamu kwa waajiri wenyewe tofauti na ilivyokuwa awali. Ili kuhakikisha kwamba, waajiri wanatekeleza majukumu yao kwa misingi sahihi, Tume ya Utumishi wa Umma ilianzishwa na kupewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika usimamizi wa Rasilimaliwatu. Aidha, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeanzishwa ili kuwasaidia waajiri kupata watumishi wenyewe sifa;

(vi) Kuimarisha taratibu za upatikanaji wa watumishi wa kutosha na kuwaendeleza kwa kuanzisha matumizi ya mipango ya Rasilimaliwatu, matumizi ya mipango ya mafunzo na mipango ya kurithishana madaraka; na

(vii) Kupanua huduma za kijamii na kiuchumi katika Sekta za Elimu, Afya, Maji na Miundombinu na kuzisogea karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanzisha na inaendelea kuboresha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo Mifuko ya Pensheni ya Watumishi wa Umma, Watumishi wa Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Watumishi wasio na ajira ya Masharti ya

Kudumu – *GEPF* na *NSSF*. Mifuko hii ya Jamii imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya Watumishi wa Umma, wanapohitimisha utumishi wao. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa ajili ya Kuboresha huduma ya Afya kwa Watumishi wa Umma pamoja na kuipunguzia serikali gharama za matibabu kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Rais (Ikulu), imeendelea kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Rais na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Rais (Ikulu), imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu wa Taasisi zilizo chini yake, ambazo ni TAKUKURU, MKURABITA, TASAF na Mfuko wa Rais wa kujitegemea. Kazi nyingine zilizotekelizwa na Ofisi ya Rais (Ikulu), pamoja na Taasisi zake ni kama zinavyooneshwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa 16 hadi ukurasa wa 33.

- (i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo mbalimbali kama vile uchumi, siasa, jamii, sheria na uhusiano wa kimataifa;
- (iii) Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, ilifanya vikao 37 na kuchambua Nyaraka 58. Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*Inter Ministerial Technical Committee - IMTC*), ilifanya Vikao 29 na Nyaraka 30 zilichambuliwa. Baraza la Mawaziri lilifanya vikao 13 na Nyaraka 25 zilijadiliwa na kufanyiwa uamuzi. Aidha, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu ilifanya Vikao vya Kazi vitatu na Kamati ya Katiba, Sheria na Bunge (KB) ya Baraza la Mawaziri ilifanya Vikao vinne na kuchambua Miswada ya Sheria sita na Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama ilifanya kikao kimoja na Hati nne zilijadiliwa;
- (iv) Mafunzo ya Utawala Bora na Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa yalitolewa kwa washiriki 100 kutoka Wizarani, Wakala wa Serikali na Idara Zinazojitegemea, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Utumishi wa Mikoa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, washiriki 60 wa Kamati za Utawala Bora za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walipatiwa mafunzo ya Utawala Bora;
- (v) Rufaa 80 za Watumishi wa Umma zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Rais kwa uamuzi. Aidha, Malalamiko 350 yalichambuliwa na kutolewa maelekezo na Rais au Katibu Mkuu Kiongozi;
- (vi) Kesi 11 za madai dhidi ya Uamuzi wa Rais au Katibu Mkuu Kiongozi zilizofikishwa Mahakamani zilitolewa utetezi na ziko katika hatua mbalimbali. Mchanganuo wa kesi hizo ni: Tanga moja, Dar es Salaam moja, Mwanza moja, Dodoma moja, Mbeya nne, Iringa mbili na Arusha moja;

(vii) Mwongozo wa Baraza la Mawaziri, Waraka wa Rais Na. 1 wa 2005, Mwongozo wa Kutayarisha na Kusambaza Nyaraka za Baraza la Mawaziri, Mwongozo wa Mikutano ya Makatibu Wakuu na Mwongozo wa Mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilihuisha;

(viii) Taarifa za Utekelezaji wa Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Taarifa hizo zilihusu maboresho yanayoendelea katika Sekta ya Utumishi wa Umma, Serikali za Mitaa, Usimamizi wa Fedha, Mazingira ya Biashara, Sekta ya Kilimo, Sekta ya Sheria na Mapambano dhidi ya Rushwa;

(ix) Taarifa ya utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni, Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 (2000 – 2010) na Mwelekeo wa Sera za CCM kipindi cha 2010 – 2020 ziliandaliwa;

(x) Ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Chamwino, kwa maana ya ukarabati wa Jengo la Mapokezi, Utawala na Makazi ya Rais umekamilika. Nyumba ya Makazi ya Katibu Mkuu Kiongozi, Ikulu Ndogo za Tabora na Tanga zimefanyiwa matengenezo na ujenzi wa Jengo la Utawala umekamilika;

(xi) Mitambo ya kufua ubaridi (*chillers*) imefanyiwa matengenezo na jenereta mpya imenunuliwa baada ya iliyokuwepo kuharibika;

(xii) Mikutano mitano iliyoshirikisha Viongozi wa Dini mbalimbali ilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Kagera. Katika mikutano hiyo, masuala ya usalama, amani, uwajibikaji na mchango wa Taasisi za Dini katika maendeleo ya Taifa yalijadiliwa kwa kina; na

(xiii) Uratibu wa Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (*MKURABITA*) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ulifanyika. Uratibu huu unafanyika ili kuhakikisha kuwa, Miradi hiyo inainua kipato cha Wananchi hususan Makundi Maalum kama vile vijana, wazee, wanaoishi na virusi vya UKIMWI na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329, jukumu kubwa la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*) ni kuelimisha umma juu ya rushwa na athari zake katika jamii na mbinu za kupambana na rushwa nichini, kuchunguza tuhuma mbalimbali na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria wale wanaojihusisha na vitendo vya rushwa. Aidha, jukumu lingine la *TAKUKURU* ni la kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, kazi zilizotekeliza ni pamoja na:-

(i) Tuhuma 2,258 zilichunguzwa ambapo tuhuma 598 uchunguzi wake ulikamilika. Kati ya tuhuma ambazo uchunguzi wake ulikamilika, tuhuma 250

zilifungwa kwa kukosa ushahidi, tuhuma 80 zilifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali na tuhuma 92 zilihamishiwa kwenye Idara nyingine za Serikali baada ya ushahidi wake kutoshabihiana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Aidha, tuhuma 21 zilitolewa mapendekezo na kuchukuliwa hatua mbalimbali na tuhuma 155 zilifunguliwa mashtaka Mahakamani;

(ii) Kesi 399 ziliendeshwa Mahakamani na jumla ya kesi 103 zilikamilika. Kati ya kesi zilizokamilika, kesi 48 watuhumiwa walitiwa hatiani na kuadhibiwa na kesi 55 watuhumiwa hawakupatikana na hatia na hivyo kuachiwa huru;

(iii) Jumla ya kesi 13 zinazowahuju wanasiasa na wagombea wa nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 zilifikishwa Mahakamani. Kesi mbili watuhumiwa wake hawakupatikana na hatia na kesi 11 zipo katika hatua mbalimbali;

(iv) Tafiti mbili kuhusu mianya ya rushwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na katika uendeshaji wa Mkoa wa Morogoro zilifanyika. Utafiti katika usimamizi wa vocha za pembejeo unaendelea katika mikoa sita ya Iringa, Morogoro, Kigoma, Mwanza, Kilimanjaro na Lindi;

(v) Klabu 821 za wapinga rushwa zilijengewa uwezo, 384 zilianzishwa na midahalo 83 kuhusu masuala ya rushwa ilifanyika kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari na Vyuo. Aidha, mikutano ya hadhara 1,701 ambayo iliwashirikisha Wananchi mbalimbali ilifanyika;

(vi) Watumishi 122 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma, Rukwa, Lindi, Mtwara, Kilimanjaro na Tanga walipatiwa mafunzo kuhusu masuala ya rushwa na miundombinu ya maadili, kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukabiliana na vitendo vya rushwa katika maeneo yao ya kazi. Vilevile Wafanyabiashara 58 kutoka Mikoa ya Mtwara, Lindi, Dodoma, Kigoma na Shinyanga walipata mafunzo ya utawala wa Kampuni. Aidha, Wananchi 422 wakiwemo Wanawake, Vijana, Vyama vya Dini na Asasi za Kiraia, walipatiwa mafunzo juu ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya Mwaka 2010 na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329;

(vii) Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha na ubora ulifanyika kwenye Miradi 4,520, yenye thamani ya shilingi bilioni 139.8. Kati ya Miradi hiyo iliyofanyiwa ukaguzi, miradi 422 ya thamani ya Shilingi bilioni 14.5 ilibainika kuwa na kasoro. Aidha, jumla ya majalada ya uchunguzi 253 yalifunguliwa na kiasi cha Shilingi milioni 679.11 kimeokolewa na kesi 16 kuhusu fedha za miradi zimefunguliwa Mahakamani; na

(viii) Ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Manyara na Lindi na Wilaya za Mpanda na Iramba umekamilika. Aidha, ujenzi wa Ofisi za Mkoa wa Pwani na Wilaya za Misenyi na Newala umeanza na unatarajiwa kukamilika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), ulianza mwaka 2004 na ulipangwa kutekelezwa

katika awamu nne ambazo ni Tathmini ya Sekta Isiyo Rasmi, Maandalizi ya Maboresho, Utekelezaji wa Maboresho na Ukuzaji wa Mtaji na Utawala Bora. Jukumu kubwa la MKURABITA ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Umiliki wa Rasilimali. Katika mwaka wa 2010/2011, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, ulitekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mpango kama ifuatavyo:-

(i) Vikosi Kazi vilivyoundwa kati ya MKURABITA na Wizara husika za Kisekta kwa ajili ya kujadili maboresho yaliyohusu ardhi na biashara viliendelea na kazi zake na hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

- Kikosi Kazi kati ya MKURABITA na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kilikamilisha kazi na maboresho ya sheria yaliyokubalika yamewasilishwa kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria. Maboresho ambayo yalionekana kuhitaji kazi zaidi yanaendelea kushughulikiwa;

- Kikosi Kazi kati ya MKURABITA na Wizara ya Viwanda na Biashara kimemaliza kazi na mapendekezo ya sheria yaliyokubalika yamewasilishwa kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria; Kikosi Kazi kati ya MKURABITA na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi Zanzibar kwa ajili ya maboresho yanayohusu ardhi kimewasilisha ripoti yake kwenye Menejimenti ya Wizara kwa maoni zaidi kabla ya kujadiliwa na Wadau wa Sekta ya Ardhi Zanzibar;

- Kikosi Kazi kati ya MKURABITA na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar kimekabidhi ripoti yake kwa Menejimenti ya Wizara kwa majadiliano ya awali;

- Kikosi Kazi kati ya MKURABITA na TAMISEMI kiliundwa kwa ajili ya kutekeleza maboresho ya ardhi na biashara yaliyoigusa TAMISEMI. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na kujifunza Mfumo wa Taarifa za Kijiografie (*Geographical Information System – GIS*) na jinsi mashamba yanavyopimwa kwa kutumia Chombo cha Upimaji (*Global Positioning System – GPS*) na kuingizwa kwenye Kompyuta na hatimaye utoaji wa hati;

(ii) MKURABITA iliendelea na kazi ya kujenga uwezo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, ambapo jumla ya mashamba 2,054 yalipimwa na kati ya hayo, 2,040 yaliingizwa kwenye mfumo wa *GIS*. Taratibu za kuandaa na kutoa hati miliki za kimila zinaendelea. Aidha, MKURABITA iliendelea kuratibu shughuli za urasimishaji zilizoendelea katika Wilaya 24 ambazo kazi zake zilikuwa ni mwendelezo wa kazi zilizofanyika mwaka 2009/2010, ambapo mashamba 44,763 yalipimwa na mashamba 31,573 yaliingizwa kwenye kompyuta kwa ajili ya kutayarisha Hati Miliki za Kimila. Jumla ya Hati Miliki za Kimila 13,443 ziliandaliwa;

(iii) Ujenzi na ukarabati wa masjala za ardhi vijijini uliendelea katika vijiji vya Wilaya mbalimbali nchini na uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vijiji

vinavyohusika na ujenzi huu vimo katika Wilaya za Manyoni, Nachingwea, Serengeti, Musoma Vijijini, Mpwapwa, Makete, Mvomero, Rufiji, Masasi, Sumbawanga, Mbarali, Mwanga, Mbanga, Sikonge, Muleba, Kahama, Kasulu, Geita, Meru, Moshi Vijijini na Shehia ya Kiungoni kwa upande wa Zanzibar;

(iv) Urasimishaji wa ardhi mijini uliendelea katika Halmashauri za Manispaa ya Morogoro na Arusha, katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro viwanja 878 vimepimwa na katika Halmashauri ya Manispaa ya Arusha viwanja 852 vimepimwa. Ukaguzi wa maeneo ya urasimishaji unafanyika katika maeneo ya Maporomoko Tunduma (Mbeya) na Kimara Baruti (Dar es Salaam);

(v) Urasimishaji wa biashara ulifanyika eneo la Gerezani Jijini Dar es Salaam ambapo wafanyabiashara 1,200 walipatiwa mafunzo ya namna ya kutunza kumbukumbu za biashara, kutumia huduma za kibenki, mbinu za masoko na usajili wa majina ya biashara. Kwa upande wa Zanzibar, mafunzo juu ya urasimishaji wa biashara yalitolewa kwa wafanyabiashara 500 wa eneo la Darajani Unguja na Chake-Chake Pemba; na

(vi) MKURABITA imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano ili kutoa elimu ya urasimishaji na fursa zinazopatikana katika kushiriki shughuli za uchumi rasmi. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Mawasiliano umeanza kwa ajili ya Kanda ya Kati katika eneo la Nzuguni Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ilianza kutekelezwa mwaka 2005 na inatarajjiwa kukamilika Juni, 2013. Kuanza kutekelezwa kwa Awamu hii, kulifuatia mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Awamu ya Kwanza iliyanza kutekelezwa mwaka 2000. Jukumu kubwa la TASAF ni kushirikisha Vikundi vya Jamii, kuainisha, kuchambua mahitaji na kukusanya rasilimali kwa ajili ya maendeleo endelevu katika ngazi ya Vijiji, Shehia na Wilaya. Baadhi ya kazi zilizofanyika katika mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

(i) Maandalizi ya Mpango wa Awamu ya Tatu ya *TASAF (TASAF III)* yameanza kwa Serikali kuteua Timu ya Wataalam ambayo inashirikisha sekta mbalimbali. Timu hii imeshaandaa Andiko la Mradi (*Program Design Document*), ambalo limejadiliwa na Wadau mbalimbali Serikalini na Sekta Binafsi. Awamu ya Tatu ya *TASAF* inatarajja kugharimia Miradi itakayonufaisha Kaya maskini na zilizo katika mazingira hatarishi (asilimia 33.6 ya Watanzania walio maskini zaidi). Aidha, Wadau mbalimbali wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, *DFID*, *WFP* na *UNICEF* ni mionganoni mwa walioonesha nia ya kuchangia. Awamu hii imepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi chenye awamu mbili kuanzia mwaka 2012;

(ii) Miradi 198 yenye thamani ya Shilingi 2,993,196,106 iliibuliwa na Wananchi na kupatiwa fedha kwa utekelezaji wa Miradi hiyo. Aidha, jumla ya Shilingi 36,942,105,529 zilitolewa kusaidia kukamilisha Miradi nchi nzima ambayo ilikuwa haijakamilika, ili miradi hiyo iweze kutoa huduma zilizokusudiwa.

(iii) Mafunzo ya namna ya kuimarisha utekelezaji wa Miradi yalitolewa kwa wataalam kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa wapatao 5,804, Wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa Miradi 104,689 na Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Kamati za Mitaa na Shehia 62,745;

(iv) Mpango wa Majaribio wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini uliendelea kutekelezwa kwenye Halmashauri za Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Chamwino. Kaya zilizonufaika na Mpango huu zimeongezeka kutoka 2,500 mwaka 2009 hadi kaya 4,864 mwaka 2011. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011, kiasi cha Shilingi milioni 549 zimelipwa kwa walengwa tangu mpango huu uanze Desemba, 2009;

(v) Shilingi 209,982,782 zilitolewa ili kuendeleza vikundi 30 vinavyotekeleza Mpango wa Kuweka Akiba na Kuwekeza (*Community Savings and Investment Program – COMSIP*) katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Aidha, wanachama wa vikundi 35 kutoka Halmashauri ya Wilaya za Korogwe na Unguja vyenye idadi ya wanachama 825, walipewa mafunzo katika maeneo ya Usimamizi wa Miradi, Uwekaji Kumbukumbu za fedha na mali wanazomiliki;

(vi) Mifumo ya utoaji wa taarifa imeendelea kuimarishwa ngazi zote za utekelezaji wa Miradi ikiwa ni pamoja na kuingiza taarifa zote za Miradi kwenye mfumo wa kompyuta uliopo *TASAF* Makao Makuu;

(vii) Miradi 376 yenye thamani ya Shilingi 8,683,502,908 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 63 za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba ilitekelezwa kwa utaratibu wa kazi kwa malipo ili kukabiliana na upungufu wa chakula katika Halmashauri hizo; na

(viii) Mafunzo kwa Wananchi na Viongozi kuhusu utekelezaji wa Miradi yalitolewa kwa kutumia vyombo vya habari, ikiwemo Radio, Televisheni, Magazeti, Mabango, Vipeperushi na Machapisho mbalimbali. Aidha, *TASAF* ilishiriki katika maonesho mbalimbali na kutumia fursa hiyo katika kutoa elimu na ufanuzi kuhusu shughuli zinazoteklezwa na *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibashara ili kuongeza ufanisi katika biashara. Baadhi ya kazi zilizoteklezwa katika mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 343,000,000 kwenye vikundi mbalimbali katika Matawi 19 ambayo ni Kinondoni, Ilala, Kibamba, Mbagala, Mkuranga, Kibaha, Chalinze, Morogoro, Turiani, Iringa, Mafinga, Makambako, Mbarali, Uyole, Kilosa, Kongwa, Kilombero, Songea na Kilwa Road (Tawi linalohudumia Polisi);

(ii) Mfuko umetoa mikopo ya Uwezeshaji SACCOs (Mabilioni ya JK) yenye thamani ya Shilingi 38,140,000 kwenye SACCOs 22 katika Wilaya za Mkuranga, Rufiji na Morogoro;

(iii) Mfuko umetoa mikopo yenyе thamani ya Shilingi 26,047,500; kati ya hizo Shilingi 9,447,500 zilitumika kwa ajili ya Ada za Shule kwa wanafunzi 15 katika matawi matano; Kinondoni, Kibamba, Kibaha, Mkuranga na Kilwa Road (Polisi); Shilingi 9,000,000 zilitumika katika ununuvi wa viwanja kwa wateja kumi na nane katika Tawi la Chalinze; na Shilingi 7,600,000 kwa Jeshi la Polisi kwa wanachama 12.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa, Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na kwamba, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Serikali iliajiri watumishi wapya 32,757 katika Sekta za Afya, Elimu na Usalama wa Raia. Watumishi wa Umma 57,387 walipandishwa vyeo na waajiri mbalimbali. Aidha, madai ya malimbikizo ya mishahara ya Watumishi wa Umma 31,428 yenyе thamani ya Shilingi 36,380,789,228 yалиhakikiwa na kuidhinishwa kwa malipo. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2011, watumishi 23,220 wamelipwa malimbikizo ya mishahara yenyе thamani ya Shilingi 25,072,199,535.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010 imeandalifiwa. Aidha, Bodi ya Mishahara na Tija katika Utumishi wa Umma imeanzishwa na inatarajiwa kuanza kazi rasmi katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi, kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105, Serikali ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma lilifanya mikutano mitano, pamoja na mambo mengine liliishauri Serikali kuhusu maslahi ya Watumishi wa Umma;

(ii) Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya Kisekta yalikutana kwa mujibu wa sheria kujadili pamoja na mambo mengine ustawi wa wafanyakazi na maslahi yao;

(iii) Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma lilikutana, pamoja na mambo mengine lilipitisha Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya kada zilizo chini ya Wizara nne: Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Wizara ya Kazi na Ajira na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na

(iv) Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa kazi yalikutana kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Umma, Sura ya 105 kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali kuhusu ufanisi wa kazi, haki na wajibu wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelawa katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 ni pamoja na kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa 12 kwa mujibu wa Sheria, Sura ya 225 ya Mwaka 1999 na Marekebisho yake ya Mwaka 2005, kukamilisha taratibu za upatikanaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu na kufanya ukarabati wa majengo ya zamani yakiwemo maktaba, vyumba vya ofisi, jengo la Kumbukumbu za Nyaraka na vibanda viwili vya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma kwa maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundo na mifumo ya utoaji huduma katika Utumishi wa Umma, yafuatayo yalitekelezwa:-

(i) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara na Idara Zinazojitegemea 29 ilihuishwa na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miundo hiyo imepelekwa kwa taasisi husika kwa utekelezaji;

(ii) Taasisi mbili ambazo ni Ofisi ya Makamu wa Rais na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ziliwezeshwa kuandaa orodha ya kazi zao;

(iii) Wakala wa Serikali Mtando (eGovernment) na Wakala wa Huduma za Misitu (*Tanzania Forest Services – TFS*) zilianzishwa;

(iv) Mafunzo ya usimamizi wa mabadiliko ya kimenejimenti, usimamizi wa Miradi, uandaaji wa Mpango Mkakati na Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Wakala tarajiwa tatu yalikamilika. Wakala tarajiwa hizo ni pamoja na Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtando - *Tanzania Global Learning Agency (TaGLA)*, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi – *Fisheries Education and Training Agency (FETA)*; Wakala wa Vyuo vya Mifugo – *Livestock Training Agency (LITA)*; na Wakala wa Maabara ya Vetenari – *Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA)*;

(v) Taasisi za Umma kumi, Wizara tisa na Idara Inayojitegemea moja zilipatiwa mafunzo ya Ufutiliaji na Tathmini pamoja na uandaaji wa Taarifa za Utendaji Kazi Serikalini;

(vi) Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Serikali ilianzisha Tovuti Kuu ya Taifa ambayo inajulikana kama (www.eGov.go.tz), itakayotumika kutoa huduma kwa njia ya mtando, ilianzishwa na taratibu za kuwaelimisha Wadau kuhusu matumizi ya tovuti hiyo yameanza; (*Makofi*)

(vii) Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 ziliwezeshwa kutumia mfumo wa kompyuta kuwasilisha taarifa za watumishi wapya kwa lengo la kuwaingiza kwenye orodha ya malipo ya mishahara kwa wakati. Aidha, mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi na mishahara uliboreshw na mafunzo ya matumizi

yalitolewa kwa Watumishi wa Wizara 26, Sekretarieti za Mikoa 21, Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 na Taasisi za Elimu ya Juu 12;

(viii) Rasimu ya mwongozo wa matumizi bora na salama ya vifaa na mifumo ya TEHAMA Serikalini iliandaliwa na kusambazwa kwa wadau kupata maoni;

(ix) Taratibu za kuunganisha Wizara zote katika mtandao wa mawasiliano Serikalini zilianza kwa kuainisha mahitaji ya Wizara kuijiunga katika mtandao huo;

(x) Utafiti wa athari za kimazingira (*Environmental Impact Assessment*) zitakazosababishwa na ujenzi wa kituo cha kumbukumbu Dodoma ulikamilika na ujenzi wa kituo hiki unaendelea;

(xi) Utunzaji wa kumbukumbu za Watumishi wa Umma uliboreshwu katika Wizara 14 kwa kuwekewa mfumo wa kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watumishi;

(xii) Mfumo wa masjala uliwekwa katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya 15. Aidha, Ofisi hizi zilipatiwa vifaa vipyta vya masjala; na

(xiii) Mfumo wa kompyuta utakaotumiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuwasiliana ndani ya Ofisi ulikamilika na taratibu za mafunzo zilianza kwa ajili ya watumishi wote watakaoutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uendelezaji Sera katika Utumishi wa Umma, yafuatayo yametekelozwa:-

(i) Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010 imetungwa na kuidhinishwa; na

(ii) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayotumika katika kusimamia utendaji katika Utumishi wa Umma umefanyika kwenye Ofisi za Makatibu Tawala na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Matokeo ya tathmini hizi yatatumika kuhuisha Sera na Miongozo mbalimbali ya Utumishi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uwajibikaji na usikivu kwa Umma, yafuatayo yametekelozwa:-

(i) Kampeni za kukuza uelewa wa maadili ya Utumishi wa Umma na uwezeshaji wa matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko ya Wananchi kwa ufanisi zilifanyika katika Wilaya na Halmashauri zote za Mikoa ya Pwani na Lindi. Pia utaratibu wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa namna ya kushughulikia malalamiko ya Wananchi katika Taasisi za Umma iliandaliwa.

(ii) Elimu kwa umma kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika Utumishi wa Umma ilitolewa katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa - Sabasaba, Siku ya Wakulima – Nane Nane, pamoja na mikutano

mbalimbali iliyofanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 14 za Mikoa ya Kagera na Mara na jumla ya washiriki 2,037 walinufaika na elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa Watumishi wa Umma, yafuatayo yalitekelezwa:-

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa 37 za Mikoa ya Kigoma, Singida, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Arusha na Dodoma ziliwezeshwa namna ya kutekeleza Mwongozo wa Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma;

(ii) Watumishi 82 kutoka katika Wizara moja, Sekretarieti ya Mkoa mmoja, Wakala za Serikali nne na Mamlaka za Serikali za Mitaa 76, walipatiwa mafunzo kuhusu taratibu bora za utendaji katika Utumishi wa Umma zinazohusu masuala ya ajira, nidhamu, usuluhishi na upatanishi;

(iii) Taratibu za kusimamia masuala ya kiutumishi zilihuishwa ili kuhakikisha kuwa teknolojia ya Kompyuta inawafikia waajiri wote katika kuwawezesha kuwa na taarifa sahihi kuhusu watumishi wanaowasimamia ili kuondoa tatizo la watumishi hewa;

(iv) Taarifa za kiutumishi na mishahara kwa Watumishi wa Umma katika Taasisi za Serikali 88 zikiwemo Wizara na Idara zinazojitegemea 27, Sekretarieti za Mikoa 16, Mamlaka za Serikali za Mitaa 29 pamoja na Wakala wa Serikali 13 zilirekebishwa; na

(v) Malalamiko 383 ya Watumishi wa Umma yanayotokana na ukiukaji wa kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma yalipokelewa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uendelezaji rasilimaliwatu na mpango wa kurithishana madaraka, yafuatayo yalitekelezwa:-

(i) Taasisi 17 za Serikali ziliwezeshwa kufanya tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo ili ziweze kuandaa mipango ya mafunzo;

(ii) Ushirikiano na Taasisi za Jumuiya za Kimataifa na Kikanda zinazojihusisha na masuala ya utawala na menejimenti uliendelezwa. Taasisi na Jumuiya hizo ni *African Association of Public Administration and Management (AAPAM)*; *Commonwealth Association of Public Administration and Management (CAPAM)* na *ESAMI*;

(iii) Mafunzo ya Huduma kwa Mteja yalitolewa kwa Viongozi 80 wa Jeshi la Polisi na hivyo kufanya idadi ya Viongozi wa Jeshi hilo waliopata mafunzo hayo kufikia 200 kwa muda wa miaka miwili;

(iv) Viongozi wa Serikali tisa walishiriki Kongamano la 32 la AAPAM. Aidha, Viongozi saba wa Serikali walihudhuria mkutano wa tatu wa Mtando wa Mameneja Rasilimaliwatu katika Bara la Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia;

(v) Watumishi wa Umma 1.057 walipata ufadhili wa mafunzo kutoka mashirika na taasisi mbalimbali za ndani na kimataifa. Kati yao watumishi 767 walihuduria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 290 walihuduria mafunzo ya muda mrefu;

(vi) Semina Elekezi kwa Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali ya Awamu ya Nne ilifanyika, ikijumuisha Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Vyombo vya Dola na baadhi ya Wakuu wa Taasisi za Serikali;

(vii) Maelekezo na mafunzo yalitolewa kwa Taasisi za Umma kuhusu usimamizi bora wa jukumu la urithishanaji madaraka; na

(viii) Sekretarieti za Mikoa 12 ziliwezeshwa kuandaa mipango ya rasilimaliwatu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uratibu wa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma, utaratibu mpya wa utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma uliandaliwa; tathmini ya utekelezaji wa Programu za Mabadiliko katika Utumishi wa Umma ilifanyika; Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliwezeshwa kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma. Aidha, uchambuzi wa utendaji kazi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ulifanyika; Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ulifanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za mafunzo zilizo chini yake ambazo ni Chuo cha Utumishi wa Umma, Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao na Taasisi ya Uongozi. Kazi nyingine zilizotekelizwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake ni kama ilivyooneshwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ukurasa wa 36 hadi 48. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Chuo cha Utumishi wa Umma kilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kozi 18 za muda mfupi kwa Watumishi wa Umma 3,009 katika maeneo ya Utunzaji Kumbukumbu, Utunzaji Ofisi na utoaji huduma bora kwa wateja, *OPRAS*, Mafunzo Elekezi, maandalizi ya kufanya mitihani ya Serikali (*PSE*), teknolojia ya Kompyuta na Uongozi kwa Maafisa wa ngazi ya kati na chini zilitolewa;

(ii) Kozi 43 za muda mrefu kwa Watumishi wa Umma zilitolewa;

(iii) Mpango Mkakati wa Tatu (2011/2012 – 2015/2016) uliandaliwa;

(iv) Watumishi 125 kutoka Matawi ya Dar es Salaam, Mtwara na Tabora walipata mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Tathmini na Kupima Utendaji kazi (*OPRAS*); na

(v) Watumishi wa Chuo 101 walipata mafunzo ya kuwajengea uwezo, kati yao, watumishi 53 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 48 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao kiliendelea kushirikiana na vituo vya maendeleo duniani kwa kutumia teknolojia kama nyenzo ya kuwawezesha Watanzania kujenga uwezo kitaaluma wakiwa hapa nchini kwa njia ya mafunzo, midahalo na shauri za kitaalamu. Kazi zilizoteklezwa ni pamoja na:-

(i) Kukamilisha ukarabati wa awali wa Kituo cha Habari za Maendeleo Tanzania na Maabara ya Mtandao wa Kompyuta;

(ii) Kuongeza chumba cha mawasiliano kwa teknolojia ya *video-conference* na hivyo kupanua uwezo wa Kituo kutoa huduma hii;

(iii) Kutoa mafunzo ya Mifumo ya Mishahara na Utumishi kwa Wafanyakazi wa Serikali 212;

(iv) Kutoa mafunzo ya kuongeza uwezo wa kuendesha mafunzo kwa kutumia teknolojia, yakiwemo mafunzo ya kusimamia Mikataba ya Kimataifa ya Mawasiliano chini ya Ushirika wa Vituo vya Maendeleo Barani Afrika;

(v) Kukamilisha utafiti wa awali wa uanzishaji wa vituo mikoani na majadiliano ya kuanzisha vituo vishiriki vya awali kwa kutumia Mkongo wa Taifa;

(vi) Kupanua ushirikiano na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika kutoa mafunzo. Taasisi hizi ni pamoja na *Ethiopia Civil Service College, Kenya Institute of Administration, African Capacity Building Foundation (ACBF), Association of African Distance Learning Centres (AADLC)*, Jumuia ya Afrika Mashariki, na Chuo cha Benki ya Dunia; na

(vii) Kutoa mafunzo kwa washiriki 952, kati ya hao washiriki 211 ni washiriki binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na 741 ni kutoka Wizara, Idara na Wakala za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 274 la Mwaka 2010, kwa lengo la kuwa Kituo cha Utaalamu wa Hali ya Juu (*centre of excellency*) cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika ya Mashariki na hatimaye Afrika nzima.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Bodi ya Uongozi ya Taasisi hii ilizinduliwa rasmi na Mpango Mkakati wa utekelezaji wa majukumu yake uliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Chombo chenye jukumu la kujenga imani ya Wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma. Katika mwaka 2010/2011, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, iliendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398. Kazi nyingine zilizotekelawa ni kama zilivyooneshwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa 49 kama ifuatavyo:-

(i) Viongozi wa Umma 9,015 wa Kada mbalimbali walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia 31 Desemba, 2010. Hadi kufikia Juni, 2011, jumla ya Viongozi wa Umma 7,904 sawa na asilimia 88 walirejesha Fomu za Tamko;

(ii) Viongozi 23 waliitwa mbele ya Baraza la Maadili kujibu tuhuma za kushindwa kutoa Tamko la Rasilimali na Madeni. Kati ya hao, 21 walifikishwa mbele ya Baraza ambapo watatu walipewa onyo kali, kumi walipewa onyo, wanane walifutiwa tuhuma kwa kutokuwa na hatia. Aidha, viongozi wawili hawakufikishwa mbele ya Baraza la Maadili kutokana na kuumwa;

(iii) Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma 214 wa kada mbalimbali zilihakikiwa ili kujiridhisha kuhusu ukweli na uwazi katika ujazaji wa Fomu za Rasilimali na Madeni;

(iv) Malalamiko 132 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa, kuchambuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa awali ili kubaini ukweli kuhusu malalamiko hayo. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 51 yalihusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili na malalamiko 81 hayahusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa sheria. Malalamiko yasiyohusu ukiukwaji wa maadili yaliwasilishwa kwenye vyombo vingine kwa hatua;

(v) Elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitolewa kwa njia mbalimbali zikiwemo semina 22, vipindi vya redio, mikutano ya hadhara, matamasha, machapisho mbalimbali na kushiriki katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Nanenane;

(vi) Wadau 28 kutoka Taasisi za Umma, Vyama vya Kitaaluma na Asasi za Kiraia zilipewa ruzuku ili kutekeleza Miradi inayolenga kukuza uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Kiasi cha Shilingi 1,575,396,200 zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza Miradi hiyo katika mikoa 16;

(vii) Miradi 37 iliyotekelawa kupitia Mfuko wa Uadilifu, Uwazi na Uwajibikaji ilifanyiwa ufuatiliaji ili kuhakikisha inatekeleza kama ilivyopangwa; na

(viii) Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya, ilifanyiwa ukarabati na ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Kusini Mtwara ulianza. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepata Kiwanja katika Mji wa Chalinze kwa ajili ya kujenga Ofisi ya Kanda ya Mashariki na Pwani inayojumuisha Mikoa ya Pwani, Morogoro na Tanga na mchakato wa kupata hati ya kumiliki Kiwanja hicho unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni chombo kipywa kilichoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 29 kifungu kidogo cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 kazi zifuatazo zilitkelezwa:-

(i) Sekretarieti ya Ajira ilisaili na kupata waajiriwa wapya 1,608 walioajiriwa na waajiri 138;

(ii) Sekretarieti ya Ajira ilitengeneza Mfumo wa Awali wa Usaili;

(iii) Sekretarieti ya Ajira iliwaterembelea waajiri zikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Kagera, Tanga, Arusha, Mwanza, Mara na Pwani pamoja na Halmashauri zake kwa lengo la kujitambulisha na kutoa maelezo kuhusu kazi na majukumu ya Sekretarieti ya Ajira;

(iv) Hadi kufikia Mei, 2011, Sekretarieti ya Ajira ilifanikiwa kuandaa orodha ya wahitimu pamoja na Wataalam Weledi (*Professionals*) kutoka katika Vyuo Vikuu saba;

(v) Mpango Mkakati wa Mwaka 2011 – 2014 uliandaliwa;

(vi) Taratibu za Utendaji zilitengenezwa;

(vii) Mchakato wa kudhibiti tabia iliyokuwa imeanza kujitokeza ya baadhi ya Waajiriwa wapya kwenda kwenye kituo cha kazi na baadaye kutoroka, sambamba na kutokuripoti kabisa baada ya kupangiwa kwa mwajiri husika ulianzishwa. Tabia hii imekuwa ikisababisha kutangazwa tena kwa nafasi husika. Kudhibiti tabia hii kutapunguza gharama za usaili;

(viii) Kanzi Data (*Database*) ya waombaji kazi wenye ujuzi unaotakiwa na waajiri mbalimbali ilianzishwa; na

(ix) Mchakato wa kuwa na Ofisi za Mikoa, kwa kuanzia na Kanda kwenye Mikoa ya Mtwara, Mbeya, Tabora, Mwanza, Manyara na Morogoro pamoja na Zanzibar ulianza.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma: Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Vikao vya kisheria vitatu na kikao kimoja cha dharura vilivyotolea uamuzi wa Rufaa 62 na malalamiko saba vilifanyika;
- (ii) Ukaguzi wa kawaida wa ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika usimamizi wa Rasilimaliwatu kwa Taasisi 24 ulifanyika;
- (iii) Ukaguzi maalumu kwa Taasisi 15 ulifanywa kufuatia malalamiko ya Watumishi wa Umma;
- (iv) Mafunzo ya ukaguzi wa utendaji kazi binafsi kwa watumishi 23 yalifanyika;
- (v) Makala 11 kwenye magazeti na vipindi 32 vya redio vilirushwa kwa lengo la kuwawezesha Wadau;
- (vi) Miongozo mitatu; Ajira, Nidhamu na Rufaa na Ukaguzi wa Rasilimaliwatu ilihuishwa;
- (vii) Mafunzo kwa watumishi 80 kuhusu maadili na jinsi ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI yaliendeshwa;
- (viii) Tafiti mbili kuhusu chanzo na sababu ya kuongezeka kwa malalamiko dhidi ya huduma zitolewazo na Utumishi wa Umma na uwasilishaji wa taarifa za masuala ya ajira na nidhamu katika Tume zilifanyika;
- (ix) Watumishi 104 walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kati ya hao 22 wamehitimu;
- (x) Mpango Mkakati uliokwisha wa Mwaka 2008/09-2010/2011 ulipitiwa na Mpango Mkakati Mpya wa Mwaka 2011/2012 -2013/2014 uliandaliwa;
- (xi) Ofisi nane za Wilaya katika Mikoa minne; ambayo ni Singida (Iramba na Singida Vijijini), Iringa (Iringa Vijijini, Ludewa na Njombe), Morogoro (Kilombero na Morogoro Vijijini) na Mbeya (Mbarali) zilikarabatiwa; na
- (xii) Idara ya Utumishi wa Walimu ngazi za Makao Makuu, Mikoa na Wilaya zisajili walimu 2,361, kuthibitisha kazini walimu 4,581, kupandisha vyeo walimu 5,769, kubadilisha kazi/cheo walimu 1,220, kushughulikia masuala ya nidhamu 253, kushughulikia vibali vya maombi ya kustaa fu kazi kwa walimu 2,821 na kushughulikia mafao 747 ya walimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji kwa Mwaka 2010/2011, sasa ninaomba kutoa Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Shughuli kwa Mwaka wa 2011/2012 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 67 na 94 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais (Ikulu), itaendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na:-

- (i) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo mbalimbali kama vile uchumi, siasa, jamii, sheria na uhusiano wa kimataifa;
- (iii) Kuratibu uhuishwaji wa Mkakati wa Taifa Awamu ya Pili wa Kudhibiti na Kupambana na Rushwa na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na Utawala Bora. Aidha, machapisho yanayohusu taarifa za utekelezaji wa Mipango ya Utawala Bora na hatua zinazochukuliwa katika kupambana na rushwa yataendelea kutolewa. Machapisho haya hutolewa kila robo mwaka;
- (iv) Kuandaa na Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na UKIMWI mahali pa kazi;
- (v) Kutoa mafunzo kwa watumishi kulingana na Mpango wa Mafunzo ili kuwaongezea ujuzi na ubora wa kiutendaji na kusimamia shughuli za uendeshaji wa Ofisi;
- (vi) Kufanya uchambuzi wa Nyaraka na kutoa ushauri kwa Wizara juu ya uandishi wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na kuendelea kuhudumia Baraza la Mawaziri na Kamati zake, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*Inter Ministerial Technical Committee - IMTC*) na Kamati zake;
- (vii) Kushughulikia rufaa za Watumishi wa Umma zinazoletwa kwa Rais na Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, malalamiko ya watumishi wa umma na Wananchi kwa ujumla yataendelea kushughulikiwa;
- (viii) Kuratibu Utekelezaji wa Programu za Mabadiliko katika Sekta ya Umma yanayojumuisha Utumishi wa Umma, Serikali za Mitaa, Usimamizi wa fedha za Umma, Sheria, Kilimo na Mazingira ya Biashara. Maeneo mengine ambayo uratibu utafanywa ni katika mapambano dhidi ya rushwa na mabadiliko yanayoendelea chini ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na maendeleo ya sekta ya fedha na huduma za kibenki; na
- (ix) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuchunguza tuhuma 2,456 zilizopo na tuhuma mpya zitakazopokelewa;

(ii) Kufanya uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo kufuatia kupokelewa kwa malalamiko mengi kutoka kwa Wananchi;

(iii) Kuendesha kesi 466 zilizopo Mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa chunguzi mbalimbali zinazoendelea;

(iv) Kuendelea kufanya utafiti na udhibiti katika maeneo ya ununuzi, elimu, ubora wa bidhaa zinazotengenezwa nchini na zinazotoka nje ya nchi;

(v) Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu rushwa na miundombinu ya maadili kwa Watumishi wa Serikali na Makampuni binafsi na kuendeleza ushirikiano na asasi za kiraia katika mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, TAKUKURU itaendelea kufanya ufuatiliaji wa majukumu ya Kamati za Maadili;

(vi) Kuanza mchakato wa kuingiza somo la maadili, mapambano dhidi ya rushwa na Utawala Bora katika mitaala ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu; na

(vii) Kuanza ujenzi wa ofisi tatu katika Mikoa ya Ruvuma, Tabora na Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha marekebisho ya sheria na mifumo ya kitaasisi Tanzania Bara na Zanzibar kama zilivyofanyiwa kazi na vikosi kazi na kuidhinishwa na Wizara za Kisekta;

(ii) Kuendelea na shughuli za kujenga uwezo katika Wilaya mbili za Zanzibar ambazo ni Wilaya ya Kati Unguja na Mkoani Pemba kwa lengo la kuwaunganisha waliorasimisha rasilimali zao na fursa za kiuchumi;

(iii) Kuendelea na shughuli za urasimishaji wa rasilimali ardhi mjini katika Mamlaka za Mji wa Arusha, Morogoro na Njombe na kuanza urasimishaji wa ardhi mjini katika Wilaya ya Mjini Magharibi – Unguja.

(iv) Kuanza utekelezaji wa Mpango Kazi ulioandaliwa kwa ajili ya urasimishaji katika Miji ya Tunduma – Mbeya, Kimara Baruti – Dar es Salaam, Moshi na Iringa;

(v) Kuanza ujenzi wa masjala ya ardhi vijijini katika Wilaya za Manyoni, Mpwapwa, Pemba, Nachingwea na Serengeti utakamilishwa;

(vi) Kuwaunganisha wafanyabiashara waliorasimisha biashara zao na vyombo vya fedha ili waweze kupata na kukuza mitaji kwa ajili ya biashara zao;

(vii) Kumalizia urasimishaji wa biashara katika maeneo ya Wilaya na Mjini – Unguja na Wete Pemba na kuanza urasimishaji wa biashara katika maeneo ya Wilaya ya Mjini Magharibi – Unguja na Wete Pemba;

(viii) Kuendelea na uratibu wa mchakato wa kuanzishwa kwa Mfuko wa Urasimishaji Ardhi ya Wilaya (*District Land Formalization Revolving Fund*); na

(ix) Kukamilisha taratibu za kurahisisha mifumo ya kodi na uandikaji wa vitabu vya mahesabu kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (*SMEs*).

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), katika mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa zote za Tanzania Bara na Zanzibar kubuni Miradi itakayoboresha huduma za jamii na kuongeza kipato katika Miradi 1,200 itakayobuniwa na Wananchi;

(ii) Kuwezesha uundwaji wa vikundi 500 vya kuweka akiba na kuwekeza na kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuvipatia vikundi hivyo vifaa. Aidha, vikundi vitakavyoundwa na vile vilivyopo vitatambulishwa katika Taasisi za Fedha ili viweze kukopa kutoka Taasisi hizo;

(iii) Kuendesha mafunzo katika ngazi za utekelezaji wa Miradi kwa Wadau 252,315 wakiwemo: Wajumbe wa Kamati za Miradi, Wajumbe wa Kamati za Serikali za Vijiji/Mitaa na Wataalam wa Sekta zinazohusika;

(iv) Kutekeleza Mpango wa Jamii wa Uhawilishaji fedha kwa kaya maskini sana 11,000 katika Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Chamwino na Kibaha;

(v) Kukuza uelewa wa walengwa kuhusu Kanuni na Taratibu za utekelezaji wa Miradi kwa kutumia vipindi vya Redio, Televisheni na machapisho mbalimbali;

(vi) Kuboresha uendeshaji wa Mifumo ya Taarifa za Fedha na Miradi kwa kutoa mafunzo kwa wataalam mbalimbali katika ngazi zote;

(vii) Kukusanya taarifa za utekelezaji na maendeleo ya Miradi na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miradi inayotekeliza na Wananchi;

(viii) Kuchapisha kwenye magazeti Taarifa za Fedha zinazotolewa na *TASAF* kwenda kwenye Wilaya zinazotekeliza Miradi kwa lengo la kukuza uwazi na uwajibikaji; na

(ix) Kufanya ukaguzi ili kujiridhisha na matumizi ya fedha, ubora wa Miradi inayotekelozwa na iwapo Miradi inatekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya sekta husika. Kazi nyingine zitakazotekelozwa na Ofisi ya Rais Ikulu pamoja na taasisi zake ni kama zilivyooneshwu katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa 56 hadi 65.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea utafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa huduma ya mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali Wadogo na wa Kati Mijini na Vijiji;

(ii) Kuendelea kutoa huduma ya ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa wateja kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali zinazotoa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika biashara zao; na

(iii) Kuendelea kujenga uwezo kwa Wadau/Watendaji na Wafanyakazi ili kuweza kutoa huduma za viwango vya juu na kuongeza tija katika utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu hayo katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais (Ikulu), inaomba kiasi cha Shilingi 8,524,917,000 (Fungu 20) na Shilingi 200,519,723,000 (Fungu 30), kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Shilingi 66,769,353,000 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa, Utumishi wa Umma unaendelezwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na kwamba Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu wanapotoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itarekebisha mishahara ya watumishi wake kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, kasi ya mfumko wa bei, uwezo wa bajeti na makubaliano yaliyofikiwa na Baraza la Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma lililoundwa kwa mujibu wa Sheria ya majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105 ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 3.2 kugharamia malipo ya mishahara, upandishwaji vyeo na kulipia madai ya malimbikizo na mapunjo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi za Serikali. Aidha, kiasi hiki kimeongezeka kwa shilingi bilioni 938 ambayo ni sawa na ongezeko la 40.2% ya fedha zilizotengwa kugharimia malipo hayo katika Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma, Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010. Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo umeandaliwa.

Aidha, Bodi ya maslahi na tija katika Utumishi wa Umma iliyoanzishwa, itaanza rasmi kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 64,024, ambapo kipaumbele kitakuwa katika Sekta za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo. Aidha, Serikali inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 80,050 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itaendelea kusimamia matumizi sahihi ya rasilimaliwatu pamoja na kuratibu ajira katika Utumishi wa Umma kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusambaza na kusimamia utekelezaji wa mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali;

(ii) Kuimarisha Idara za Utawala na usimamizi wa rasilimaliwatu katika ngazi ya waajiri ili waweze kusimamia masuala ya ajira na malipo ya mishahara kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu;

(iii) Kuanzisha Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma itakayofuitalia kwa karibu maamuzi mbalimbali ya kiutumishi yanayotolewa na waajiri kuhusiana na malipo ya mishahara ya watumishi wa umma;

(iv) Kusimamia mfumo wa mishahara Serikalini (*Payroll Management*) ambapo, pamoja na mambo mengine, ukaguzi wa mara kwa mara wa orodha ya malipo ya mishahara na matumizi ya rasilimaliwatu utafanyika ili kuhakikisha watumishi waliopo wanatumika kwa ukamilifu na wanalipwa mishahara kulingana na stahili zao;

(v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Tathmini na Kupima Utendaji Kazi (*OPRAS*) katika Utumishi wa Umma; na

(vi) Kushirikiana na Wizara ya Fedha katika siku maalum ya kulipa mishahara ya watumishi wa umma katika vituo vyao vya malipo badala ya mishahara kupitia benki, kwa lengo la kuondoa tatizo la watumishi hewa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itaendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuhuisha na kuwianisha Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazosimamia utendaji katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa Wakala wa Serikali, kuhuisha miundo, mifumo ya utendaji kazi na viwango vya ki-menejimenti vinavyolenga katika kuboresha utoaji wa huduma katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kukuza na kusimamia uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na usikivu kwa umma ili kupunguza malalamiko na kero mbalimbali za Wananchi zinazotokana na kukiuka maadili ya kazi;

(iv) Kusimamia uendelezaji wa stadi za uongozi na kuwaendeleza Watumishi wa Umma kitaaluma kwa kuzingatia makundi maalum;

(v) Kuimarisha mifumo ya taarifa, mawasiliano ya habari Serikalini, matumizi ya TEHAMA na kuhakikisha kuwa inatoa taarifa zilizo sahihi zitakazosaidia watendaji kufanya maamuzi yaliyo sahihi;

(vi) Kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kufanikisha utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma;

(vii) Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Tuli Dodoma na cha Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza; na

(viii) Kuboresha mifumo ya utunzaji kumbukumbu katika Wizara 13, Mikoa 15 na Ofisi za Balozi zetu nne. Aidha, mfumo mpya wa masjala utawekwa katika Ofisi 14 za Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazotekelawa ni pamoja na kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria ya Kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa, Sura ya 225; kufanya upembuzi yakinifu na kufanya utafiti wa athari za kimazingira zitakazotokana na ujenzi wa Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu; kuandaa na kukamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la pamoja la Ofisi ambalo litatumika kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Tume ya Utumishi wa Umma; Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuondokana na gharama kubwa za pango katika majengo ya Taasisi binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itaendelea kusimamia Taasisi za Mafunzo zilizopo chini yake kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Chuo cha Utumishi wa Umma kimepanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kujenga uwezo wa kitaaluma kwa watumishi wa chuo 79 ili kukidhi mahitaji ya Wadau;

(ii) Kuandaa na kutoa mafunzo kwa washiriki 20,701 wakiwemo Watumishi wa Umma 14,220 na washiriki kutoka Sekta Binafsi 6,481;

(iii) Kukamilisha maandalizi ya mtaala wa kozi ya Cheti cha Utawala katika Serikali za Mitaa (*Certificate in Local Government Administration*) itakayoanza kutolewa Januari, 2012;

(iv) Kukamilisha maandalizi ya mtaala wa stashahada ya usimamizi wa fedha katika Sekta ya Umma (*Public Sector Financial Management*); Utunzaji kumbukumbu; utawala Serikalini na menejimenti ya rasilimaliwartu;

(v) Kukamilisha utaratibu wa upatikanaji wa eneo la ekari 200 huko Ikwiriri Wilayani Rufiji kwa ajili ya ujenzi wa tawi jipya;

(vi) Kufanya tafiti kuhusu utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Upimaji Utendaji Kazi (*OPRAS*); mkataba wa huduma kwa mteja; matumizi ya hatimkato (*Shorthand*). Aidha, kufanya shauri za kitaalamu kuhusu miundo ya utunzaji kumbukumbu katika Utumishi wa Umma; kutambua mahitaji ya mafunzo katika Utumishi wa Umma; kuandaa miundo ya utumishi na orodha ya kazi; kutengeneza mipango mkakati; na

(vii) Kuandika vitabu na kutoa machapisho 14 katika Jarida la Usimamizi wa Utumishi wa Umma (*Public Sector Management Journal*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, kituo cha mafunzo kwa njia ya mtandao kimepanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi wapatao 2,000 katika maeneo ya Utawala Bora, kupunguza umaskini, uongozi, jjinsia, afya, mazingira, kilimo na masoko, matumizi ya teknolojia na kuboresha utendaji kazi Serikalini na katika Sekta Binafsi;

(ii) Kuwawezesha Watanzania kushiriki katika Midahalo ya Kimataifa ya Maendeleo 40 kwa njia ya mtandao;

(iii) Kukuza Mtandao wa Kituo ili kuwafikia Watanzania wengi kwa kutumia teknolojia mpya zinazopatikana nchini; na

(iv) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili kukidhi mahitaji ya umma na matumizi ya teknolojia katika kujenga uwezo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Uongozi imepanga kufanya yafuatayo:-

- (i) Kutoa mafunzo ya kumjenga kiongozi wa umma katika kufanya uchambuzi katika masuala mbalimbali;
- (ii) Kutoa mafunzo ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sera na mikakati mbalimbali;
- (iii) Kutoa mafunzo ya kuwajenga Viongozi wa Umma ili wawe mfano wa kuigwa kimaadili; utendaji kazi, ari ya kuijendeza; na
- (iv) Kutoa mafunzo elekezi kwa viongozi mbalimbali wa umma watakaoteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu hayo katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, inaomba kutumia jumla ya shilingi 33,361,247,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wake wa mwaka. Kati ya fedha hizi Shilingi 16,022,977,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 17,338,270,000 kwa ajili ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2011/2012 na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kupokea na kufanya uchambuzi na uchunguzi wa awali wa malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (iii) Baraza la Maadili kufanya uchunguzi wa kina kuhusu malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (iv) Kuanzisha Mfumo wa kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (v) Kuchapisha na kusambaza kwa Viongozi wa Umma Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni na kufanya uhakiki katika fomu za tamko la rasilimali na madeni;
- (vi) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi (*Facility for Ethics, Accountability and Transparency – FEAT*);
- (vii) Kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa njia mbalimbali zikiwemo semina, vipindi vyta redio, mikutano ya hadhara, matamasha, machapisho mbalimbali na kushiriki katika maonesho; na
- (viii) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Kusini – Mtwarra na kutafuta jengo la kupangisha kwa ajili ya Ofisi ya Makao Makuu katika kipindi ambacho jengo jipya la maadili linajengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo na kutoa huduma mbalimbali, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inaomba jumla ya Shilingi 3,271,222,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,361,222,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 910,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuendesha mchakato wa ajira kwa nafasi wazi za kazi 64,024 katika Utumishi wa Umma kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea pamoja na Wakala za Serikali 9,655; Sekretarieti za Mikoa nafasi 1,514; Mamlaka za Serikali za Mitaa nafasi 48,720; Taasisi za Serikali 3,592 na Wakala wa Serikali nafasi 543;

(ii) Kutembelea Sekretarieti za Mikoa zilizobaki pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zilizopo kwenye Mikoa hiyo kwa lengo la kujitambulisha pamoja na kutoa maelezo kuhusu majukumu ya Sekretarieti ya Ajira;

(iii) Kuendelea na mchakato wa kuanzisha Ofisi za Sekretarieti ya Ajira kwa kila mkoa kwa lengo la kurahisisha usaili katika mikoa; na

(iv) Kuendelea na uanzishaji wa *kanzidata (Data Base)* za kutunza takwimu za waombaji wa fursa za ajira pamoja na wahitimu kutoka kwenye vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa majukumu hayo yanatekelezwa, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, inaomba jumla ya Shilingi 2,939,650,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kuratibu Mikutano ya kila robo mwaka ya Tume na kutolea maamuzi Rufaa na Malalamiko kadiri yatakavyopokelewa;

(ii) Kufanya ukaguzi wa kawaida wa Rasilimaliwatu katika Mamlaka za Ajira na Nidhamu;

(iii) Kufanya Ukaguzi Maalum kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma mara tunapopokea malalamiko ya watumishi;

(iv) Kutoa mafunzo kwa Wadau kuhusu namna ya kutumia mfumo mpya wa ukaguzi na kufanya ukaguzi kwa kutumia Mfumo huu Mpya;

- (v) Kuelimisha Wadau kuhusu shughuli za Tume kupitia vyombo nya habari na ziara;
- (vi) Kutoa elimu kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na mazingira hatarishi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI; mapambano dhidi ya rushwa;
- (vii) Kutekeleza majukumu ya kisheria kama mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu nchini;
- (viii) Kufanya tafiti kulingana na mahitaji ya Tume na Wadau wake;
- (ix) Kuwajengea uwezo kitaaluma Watumishi wa Tume 62; na
- (x) Kuboresha mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Tume katika ngazi zote kwa kuwajengea uwezo kitaaluma na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu hayo, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kutumia kiasi cha Shilingi 8,215,007,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninapenda kuzishukuru nchi na washirika wa maendeleo mbalimbali ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio mbalimbali tuliyoyapata. Hivyo, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuzishukuru Nchi na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yafuatayo: Australia, China, Finland, India, Italia, Japan, Korea Kusini, Malaysia, Misri, Norway, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujeruman, Uswisi, Marekani, Ireland, Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Japan, CIDA – Canada, DANIDA, DFID, JICA, NORAD, OPEC, SIDA – Sweeden, UNDP, UNIDO, UNFPA, USAid, GIZ na KOICA.

Mheshimiwa Spika, ili tuwe na uchumi imara na endelevu, tunahitaji Utawala Bora, ambapo Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu bora zinatumika katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za Serikali. Taasisi zenye jukumu la kuhakikisha mazingira haya yanakuwepo ni Ofisi za Rais (Ikulu), Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma. Hivyo, Mipango ya Utekelezaji ya 2011/2012 ya Taasisi hizi za Serikali inalenga kufanikisha majukumu haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza majukumu na mipango ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, ninaomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 kama ifuatavyo:-

- (a) Fungu 20: Ofisi ya Rais - Ikulu
Matumizi ya Kawaida Sh. 8,524,917,000

Jumla Sh. 8,524,917,000

(b) Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 200,519,723,000

(ii) Miradi ya Maendeleo Sh. 66,769,353,000

Jumla Sh. 267,289,076,000

(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 16,022,977,000

(ii) Miradi ya Maendeleo Sh. 17,338,270,000

Jumla Sh. 33,361,247,000

(d) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 2,361,222,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo
Sh. 910,000,000

Jumla Sh. 3,271,222,000

(e) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida Sh. 2,939,650,000

Jumla Sh. 2,939,650,000

(f) Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida Sh. 8,215,007,000

Jumla Sh. 8,215,007,000

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Hoja hii imeungwa mkono, namwita mtoa hoja wa pili Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hoja hii, ninapenda nitumie dakika mbili kutoa

rambirambi kwa familia ya Marehemu Charles Mangwale, aliyejkuwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Bunda, ambaye amefariki dunia tarehe 29 Juni, 2011 na kuzikwa katika Kijiji cha Iwovo, Wilaya ya Mbeya Vijijini jana. Ninawapa pole sana familia, vilevile Wanachama wa CCM katika Wilaya zote mbili; Wilaya ya Bunda na Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya rambirambi hizo, ninapenda kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2010/11. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, kwa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii, kuishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa ushirikiano na ushauri mzuri iliotupatia wakati wa kujadili makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/12, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Katibu Mtendaji, Dkt. Philip Mpango, Naibu Makatibu Watendaji na Wafanyakazi wote wa Tume ya Mipango, ambao wamefanya kazi kubwa kuwezesha Hotuba hii kukamilika wa wakati.

Mheshimiwa Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne: Sehemu ya kwanza ni Utekelezaji wa Maagizo yaliyotolewa na Kamati zako Tukufu kwa Tume ya Mipango katika hatua mbalimbali za maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12; Pili, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa mwaka 2010/11; Tatu, Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010; na nne Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakati ikijadili Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/11, ilishauri kuwa ni vizuri mawasiliano baina ya Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango yaimarishwe.

Mheshimiwa Spika, ushauri huo umezingatiwa ipasavyo na kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Tume ya Mipango ilishirikiana na Wizara ya Fedha katika maeneo yafutayo:-

- (i) Kazi zilizoratibiwa na Wizara ya Fedha
 - (a) Kutayarisha Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2011/12 na kuainisha Sera za Uchumi Jumla;
 - (b) Kamati ya Taifa ya kusimamia madeni;

- (c) Majadiliano na Wahisani wa Kibajeti na pia Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (*IMF*);
- (ii) Kazi zilizoratibiwa na Tume ya Mipango
- (a) Kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- (b) Kuandaa Mpango Elekezi wa Utekelezaji wa Dira 2025;
- (c) Kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025;
- (d) Kutayarisha mfumo wa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Marekani kuhusu ukuzaji wa uchumi (*Partnership for Growth*); na
- (e) Kuratibu matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA katika klasta ya Ukuaji wa Uchumi.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu umekuwa wa manufaa makubwa. Tunapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa ushirikiano huo utaendelezwa na kudumishwa wakati wote kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mukutano wa kwanza wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Tume ya Mipango, uliofanyika tarehe 23 Machi 2011, kuhusu Muundo na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume, Kamati ya Fedha na Uchumi, iliiagiza Tume ya Mipango kuzingatia masuala mbalimbali. Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu juu ya utekelezaji wa maagizo hayo kama ifuatavyo:-

Kwanza; Tume ya Mipango ijengewe uwezo kwa kuwa na wataalam wa kutosha, wenyе sifa, ili iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu kama Chombo cha Mawazo Rejea (*Think Tank*) katika usimamizi wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wapya 22 wameajiriwa kuanzia mwezi Mei 2011. Hata hivyo, bado kuna upungufu mkubwa. Katika muundo wa sasa wa Tume, wanatakiwa wataalam wachambuzi wa sera 80 wa taaluma mbalimbali. Hadi sasa kuna wataalam wachambuzi wa sera 42 tu. Aidha, bado kuna upungufu mkubwa wa kitaaluma hususan katika maeneo ya uratibu na ufuatiliaji, kufanya maoteo ya uchumi jumla (*macro-economic modeling and forecasting*) na maeneo mahususi kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa siku zijazo (Viwanda mama, miundombinu, mipango miji na kukuza ubunifu). Hivyo, mkazo umewekwa katika kuwaendeleza wataalam waliopo kwa kupatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ndani na nje ya nchi, ili kuwaongeza uwezo kukabiliana na majukumu mapya ya Tume ya Mipango.

Pili, Tume ibainishe na kuishauri Serikali kuhusu vipaumbele vichache vitakavyoweza kuleta matokeo ya haraka katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano vimebainishwa sawia katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/12 - 2015/16. Wakati nikiwasilisha Mpango huo mbele ya Bunge lako Tukufu, mnamo tarehe 13 Juni, 2011, nilianisha vipaumbele vya Taifa kwa miaka mitano ijayo kuwa ni:-

- (i) Miundombinu, hasa upatikanaji wa nishati ya umeme toshelevu kwa mahitaji ya ndani na kuuza katika nchi jirani. Miundombinu ya usafirishaji, hasa bandari, reli, barabara, na usafiri wa anga;
- (ii) Kilimo: Msisitizo ni katika kujitosheleza kwa chakula, kilimo cha biashara na uongezaji wa thamani. Aidha, msisitizo umewekwa katika mazao yenye thamani kubwa (*high value crops*) kama vile maua, mbogamboga, matunda, viungo na zabibu;
- (iii) Viwanda: Mkazo umewekwa katika kuendeleza viwanda vinavyotumia kwa wingi malighafi zinazopatikana hapa nchini ikiwa ni pamoja na pamba, miwa, katani, samaki, mifugo na maliasili;
- (iv) Maji kwa maana ya kuongeza hifadhi na vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa muindombinu ya ugavi wa maji, mijini na vijijini, kwa ajili ya matumizi ya binadamu, viwanda, kilimo na mifugo na vilevile kuboresha upatikanaji wa huduma za maji-taka; na
- (v) Rasilimali watu: Hasa katika kuboresha elimu ya sayansi na ufundi na kuongeza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa vipaumbele hivi ulizingatia dhamira ya Serikali katika miaka mitano ijayo, ambayo ni kutanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi vilivyopo; kujenga uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini kwa haraka; na kujizatiti katika kutumia kwa ufanisi na kimkakati fursa zinazoibuka kutohana na mahusiano mapya ya kiuchumi, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tofauti na upangaji wa vipaumbele katika mipango na programu mbalimbali za awali, ambavyo vilikuwa vya kisekta, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umebainisha shughuli au Miradi Maalum ya Kimkakati. Aidha, Mpango umebainisha malengo mahususi yatakayotumika kupima ufanisi wa utekelezaji wa Miradi hiyo na matokeo tarajiwu kiuchumi na ustawi wa jamii.

Tatu; matokeo ya kazi za Tume ya Mipango yawafikie Waheshimiwa Wabunge, agizo lingine la Kamati ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango imezingatia kikamilifu ushirikishwaji wa Waheshimiwa Wabunge katika kujadili matokeo ya kazi za Tume, hususan, kupitia Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu.

Miongoni mwa kazi zilizofikishwa katika Kamati yako Tukufu ni pamoja na Sera za uchumi jumla kwa mwaka 2011/12; Mapitio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025; Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/12 – 2015/16; na Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, Ushauri wa Kamati ulikuwa msaada mkubwa kwa Tume. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Tume ya Mipango daima itahakikisha ushirikiano huu unadumishwa na kwamba, matokeo ya kazi zake yataendelea kuwasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge kadiri inavyowezekana.

Nne, kuainisha yatakayojitokeza katika kutekeleza Agizo la Mheshimiwa Rais, la kufanya mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba yangu ya kuwasilisha Mpango wa Miaka Mitano Bungeni, nilieleza kwa kirefu matokeo ya mapitio ya Dira 2025. Mapitio ya utekelezaji wa Dira 2025 katika kipindi cha miaka kumi ya utekelezaji wake, yamebaini matokeo mchanganyiko. Kimsingi, ilibainishwa kuwa Dira na malengo yake bado ni maridhawa kwa mustakabali wa Taifa.

Vilevile utekelezaji wa Dira 2025 umekuwa na mafanikio hasa katika malengo ya kuwaletaa Watanzania maisha bora na mazuri na kujenga uchumi imara na shindani. Kwa ufupi ningenda kurejea yafuatayo:-

(a) Mafanikio: Ongezeko la wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 51 mpaka 59;

(b) Udhili wa wanafunzi shule za msingi umeongezeka kutoka 4,400,000 hadi 8,400,000; sekondari kutoka 262,000 hadi 1,500,000; na elimu ya juu kutoka wanafunzi 20,740 hadi 118,000;

(c) Vifo vya wajawazito vimepungua kutoka 578 mpaka 454 kati ya wajawazito 100,000 na vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja kutoka vifo 68 hadi 51 kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa hai, ambapo vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 112 hadi 81 kati ya watoto 1,000; na

(d) Kuimarika kwa huduma ya maji ambapo idadi ya watu wanaopata maji safi na salama vijijini imeongezeka kutoka asilimia 53.1 hadi asilimia 58.7 na kwa mijini kutoka asilimia 74 mpaka asilimia 84.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mapitio ya utekelezaji wa Dira 2025 yilibainisha changamoto zifuatazo:-

(a) Japokuwa wastani wa kipato uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 270 hadi 540 bado ni chini ya maoteo ya kufikia Dola za Kimarekani 995 mwaka 2009. Aidha, Tanzania inabaki kuwa mionganoni mwa nchi maskini sana duniani.

(b) Ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 6.5 kwa mwaka ulikuwa chini ya lengo la wastani wa asilimia 8 au zaidi;

(c) Mfumko wa bei bado ni tatizo, ukiathiriwa na ongezeko la bei ya mafuta na chakula katika soko la dunia au ukame hapa nchini;

(d) Gharama ya kufanya biashara bado ni kubwa hasa kutokana na urasimu, miundombinu hafifu, tija ndogo ya rasilimali watu na upungufu wa kisheria;

(e) Ukuaji wa Sekta ya Kilimo bado ni mdogo (asilimia 4.2 kwa mwaka) na hivyo kushusha mchangano wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa, wakati Sekta ya Kilimo ikibakia ndiyo mwajiri mkuu wa nguvu kazi ya nchi kwa asilimia 75. Hali hii imechangia kuwa na mafanikio hafifu katika kuondoa umaskini; na

(f) Uchanga wa Sekta ya Viwanda na hivyo nchi kuendelea kuuza mazao ghafi badala ya mazao ya viwandani na huduma. Mchangano wa Sekta ya Viwanda nchini katika Pato la Taifa ni asilimia 24 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 31 kwa nchi za kipato cha kati;

Mheshimiwa Spika, faraja ni kuwa, mapitio yilibainisha kuwepo kwa rasilimali na fursa tele kuwezesha malengo ya dira kufikiwa katika kipindi cha miaka 15 iliyobaki. Hata hivyo, ipo haja ya kujipanga vizuri na kutumia rasilimali na fursa za nchi kimkakati zaidi. Hii ikiwa ni pamoja na kuwa na mipango ya maendeleo ya muda mrefu kulingana na malengo ya dira. Aidha, hapana budi kuwa na mkakati thabiti wa kuitangaza Dira na Mpango kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maoni haya, Serikali imeamua kurejea utaratibu wa kuwa na mipango ya maendeleo ya muda mrefu, wa kati na mfupi na kuimarisha mfumo wa kuratibu, kufuatilia na kufanya tathmini utekelezaji wa mipango yake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 iliweka ahadi za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(a) Kupitia malengo na viashiria vya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ili kubaini kama bado vinaendana na matakwa na mustakabali wa maendeleo ya Taifa;

(b) Kuandaa mfumo mpya wa utayarishaji mipango kutoka miaka mitatu kuwa miaka mitano;

- (c) Kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2011 - 2016;
- (d) Kutoa mwongozo wa sera za kitaifa kumwezesha mwananchi kushiriki katika ukuaji na mageuzi ya kiuchumi;
- (e) Kutafiti na kutathmini raslimali zilizopo na kuelekeza matumizi yake kimkakati kwa maendeleo ya Taifa na kupunguza umasikini;
- (f) Kuibua na kufanya tafiti za kina kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii;
- (g) Kujenga uwezo wa Tume kitaaluma ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- (h) Kuratibu na kuchambua mwelekeo wa maendeleo kiuchumi na kijamii katika ngazi za kisekta, kitaifa, kikanda, kimataifa na kubaini changamoto zinazojitokeza; na
- (i) Kutekeleza masuala mtambuka kama vile mazingira, masuala ya UKIMWI, Jinsia na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya utekelezaji wa ahadi hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya mapitio ya dira ya mwaka 2025 imekamilika. Mapitio hayo yamezingatia, pamoja na mambo mengine, hatua za utekelezaji wa malengo ya dira ya mwaka 2025 na mabadiliko ya kiuchumi nchini, kikanda na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mapitio yamebainisha kuwa dira na malengo yake yanakidhi haja kwa mustakabali wa Taifa letu. Aidha, utekelezaji wake umekuwa na mafanikio kiasi cha kuridhisha. Hivi sasa Tanzania ni moja kati ya nchi 17 za kusini mwa jangwa la Sahara zinazoongoza katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini, na kuwa na utawala bora na uwajibikaji. Hata hivyo, juhudhi zaidi bado zinahitajika kufikia malengo ya dira. Hili linawezekana kama tutajipanga vizuri kutumia raslimali na fursa za nchi kimkakati zaidi.

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo umeandaliwa kwa kipindi cha miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016) badala ya mfumo wa miaka mitatu mitatu. Mwongozo wa Mpango na Bajeti nao umeandaliwa kwa kuzingatia kipindi cha miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016). Aidha, mipango ya maendeleo ya kisekta inatakiwa kuzingatia utaratibu huo kuanzia mwaka 2012/2013 ili kwenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuandaa mpango elekezi (2011/2012 - 2025/2026) inaendelea. Mpango elekezi unakamilishwa kwa kuzingatia maoteo ya malengo mahsus yatakayotakiwa kufikiwa katika vipindi vitatu vya miaka mitano mitano ili Taifa liweze kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati mwaka 2025. Malengo hayo yalichambuliwa wakati wa mapitio ya dira 2025. Kilicho dhahiri ni kuwa, kufikiwa malengo haya kunahitaji mabadiliko makubwa katika muundo wa uchumi nchini kuendana na

mabadiliko makubwa ya mfumo wa utashi katika masoko. Utashi wa soko hivi sasa unatawaliwa na biashara ya bidhaa za viwandani na huduma.

Hivyo, ili Tanzania ishiriki katika biashara ya Kimataifa haina budi kujielekeza kukidhi matakwa hayo. Mkazo hauna budi kuwekwa katika kujenga misingi endelevu ya ujenzi wa uchumi wa kisasa unaoongozwa na Sekta ya Viwanda na Kilimo cha Kisasa. Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano umezingatia hitajio hilo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) ni awamu ya kwanza ya mpango elekezi (*roadmap*) wa miaka 15 wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa utaratibu wenyewe viashiria mahsusini vya kupima mafanikio ya utekelezaji. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unajielekeza zaidi kuvunja vikwazo vya kukuza uchumi wa Taifa hususan miundombinu ya nishati na usafirishaji (reli, bandari, barabara na *TEHAMA*). Aidha, unajielekeza katika kuharakisha mapinduzi ya kilimo (kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi), maji na maendeleo ya raslimali watu.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Sera ya Taifa kumwezesha mwananchi kushiriki katika ukuaji na mageuzi ya uchumi, Serikali inatambua kuwa ili kuwe na maendeleo endelevu na yenye manufaa kwa umma wa Watanzania, pana haja ya msingi ya kuwawezesha kushiriki katika ukuaji wa uchumi. Kwa kutambua hili, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umebainisha yafuatayo:-

(a) Kuweka kipaumbele katika shughuli za kiuchumi za msingi kwa wananchi walio wengi. Hii ni pamoja na kilimo cha mazao, ufugaji, uvuvi, uendelezaji misitu na maliasili;

(b) Uendelezaji wa raslimali watu, hususan ujuzi na stadi za kazi kukidhi mahitaji ya maendeleo ya uchumi wa kisasa na ajira; na

(c) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na kuimarisha mitaji ya Benki ya Raslimali (*TIB*), Benki ya Kilimo, Benki ya Wanawake na uhamasishaji wa maendeleo ya Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa (*SACCOS*) na *VICOBA*. Aidha, kuimarisha mitaji ya Mashirika ya Umma ya Uwekezaji ikiwa ni pamoja na Shirika la Taifa la Petroli (*TPDC*), Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*), Shirika la Taifa la Madini (*STAMICO*), na Shirika la Utafiti wa Madini (*GST*).

Mpango vilevile unatoa fursa ya kuwekeza katika viwanda vitakavyosaidia kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na maliasili na vile ambavyo vitawezesha utumiaji wa malighafi zinazopatikana humu nchini na hivyo kumwezesha mwananchi kushiriki ipasavyo katika ukuaji na mageuzi ya kiuchumi nchini. Aidha, mpango unatoa fursa kwa watu wenyewe mahitaji maalum na watu wa jinsia zote waweze kushiriki kikamilifu katika fursa zinazojitokeza ndani ya mpango wenywewe. Fursa hizo ni pamoja na huduma za fedha na kujiendezea kielimu ili kuondokana na umasikini kwa watu wa makundi yote.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, imeelekeza matumizi ya kimkakati ya raslimali za nchi; hususan rasilimali watu, rasilimali fedha na rasilimali asili, kwa maendeleo ya Taifa na kupunguza umasikini.

Katika suala la raslimali watu, Mpango umetilia mkazo katika kuendeleza ujuzi na stadi za kazi kuwawezesha wananchi kuajiriwa na kujajiri katika sekta za kisasa. Pamoja na hili, Mpango pia unasisitiza umuhimu wa kuendeleza utulivu wa uchumi jumla na mazingira wezeshaji kwa biashara na uwekezaji ikiwa ni pamoja na mkazo katika nidhamu ya kibajeti kwa kuelekeza fedha zaidi katika vipaumbele vichache. Mpango pia unasisitiza na kubainisha matumizi bora na endelevu ya raslimali asili (madini, gesi asili, misitu, raslimali bahari, ardhi na kadhalika), hususan, uongezaji thamani na kusaidia wachimbaji wadogo wa madini.

Hata hivyo, ni vizuri tukakumbushana kwamba, ni jukumu la kila mdau wa maendeleo kutumia fursa zilizoainishwa katika mpango huo kujiletea maendeleo yake na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango imeendelea kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali na tafiti hizo ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Moja ya tafiti zilizofanyika ilihusu namna Tanzania itakavyoweza kutumia fursa za kiuchumi katika jumuiya za Kikanda na Kimataifa ili kufikia malengo ya Dira ya mwaka 2025 (*Harnessing Tanzania's Participation in Regional and Global Economies to Achieve Tanzania Development Vision 2025*). Kazi hii imefikia hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine iliyofanyika ilikuwa ni kuratibu ukamilishwaji wa utafiti wa awali kuhusu hali ya ajira hapa Tanzania chini ya “*EAC Manpower Pilot Survey*”, ikiwa ni maandalizi ya “*EAC Manpower Main Survey*”. *Pilot Survey* imekamilika, lakini *Main Survey* inasubiri upatikanaji wa fedha kutoka Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utafiti huu unalenga katika kujiandaa vyema katika ushindani wa soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, tafiti nyingine bado ziko katika hatua ya matayarisho. Tafiti hizi ni pamoja na:-

- (a) Maendeleo ya Miundombinu kwa ajili ya kilimo cha kisasa na masoko (*Infrastructure Development for Modern and Market Oriented Agriculture in Tanzania*);
- (b) Muundo wa kitaasisi kuweshera ukuaji wa kimkakati wa viwanda Tanzania (*Study on the institutional Framework to facilitate Implementation of the Industrial Development Strategy*);
- (c) Matumizi yenye manufaa ya raslimali asili za nchi, hususan dhahabu (*Maximizing Benefits Retention from Natural Resources in Tanzania: The case of Gold*);
- (d) Kutambua na kutafiti shughuli na maeneo yaliyofanikiwa kiuchumi na kijamii hapa nchini (*Identification of Country's Socio-economic Success Stories*) ili kubaini namna ya kuyakuza au kuyaendeleza katika maeneo mengine;
- (e) Uchambuzi wa mahitaji ya rasilimaliwatu yenye ujuzi kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Taifa katika karne ijayo;

(f) Kuibua masuala ya ukuaji wa miji yatakayojuishwa katika Mpango Elekezi 2011 - 2025 ili kuonyesha mwelekeo wa ukuaji wa miji (*Identification of key Urbanization Issues to feed into the Long Term Perspective Plan 2011-2025*); na

(g) Utafiti kuhusu kujipanga upya kwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango katika kutekeleza majukumu yake mapya. (*The Re-Alignment of POPC Functions in the Context of its New Roles*).

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ilifanya uchambuzi wa mwelekeo wa maendeleo kiuchumi na kijamii katika ngazi za kisekta, kitaifa, kikanda, kimataifa na kubaini fursa na changamoto mbalimbali. Uchambuzi huo uliiwezesha Serikali kubuni namna ya kutanzua vikwazo vya maendeleo na kujiwekea malengo ya miaka mitano kupitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Aidha, ripoti ya utekelezaji wa dira imetoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kufikia malengo ya dira itakapofika mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zimefikiwa katika kujenga uwezo wa Tume ya Mipango kitaaluma ikiwa ni pamoja na:-

- (a) Kukamilika kwa kazi ya kubainisha muundo, ikama na tange la watumishi;
- (b) Wachambuzi wa sera wapya 22 wameajiriwa;
- (c) Watendaji Wakuu wa Tume ya Mipango wamefanya ziara za mafunzo katika nchi za Vietnam, China, Namibia na Brazil ili kujifunza jinsi taasisi za Mipango (*Think Tanks*) zinavyoendeshwa; na
- (d) Wafanyakazi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na wengine saba wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Tume ya Mipango iliendelea kutoa huduma za matibabu na chakula kwa watumishi walioathirika na UKIMWI na familia zao. Aidha, elimu kuhusu maambukizi ya VVU/UKIMWI iliendelea kutolewa kwa watumishi wote wa Tume ya Mipango kupitia Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi na mafunzo/semina maalum.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango, katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, ilijielekeza katika malengo yafuatayo:-

- (i) Kujenga uchumi wa kisasa (*modenization of the economy*);
- (ii) Kuiwezesha fola kupanga na kusimamia uchumi;
- (iii) Kuongeza uwezo na maarifa katika nchi kwa kutilia mkazo ubora wa elimu na raslimali watu ya nchi;
- (iv) Kuweka msingi wa miundombinu ya uchumi wa kisasa kwa kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya uhakika na uboreshaji wa miundombinu na huduma kwa uchumi; na

(v) Kutumia fursa za kijiografia katika kukuza uchumi wa kisasa wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, maeneo haya yalizingatiwa katika mapitio ya utekelezaji wa Dira ya mwaka 2025 na maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kama ilivyobainishwa katika hotuba yangu ya kuwasilisha Mpango hapa Bungeni, Mpango umejikita katika kujenga miundombinu ya msingi kwa maendeleo ya uchumi wa kisasa, kuruhusu matumizi ya raslimali za asili kwa ufanisi na tija na kuwezesha ushiriki mpana wa jamii katika ukuaji wa uchumi kwa kuharakisha maendeleo ya raslimali watu na upatikanaji wa mitaji. Aidha, Mpango umezingatia mahitaji ya msingi kuiwezesha Tanzania kutumia vyema na kimkakati fursa yake ya kijiografia kwa kuweka kipaumbele katika ujenzi wa bandari, reli, barabara, viwanja vya ndege na *TEHAMA*.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Bunge lako Tukufu, pamoja na kuridhia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016, liliafiki pia kuwa mwaka 2011/2012 uwe ni mwaka wa mpito kuwezesha maandalizi ya msingi kwa ufanisi wa utekelezaji wa Mpango. Hivyo, Mpango na Bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2011/2012 imezingatia utekelezaji wa masuala ya msingi kwa mwaka wa mpito, ikiwa ni pamoja na kuitangaza Dira 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika mwaka 2011/2012. Wananchi wataelimishwa juu ya Dira 2025 na Mpango wa Miaka Mitano na utekelezaji wake kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, warsha, semina, vyombo vya habari na machapisho maalum ikiwa ni pamoja na vipeperushi, makala na matangazo endelevu katika vyombo mbalimbali vya habari. Kwa ajili hii, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, pamoja na kuhaririwa upya, utafanyiwa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili, kuwezesha wananchi wengi kuuelewa na hivyo kushiriki katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kukamilisha utayarishaji wa Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano (2011/2012 - 2025/2026). Katika mwaka 2011/2012, Tume ya Mipango itashirikiana na wadau mbalimbali kukamilisha utayarishaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/2012 – 2025/2026). Mpango huo utajadiliwa na wadau katika ngazi mbalimbali na hatimaye kupitishwa na Serikali kabla kuwasilishwa rasmi Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuibua na kufanya tafiti za kina kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii, ajenda hii ni ya kudumu kwa kuzingatia majukumu ya Tume ya Mipango katika mwaka 2011/2012. Tume ya Mipango itakamilisha tafiti zilizoibuliwa mwaka 2010/2011. Aidha, Tume itaandaa Agenda ya Utafiti (*Research Agenda*) na Mpango kazi wa kufanya tafiti hizo kwa miaka mitano ijayo (2011/2012 – 2015/2016). Tume ya Mipango itaendelea kuratibu ukamilishwaji wa utafiti kuhusu hali ya ajira hapa Tanzania chini ya “*EAC Manpower Main Survey*”.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Tume ya Mipango itaendelea kujenga uwezo wake kwa kuajiri watumishi kutoa mafunzo kwa watumishi waliopo na kuboresha vitendea kazi. Aidha, Tume ya Mipango itaendelea kutafuta wataalam wenye uzoefu kutoka ndani na nje ya utumishi wa umma (Serikali, mashirika ya umma, *Diaspora*, sekta binafsi) na hata wataalam wenye uzoefu kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya kuundwa upya kwa Tume ya Mipango ni kuifanya kuwa kituo cha mawazo rejea na ushauri kwa Serikali (*Think Tank*), hususan katika masuala ya usimamizi wa uchumi na maendeleo ya jamii. Chombo hiki kimewekwa makusudi chini ya Ofisi ya Rais ili kiweze kushirikisha juhudhi mtambuka zinazofanywa na wadau wa maendeleo chini ya taasisi mbalimbali na kukiwezesha kuratibu na kutathmini utekelezaji wake. Pamoja na hayo, muundo wa Tume unatambua utajiri mkubwa wa fikra na mitazamo tofauti ya kimaendeleo katika jamii. Hivyo, Tume haiwezi kuwa na hati miliki ya mawazo. Kwa kutambua hili, muundo wake unatoa fursa kwa wadau mbalimbali kushiriki katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa wanayo nafasi adhimu ya kuchangia mawazo na kutoa ushauri kuhusu masuala yote yanayotekelizwa na Tume ya Mipango kwa niaba ya wananchi. Aidha, wananchi wanao wajibu wa kushauri na kutoa mapendekezo yao juu ya namna nzuri ya kutekeleza mipango iliyoandaliwa na Tume.

Mheshimiwa Spika, shughuli zinazopendekezwa kwa mwaka 2011/2012 zinalenga katika kusimamia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kuitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao umebainisha hatua zinazokusudiwa katika azma hiyo. Lengo la Taifa ni dhahiri kabisa katika hili. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, hatua za makusudi hazina budi kuchukuliwa kutanzua vikwazo na hivyo kuchochaea ukuaji wa uchumi. Kwa mantiki hiyo, Mpango huo umebainisha vipaumbele vichache vyta utekelezaji vitakavyozingatiwa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kwa kumalizia, napenda nikushukuru wewe binafsi, Bunge lako Tukufu na umma wote wa Watanzania kwa kufikia uamuzi wa kupitisha kwa kauli moja utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/2012 – 2015/2016 ambao ni sehemu ya Mpango Elekezi wa Utekelezaji wa Malengo ya Dira. Kwa mara nyingine, napenda kutumia fursa hii kuhimiza ushiriki wa dhati wa umma wa Watanzania katika utekelezaji wa Mpango. Kwa kufanya hivi, tutakuwa tumeudhihirishia ulimwengu umakini na uzalendo wetu. Ni vyema tukaelewana kuwa tumeamua kwenda vitani, vita ya kimaendeleo, na ili tushinde tunahitaji umoja na mshikamano wa kweli. Kwa umoja huo, sina shaka tutashinda na kufikia dhamira yetu ya Dira 2025. Katika vita hivi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wana wajibu wa kulinda na kutetea utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango. Aidha, ni wajibu wa kila mdau kukubali kuwajibika pale atakaposhindwa kufikia malengo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2010/2011 na shughuli zitakazotekelizwa kwa mwaka 2011/2012, naomba sasa kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida: Mishahara Sh. 2,354,123,000/=, Matumizi Mengineyo Sh. 4,835,436,000/=. Jumla Sh. 7,189,559,000/=. Shughuli za Maendeleo: hakukuwa na fedha za ndani na fedha za nje Sh. 200,000,000/= ambazo zitatumika kwa ajili ya *Survey* ya idadi ya watu. Jumla ya fungu zima la 66 Sh. 7,389,559,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, kwa Mwaka 2010/2011 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99(7) na 114(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais inahusisha mafungu sita, Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu); Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, tarehe 1 Juni, 2011, Kamati ilikutana Dar es Salaam kushughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, kama nilivyoeleza hapo juu. Katika kikao chake, Kamati ilipokea maeleo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2011/2012, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma akishirikiana na Mheshimiwa Mathias Chikawe - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) na Mheshimiwa Stephen Wasira - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mambo ambayo Kamati ilielezwa ni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais. Katika maeleo hayo, mtoa hoja alieleza pia kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2010/2011, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Vitendea kazi vya TAKUKURU kupewa umuhimu ili kuwezesha Taasisi kufanya kazi vizuri wakati wa uchaguzi ili haki iweze kutendeka, Serikali iliipatia TAKUKURU magari 120 ambayo yalisambazwa katika Ofisi zote za TAKUKURU

Wilayani na vifaa maalum vyatuhunguzi vilinunuliwa na kutumika kufuatilia nyendo na vitendo vinavyoikiuka Sheria za Uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kuifanya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Serikali kuwa Taasisi inayojitegemea. Uchambuzi wa kina wa majukumu ya Idara na ofisi zake za Kanda (Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma) umeanza kufanyika kwa kuangalia uwezekano wa kuifanya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kuwa Idara Inayojitegemea.

(iii) Upanuzi wa Majengo ya Chuo cha Utumishi wa Umma hususan mabweni na kuongeza uwezo wa kudahili, upanuzi wa majengo ya Chuo (mabweni na madarasa) katika matawi yake ya Dar es Salaam, Tabora na Mtwara haukuweza kufanyika katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, Chuo kimeweza kuongeza udahili wa wanachuo katika kozi za muda mrefu kutoka wanafunzi 6,029 mwaka 2009/2010 hadi wanafunzi 6,795 mwaka 2010/2011 kwa kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa zamu tatu kwa siku badala ya moja kama ilivyokuwa awali.

(iv) Serikali kuongeza umakini katika kutunza kumbukumbu za watumishi, kuwaendeleza watumishi na kuweka mikakati ya kuwabakiza katika Utumishi wa Umma, zoezi la kusafisha taarifa za kiutumishi na mishahara ya watumishi wa umma limeendelea kufanyika ambapo hadi sasa taarifa za Taasisi za Serikali 88 kati ya 356 zimekamilika ili kuwa na taarifa sahihi ambazo zitaingizwa katika mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara. Lengo ni kukamilisha kazi mwezi Agosti, 2011. Aidha, mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za watumishi umeboreshwa katika Wizara 27 kwa kuondoa majalada ya watumishi walioacha Utumishi wa Umma kwa njia mbalimbali (kustaafuli, kufariki, kuacha, kufukuzwa, kuachishwa) na kuyahifadhi katika kituo cha kuhifadhi kumbukumbu Tuli.

(v) Mchakato wa kurekebisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 (Sura ya 368) kwa lengo la kutenganisha biashara na uongozi wa umma uwahusishe wadau katika eneo hilo kwa namna itakayofaa, uchambuzi wa maeneo yanayotakiwa kufanyiwa marekebisheshwa umefanyika kwa kuzingatia usoefu wa mataifa mengine yenye utaratibu kama huo hususan Trinidad na Tobago, Marekani, British Columbia - Canada, Uingereza na Sri-Lanka. Hatua inayofuata ni kuwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Vyama vya Siasa, Waheshimiwa Wabunge, Taasisi za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali na Vyama vya Kitaaluma katika kujadili na kutoa mapendekezo yao ya namna bora ya kutenganisha biashara na uongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipoingeza Ofisi ya Rais na Serikali kwa ujumla kwa kutekeleza maagizo ya Kamati. Pamoja na pongozi hizo, kwa kuwa masuala mengi bado yako kwenye hatua za mwanzo za utekelezaji, Kamati inashauri yafuatiliwe kwa makini ili yaweze kutekelezeka kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia dhima, azima ya Serikali na majukumu ya Ofisi ya Rais, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Ofisi hii na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipotembelea Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilielezwa pamoja na mambo mengine kwamba kuna changamoto ya Watumishi wa Umma kutobadilika kifikra katika uwajibikaji ili kuwajibika kwa haraka na kuzingatia muda, maadili na kanuni za kazi. Kamati inashauri Watumishi wa Umma wabadilike kifikra katika uwajibikaji (*change of attitude*) kwani ndio wenyewe dhamana ya kusimamia na kutekeleza sera zinazoongoza maendeleo kama vile Dira ya Taifa (*National Vision 2025*), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) pamoja na Ilani ya chama kilichopo madarakani. Hivyo, wafanyakazi wanapaswa kuwajibika kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuondoa tatizo hili la kubadili fikra (*change of attitude*) linadhoofisha jithada za Serikali za kukuza uchumi kwa kuimarisha utawala bora utakaowezesha kuwepo na uwajibikaji, uadilifu na usikivu katika kuwashudumia wananchi. Aidha, Kamati inashauri kupanua wigo wa upatikanaji wa wataalamu na kuweka vivutio maalumu ili kuimarisha maadili ya watumishi wa umma na kupambana na tatizo la rushwa na kuvujisha siri za Serikali kwa ngazi na kada zote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa mageuzi na maboresho yanayoendelea katika Utumishi wa Umma. Pamoja na hayo, bado Kamati inashauri Serikali ifuatilie utendaji kazi wa Watumishi wa umma wasiowajibika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeanzisha utaratibu wa Mfumo wa Wazi wa Upimaji Utendaji Kazi, *Open Performance Appraisal System (OPRAS)* ambapo mwajiri na mwajiriwa wanaingia mkataba na kukubaliana juu ya kazi zitakazofanyika na hatimaye kutathmini kwa uwazi kama malengo yamefikiwa, Kamati inashauri kuwa ni vyema mfumo huu ukatiliwa mkazo sana kwani ndiyo unaoweza kusaidia kurudisha nidhamu ya uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Aidha, Kamati inashauri Wizara kuangalia upya fomu hizi na kuziboresha ili upimaji huo ufanyike kama inavyotakiwa ili kukidhi mahitaji ya *OPRAS*.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwajibikaji katika Utumishi wa Umma, Kamati inashauri kuwa Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) ambayo kila Taasisi imeitoa ifuatwe kama ilivyoelezwa kwenye mikataba hiyo, na uwepo utaratibu wa wateja kueleza kukiukwa kwa mikataba hiyo na hatua kuchukuliwa ili kuongeza uwajibikaji katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inalazimika kuamini kuwa kuna baadhi ya Watumishi katika Ofisi za Serikali ambao wanafanya kazi kwa mazoea bila kuzingatia maadili ya kazi zao kwa kufika kazini kwa muda wanaotaka na kutoka kazini muda wanaotaka bila kufuata Kanuni na Sheria za Kazi. Kamati inashauri kwamba wafanyakazi wafuate taratibu za kazi mara wanapotaka kutoka kazini, yaani kuomba ruhusa na kumwachia au kukaimisha majukumu mfanyakazi mwingine ili ofisi za Serikali ziendele kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha mwaka huu, inaonesha mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 5.6 kwa kipindi kilichoishia Desemba, 2010 hadi asilimia 6.4 Januari, 2011 na kuendelea kupanda hadi asilimia 8.6 mwezi Aprili, 2011. Kasi hii ilitokana na kupanda kwa bei za nishati, maji, makazi, usafirishaji, vyakula na vinywaji. Mfumuko huu wa bei umesababisha hali ya maisha kwa Watumishi wa Serikali kuwa ngumu kwa kushindwa kumudu kupanda huko kwa maisha. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kusema kwamba kwa mwaka huu wa fedha itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa mwaka huu wa fedha, Kamati inashauri kwamba ni vyema maslahi ya watumishi yakaangaliwa upya kwa kuoanisha na hali ya maisha ya sasa ili kuwapunguzia makali ya maisha watumishi wa Serikali na kuongeza uwajibikaji zaidi. Aidha, kwa vile bado kuna watumishi ambao wana madai mbalimbali kama vile madai ya likizo, uhamisho na kupandishwa vyeo ambayo wanaidai Serikali, Kamati inashauri Serikali kuwa baada ya kulipa madeni hayo, iwe makini kutozalisha madeni mapya na hasa kutotoa uhamisho kwa mtumishi iwapo hakuna fedha za uhamisho wake.

Mheshimiwa Spika, kuna watumishi wanaofanya kazi kwenye hospitali zilizoingia mkataba kati ya ama Wilaya au Misheni na Serikali ambazo zinajulikana kama *District Designated Hospital (DDH)*. Baada ya mkataba huo, baadhi ya watumishi wameamua kuajiriwa na Serikalini lakini kumekuwa na tatizo la kurekebishiwa mishahara yao ili iendane na ya Serikali. Kamati inashauri Wizara kulifuatilia suala hili kwa karibu zaidi ili watumishi hawa waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na maoni ya Kamati kuhusu Ofisi za Serikali kutumia samani zinazozalishwa hapa nchini kwetu. Hatua hii itasaidia kutangaza miti yetu na hasa Mnninga, kutoa ajira kwa wananchi na kukuza uchumi kulikoni kutumia fedha nyingi kuagiza samani toka nje ya nchi ambazo hazina ubora.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia vitabu vya bajeti, Kamati imegundua kwamba Serikali inatumia fedha nyingi sana katika ukodishaji na ukarabati wa majengo yanayotumiwa na Taasisi/Wizara zake kama Ofisi. Mfano, taasisi moja inakodisha jengo kwa Sh. 300,000,000/= kwa mwaka na inakarabati jengo hili kwa Sh. 200,000,000/= kiasi ambacho ni kikubwa sana. Kamati inashauri kuwa ili kuondokana na gharama hizi, kila Wizara/Taasisi ambazo hazina majengo yao kwanza zifanye jitihada za kupata viwanja Dar es Salaam na hata Dodoma ambapo ni Makao Mkuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ni muhimu sana hasa kwa waajiriwa wapya ili waelewe wajibu na taratibu mbalimbali za ufanyaji kazi Serikalini kwa vile wengi huwa ni mara yao ya kwanza kufanya kazi. Kwa vile agizo hili lilishatolewa siku za nyuma, Kamati inashauri Wizara ifuatilie taasisi zake kuona kama kweli mafunzo haya yanafanya na kama waajiri kwenye bajeti zao wanatenga fedha hizo. Mafunzo haya yatasaidia suala zima la maadili katika utumishi wa umma, Kanuni za Utumishi na kuondoa tatizo la kuvuja siri za Serikali kwani inawezekana wakati mwingine siri zinavuja kutokana na waajiriwa kutojua wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, Siku ya Utumishi wa Umma ni kutambua mchango wa watumishi katika maendeleo ya nchi na inasheherekewa kila tarehe 23 Juni, duniani kote. Lengo ni kukutana na wadau kuwaeleza utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Kwa mara ya kwanza siku hii imefanyika Afrika na Tanzania ndiyo imepata bahati ya kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa maadhisho haya. Siku ya Utumishi wa Umma ilifanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 20 - 23 Juni, 2011 ambayo imekwenda sambamba na maadhisho ya miaka 50 ya uhuru wa Tanzania na kauli mbiu zilikuwa: “*Mabadiliko na Ubunifu wa Viongozi katika Utumishi wa Umma Utaleta Maisha Bora kwa wote*”, “*Mkataba wa Kanuni na msingi ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni Chachu ya Kuimarisha Utoaji Huduma bora kwa Umma*” na “*Miaka 50 ya Utumishi wa Umma Tanzania*”

Maadhisho haya yameshirikisha washiriki zaidi ya 400 wakiwemo Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia Maendeleo ya Uchumi na Jamii, Mawaziri na Viongozi wa Serikali, wawakilishi kutoka Asasi za kiraia, wasomi, sekta binafsi na Mashirika ya Kimataifa na ya Kikanda. Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikisha siku hii muhimu na hii ni dhahiri kuwa Tanzania inaaminika na kukubalika Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira inayo jukumu la msingi la kuendesha mchakato wa ajira wa Watumishi wa Umma kwa niaba ya Waajiri nchini kwa mujibu wa Kifungu cha 29(4) cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya mwaka 2007. Watumishi hao ni wale wa kada za kuingilia katika utumishi wa umma (*entry points*). Sekretarieti ina wajibu wa kutangaza, kusaili, kutoa matokeo ya usaili na kuwapangia vituo watumishi wapya kwa mujibu wa matokeo ya usaili.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipokutana na Sekretarieti hii, ilipewa taarifa ya utekelezaji wa majukumu pamoja na changamoto wanazokumbana nazo. Kamati inaipongeza Sekretarieti kwa kazi nzuri, japo bado inayo kazi kubwa ya kumaliza changamoto nyingi ilizonazo kama vile kukidhi matarajio ya Waajiri, kuondoa malalamiko ya upendeleo wa ajira katika Utumishi wa Umma, upatikanaji wa watumishi wenye sifa za kuajiriwa kwenye Ofisi za Sekretarieti ya Ajira zitakazoanzishwa Mikoani, upatikanaji wa ofisi na vitendea kazi, ugumu wa kutambua waombaji waliofukuzwa kazi na wanaodanganya sifa zao. Aidha, Kamati ilielezwa kwamba Waajiri bado wanao wajibu wa kubainisha ikama zao, kutengea bajeti katika nafasi hizo na baadaye kuingia Mikataba ya Ajira kwa wale wanaopangiwa vituo vy'a kazi na Sekretarieti ya Ajira. Majukumu mengine ya waajiri ni kuwapandisha vyeo, kuwaendeleza, nidhamu na kufuutilia utendaji bora wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kwa kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma isaidie Sekretarieti ili kukabiliana na changamoto. Aidha, bajeti finyu inayotengewa Sekretarieti ya Ajira ili kukabiliana na changamoto hizi ziangaliwe, hasa kwa kuzingatia kwamba Sekretarieti ya Ajira bado ni changa na hivyo Serikali ichukue hatua za makusudi ili iweze kuiongezea bajeti itakayoweza kuwasaidia angalau kupunguza changamoto walizonazo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba hatua za haraka zichukuliwe ili kufungua ofisi za Mikoani na kwenye Kanda ikiwa ni pamoja na kuwapatia watumishi wenye sifa ili kupunguza tatizo ambalo linajitokeza hivi sasa kwamba inapotokea nafasi za ajira hata kama nafasi hiyo iko Mikoani, inawalazimu watahiniwa wa nafasi hizo kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kufanyiwa usaili.

Kamati inashauri pia kwamba kwa vile Sekretariati ya Ajira ina majukumu mengi ya kuajiri hasa Mikoani na kwenye Halmashauri, ni vyema jukumu la kuajiri watumishi kada ya Uhudumu na Madereva, likaachwa kwenye Mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri kuwa ili kuondoa dhana ya upendeleo iliyojengeka mionganoni mwa Halmashauri kwamba kuna Halmashauri zinapelekewa watumishi mapema hata kama maombi yalichelewa, ni vyema Sekretarieti ikachukua jukumu la kutoa elimu ya jinsi inavyofanya kazi kwa wadau wake wote kitu ambacho kitasaidia kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Sekretarieti ya Ajira inatangaza ajira kupitia Vyombo vya Habari kama magazeti, redio au televisheni na hivyo kufanya wale wanaoishi maeneo ambayo hawawezi kupata mawasiliano ya vyombo hivyo au wale wasio na uwezo kushindwa kujua kama kuna kazi zimetangazwa na kutuma maombi. Kamati inapendekeza kuwa Sekretarieti ya Ajira ipeleke matangazo ya nafasi za kazi hadi kwenye ngazi za Halmashauri na iwajibike kubandika kwenye Ofisi husika na kwenye maeneo mbalimbali ili wananchi waweze kupata taarifa.

Mheshimiwa Spika, suala la kutolewa kwa vibali vya ajira limeonekana kuwa ni changamoto. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwa Serikali iliangularie kwa makini suala hili kwani linachelewesha maendeleo kwa kukosa raslimali watu ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Sekretarieti ina changamoto ya kuajiri watumishi walioachishwa kazi katika Utumishi wa Umma kutokana na makosa mbalimbali, mfano, ukosefu wa maadili na ubadhirifu wa mali za umma, inapendekezwa kuwa Sekretarieti iwe na Kanzidata (*Database*) ambayo itaweka kumbukumbu ya watumishi wote walioachishwa kazi ili kuzuia uwezekano wa kuajiriwa tena katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu MKURABITA katika kutekeleza majukumu yake, Kamati iliweza kutembelea MKURABITA (Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania) na kujionea utendaji wa majukumu ya Ofisi hiyo. Baada ya kupewa taarifa ya jinsi mpango wa MKURABITA inavyofanya kazi, Kamati inapendekeza kwamba ni vyema Serikali ikasambaza mpango huu kwa nchi nzima kuliko inavyofanyika hivi sasa ambapo Wilaya huchaguliwa kwa kutumia vigezo vilivyofanyiwa tathmini. Elimu inabidi itolewe kwa umma kuhusu MKURABITA na kwamba kazi ya urasimishaji kwa dhana ya MKURABITA ni shirikishi, hivyo wananchi inabidi wachangie gharama katika kazi ya urasimishaji raslimali na biashara za wanyonge katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa kwamba utekelezaji wa MKURABITA kwa nchi nzima unagharimu fedha nyingi na ndio maana hadi sasa ni Hati za Kimila (*Customary Certificate of Right of Occupancy*) inayotolewa kwa mujibu wa

Sheria Na.5) 808 tu zimeshaandaliwa na kuwafikia wananchi, wakati Hati za Kimila 17,093 zimeshaandaliwa lakini zitatolewa kwa wananchi baada ya Masijala za Ardhi za Vijiji vyao kukamilika. Aidha, jumla ya Hati Miliki (*Certificate of Right of Occupancy*) 847 zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria Na.4 zimekabidhiwa kwa wahusika na jumla ya mashamba 51,036 yamepimwa. Kamati inaishauri Serikali kuptitia Wizara ya Ardhi iweze kusaidia tatizo la kutokamilika Masijala za Ardhi za Vijiji na hivyo kuwawezesha wananchi kupata hati miliki zitakazowasaidia kutumika kama dhamana katika kupata mikopo kutoka kwenye mabenki kwani hati miliki za kimila ni uthibitisho halali wa shamba na kitambulisho cha uraia ni uthibitisho kamili wa mmiliki wa shamba na hivyo kwa pamoja vinatoa uhakika kwa benki juu ya aliyekopeshwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo mazuri ya mpango wa MKURABITA, bado kuna changamoto ambazo Kamati inaomba zifanyiwe kazi mapema ili kutoa fursa kwa wananchi wengi kufaidika na mpango huu. Moja ya changamto hizo ni sheria zinazoleta mgongano na hivyo kusababisha upungufu na ugumu katika utekelezai wa Mpango wa MKURABITA. Sheria hizo ni Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 na Sheria ya Mipango Miji Na.8 ya 2007 ambazo ni mionganoni mwa sheria zinazotumika katika kusimamia sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata taarifa kwamba sheria hizi tayari zimekwishawasilishwa Serikalini kwa mapendekezo ya marekebisho. Kamati inaishauri Serikali iharakishe mchakato wa marekebisho ya Sheria hizi, ziweze kuletweta mbele ya Bunge lako Tukufu na hivyo kufanyiwa marekebisho ili kuzifanya zitekelezwe kwa urahisi na kuleta mafanikio yaliyokusudiwa ili kuepusha migongano na hivyo kuweshesha mpango wa MKURABITA kutimiza azma yake ya kusambaa nchi nzima ifikapo mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, ili mpango wa MKURABITA uweze kutimiza malengo yake, inabidi Serikali iwe na dhamira ya kweli ya kuiwesha kwani hivi sasa MKURABITA imekuwa haifikii malengo kutokana na siyo tu ufinyu wa bajeti, bali pia hata hiyo bajeti wanayopangiwa kwa kiasi kikubwa haiwafikii. Mfano, bajeti ya utekelezaji wa MKURABITA imekuwa ikipanda kutoka shilingi za Kitanzania bilioni tatu mwaka 2008/2009 hadi shilingi bilioni sita mwaka 2010/2011. Hata hivyo, MKURABITA imekuwa ikipokea fedha pungufu katika kila mwaka wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, MKURABITA ilitengewa Sh. 6,000,000,000/= lakini hadi Machi, 2011 ilipokea Sh. 1,700,000,000/= tu.

Mheshimiwa Spika, sababu hii imekuwa ikipunguza kazi ya utekelezaji wa Mpango wa urasimishaji katika Wilaya na hivyo kusababisha hata utekelezaji wa awamu ya Tatu ya Mpango huu ambayo ndiyo hasa iliyokusudiwa kuleta mabadiliko yaliyokusudiwa kuanza 2008 badala ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba utekelezaji wa awamu ya tatu ulioanza Julai, 2008 unasuasua kwa sababu ya upungufu mkubwa wa fedha za kugharamia shughuli za urasimishaji raslimali na biashara za wanyonge vijijini na mijini. Kamati inaishauri Serikali itafute fedha za kutosha, hususan kwa kupata mkopo maalum wa masharti nafuu kutoka vyombo vya fedha vya Kimataifa kama Benki ya Dunia, Benki

ya Maendeleo ya Afrika na kadhalika utakaotumika kutekeleza Mpango Kazi kabambe wa urasimishaji raslimali za biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza ukubwa wa sekta isiyo rasmi katika uchumi wa Taifa letu sambamba na kupanua na kukuza sekta rasmi na hivyo kuimarisha ushiriki wa wananchi katika sekta rasmi za uchumi, Kamati inashauri Serikali ianzishe Taasisi ya Umma (*Executive Agency*) ya kuongoza urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Taasisi hii ikiundwa itakuwa chombo muhimu katika suala zima la kuongoza shughuli za urasimishaji na uratibu wa ukubwa wa sekta isiyo rasmi katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza mafanikio makubwa yaliyoletwa na Mfuko wa *TASAF* awamu ya kwanza tangu ulipoanzishwa mwaka 2000, kwa kipindi cha miaka minne na kufanikiwa kutekelezwa katika Halmashauri 40 Tanzania Bara, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua mchango mkubwa wa Mfuko huu katika miradi mbalimbali ya kijamii kama vile shule, zahanati, maji, miradi ya ujenzi, umwagiliaji na mingineyo. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa na utendaji usioridhisha wa *TASAF II* hasa baada ya shughuli ya *TASAF* kuhamishiwa kwenye Halmashauri wakati hakukuwa na maandalizi kwa watumishi katika Halmashauri kufanya uwezeshaji ngazi za jamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba kuna malengo ya *TASAF II* hayajafanikiwa kwani pamoja na awamu hii kuanza mwaka 2005 katika Halmashauri zote za Tanzania Bara na Visiwani, kwa kipindi chote cha utekelezaji kwa miaka mitano bado imekabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo za maombi mengi ya miradi ya jamii yenye thamani ya mabilioni kuliko uwezo wa *TASAF II*, baadhi ya Halmashauri kutozingatia taratibu za matumizi ya fedha, baadhi ya wanasiasa kuzuia jamii kuchangia miradi yao, hivyo kukiuka dhana ya ushirikishaji jamii na umiliki wa miradi na nyinginezo.

Mheshimiwa spika, Kamati inadhani changamoto za Mfuko huu zingeweza kupatiwa ufumbuzi iwapo kungekuwepo na Sheria ya Kuanzisha *TASAF* na hivyo kuifanya kuwa endelevu. Kamati inaishauri Serikali kuangalia na kuwezesha mchakato wa kuleta Muswada wa Sheria ya Kuanzisha *TASAF* ili Bunge lako Tukufu liweze kuipitisha na hivyo kuwezesha Mfuko huu kuwepo kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea *TASAF* na inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta eneo jipya Dodoma kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za *TASAF* kwani eneo ambalo Ofisi hiyo ipo hivi sasa ni finyu na kwa hakika inawawia vigumu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*Presidential Trust Fund*) ulianzishwa mwaka 1983. Wazo la uanzishaji lilitoka kwa aliyekuwa Waziri Mkuu kwa wakati ule Marehemu Edward Moringe Sokoine. Shughuli za mfuko huu zilianzishwa rasmi mwaka 1984 na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *PTF* ilisajiliwa rasmi kama Shirika

lisilo la Kiserikali (*NGO*) tarehe 02, Agosti, 1988 chini ya Sheria ya Tanzania ya ‘*Trustee Incorporation Ordinance Chapter 375*’.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kusaidia jitihada za Serikali za kuendeleza uchumi wa nchi na kuwakwamua watu wa hali ya chini kwa kuwawezesha kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi na shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuongeza kipato na ajira kwa madhumuni ya kupunguza umaskini na kuongeza uzalishaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi mijini na vijiji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kupongeza juhudu kubwa zinazofanywa na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) ambapo umewezesha vikundi mbalimbali nya jamii kupata mikopo ya ada za shule na mikopo ya ununuzi wa viwanja, Kamati imegundua kwamba riba inayotolewa na mfuko ya 2.5% kwa mwezi ambapo kwa mwaka ni 30% ni kubwa kwa wananchi wengi wa Tanzania na hivyo hata wigo wa kufikia taasisi nyingine bado ni mdogo sana kwani mpaka sasa imetoa mikopo 12 tu kwa Jeshi la Polisi yenye thamani ya Sh. 7,600,000/=. Kamati inapendekeza kuwa suala la riba liangaliwe upya ili kuwasaidia wananchi kuinuka kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza agizo la Kamati na hivyo kuendelea kuboresha mazingira ya Utendaji kazi wa TAKUKURU (Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa). Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Taasisi hii na kujionea utekelezaji wa majukumu ya TAKUKURU pamoja na kukutana na Uongozi na wafanyakazi wa Taasisi hii. Kamati inatoa pongezi kwa Taasisi kwa kusambaza Maafisa wake nchi nzima na kufanikiwa kutoa elimu kwa njia mbalimbali mfano vipeperushi, televisheni na radio.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba, pamoja na jitihada za Taasisi hiyo, bado wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa Bajeti unaosababisha Taasisi kutofikia malengo yake. Ikumbukwe kwamba hivi sasa Taasisi hii imesambaa mpaka Wilayani lakini ni jambo la kusikitisha kwamba Wilaya nyingi zinahudumiwa na Maafisa wasiozidi watatu. Hali hii imesababisha malalamiko mengi kwa jamii kwani idadi hiyo ndogo ya Watendaji imekuwa haikidhi haja ya mahitaji katika kuzuia, kupambana na kutoa elimu ya rushwa. Mfano mzuri ni wakati wa uchaguzi ambapo ni dhahiri taasisi hii ilizidiwa na hivyo kusababisha malalamiko ya vitendo vya rushwa kuwa vingi. Tatizo la ufinyu wa Bajeti limesababisha Taasisi kutokuwa na vitendea kazi vya kutosha na hivyo kutotekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazidi kupendekeza kwamba Serikali iongeze Bajeti zaidi kwa Taasisi hii ili iweze kufanya shughuli zake kisayansi zaidi kuliko ilivyo sasa. Mfano, kwa mwaka wa Fedha 2010/2011, Taasisi hii iliendesha kesi 299 Mahakamani ambapo kesi 103 zilikamilika na kati ya hizo zilizokamilika, Taasisi ilishinda 48 na kesi 55 Watuhumiwa hawakupatikana na hatia. Hii inaashiria kwamba Taasisi bado inayo changamoto ya mafunzo zaidi, mbinu na utaalamu wa upelelezi na ukusanyaji wa ushahidi ili iweze kufanikisha majukumu na kufikia malengo iliyojipangia. Kamati inapendekeza kuwa Taasisi ifanye utafiti zaidi na kuishauri Serikali kuhusu mianya ya rushwa na hasa rushwa kubwa kubwa kwenye madini, maliasili na kwenye Mikataba ambayo Serikali imekuwa inapata hasara kubwa na kulikosesha Taifa mapato ya kuendeshea shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru Serikali kwa kuanzisha ushirikiano kati ya TAKUKURU, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati inaamini kwamba lengo la ushirikiano huo ni kuongeza kasi ya kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa katika eneo la manunuzi kadri yanavyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati inashauri kwamba eneo lolote iwe Wizara, Idara au Halmashauri panapotokea tuhuma za rushwa, isiishie tu kusema kwamba kuna tuhuma za rushwa au hati chafu bali wahuksika mapema iwezekanavyo wapelekwe kwenye vyombo vya dola ili Sheria iweze kuchukua nafasi yake dhidi ya watuhumiwa hao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kazi nzuri wanazozifanya japo wanazifanya katika mazingira magumu. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi za Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma huko Dar es Salaam. Kutokana na mazingira duni ya Kiofisi Kamati inashauri Serikali ama izifanyie matengenezo Ofisi za Sekretariati au itafute eneo jipya la kujenga ofisi hizo.

Kamati inarejea tamko lake ililolitoa katika taarifa yake kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 kwamba, majengo yanayotumiwa na Sekretarieti hiyo hayalingani na hadhi yake. Mengi ya majengo hayo ni chakavu na inatia shaka kwamba kweli yanaweza kuhifadhi nyaraka muhimu za viongozi. Kamati inasisitiza kuwa jitihada za kujenga eneo jipya zikamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inashauri Kanuni na Taratibu za Sekretarieti hii zifanyiwe maboresho ili pia ziweze kuwashughulikia Viongozi wa kada za chini, tofauti na utaratibu wa sasa wa kushughulikia kada za juu tu. Hii ni kwa sababu viongozi wa kada za chini kwa kiasi kikubwa ndio wanaoshughulika na jamii na uwezekano wa kutumia madaraka yao vibaya ni mkubwa. Hivyo, Sekretarieti iangalie uwezekano wa kuwawajibisha viongozi hawa.

Mheshimiwa Spika, mmomonyoko wa maadili hivi sasa ni changamoto kubwa mionganoni mwa jamii. Chanzo cha tatizo hili ni pamoja na ukosefu wa elimu ya kizalendo ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikijengwa kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kurudisha mfumo wa vijana kuhudhuria mafunzo ya JKT pindi wamalizapo mafunzo yao ili kuwajengea moyo wa kupenda nchi yao maana hao ndio wanaotarajiwa baadaye kuwa viongozi. Hii ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuingiza somo la uzalendo katika mitaala ya elimu ya Msingi na Sekondari hadi Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maoni na ushauri ambao Kamati yangu ilioutoa iliposhughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais. Napenda nilieleze Bunge lako Tukufu kuwa baada ya ufanuzi uliotolewa na Ofisi hiyo, hatimaye Kamati yangu iliyapitisha makadirio ya Ofisi hiyo na kuruhusu yawasilishwe Bungeni kwa hatua inayofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, kwanza, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudui, busara, hekima, uchapakazi na umakini uliopo katika Serikali na ofisi hii ya Rais.

Aidha, napenda kumshukuru pia kwa kutuendeshea meli yetu salama kuelekea kwenye ile nchi ya ahadi yenye wingi wa maziwa na asali na nasema Mungu ambariki sana Mheshimiwa Rais aendelee kuongoza nchi yetu kwa amani na utulivu na Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, tunakupongeza kwa busara zako katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Hawa Abdulrahmani Ghasia - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa wakati wote Kamati tulipochambua makadirio ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote wanaonisikiliza na kipekee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2011/2012. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Utawala, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mwenyekiti, Mheshimiwa Angella J. Kairuki - Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mheshimiwa Zahra A. Hamadi, Mheshimiwa Mussa H. Kombo, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Jaddy S. Jaddy, Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina na Mheshimiwa Jason S. Rweikiza. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah - Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Charles Mloka - Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Peter Magati na Asia Minja - Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI -
MHE. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7)

ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana tarehe 30 Mei, 2011 na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Fungu 66. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2010/2011; hapo awali kabla ya kubadilika kwa Kanuni za Bunge, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ilikuwa ikiwajibika chini ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Aidha, Kamati ya Fedha na Uchumi inaipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kutoa mapendeleko na ushauri mzuri kwa Tume ya Mipango na ikaweza kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha kuandaa Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2011/2012 - 2015/2016 pamoja na sera za uchumi jumla.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 13 Juni, 2011, Kamati ya Fedha na Uchumi iliwasilisha Taarifa yake kuhusu Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012-2015/2016) ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025. Katika taarifa hii, Kamati ilitoa mchango mkubwa ikiwemo ushauri na maelekezo kwa Tume ya Mipango ili kuhakikisha inatekeleza majukumu yake ipasavyo katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kamati inaanini kwamba ushauri uliotolewa utazingatiwa.

Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2011/2012. Maoni na ushauri wa Kamati utakaotolewa hapa kwa Tume ya Mipango ni mwendelezo wa maoni yaliyotolewa wakati wa uwasilishwaji wa Taarifa yake kuhusu Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025, hivyo Kamati inapenda kusisitiza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango uzoefu unavyoonyesha kwenye nchi nyingi zenyenye mfumo huu, pamoja na India, China na kadhalika, ni chombo au taasisi inayotakiwa kuwa na nguvu na uwezo wa kiutendaji. Hii ni kwa sababu Tume ya Mipango ni Kituo cha Mawazo Rejea na Ushauri kwa Serikali (*Think Tank*) katika nyanja zote. Kwa vile Sheria iliyozishwa Tume ya Mipango ilikuwa ni Sheria ya Mwaka 1989, upo umuhimu kuifanyia marekebisho Sheria hii ili tuanze vizuri na twende na wakati. Tume ya Mipango ni Chombo/Taasisi ya Kuratibu Mipango ya Nchi nzima. Kamati inashauri Sheria ihuishwe na itoe nguvu zaidi kwa Tume ya Mipango katika masuala ya ufuatiliaji, tathmini, usimamizi na uratibu wa mipango ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile majukumu ya Tume ni makubwa, pamoja na yale ya kuelekeza na kuongoza mipango na uchumi wa nchi, ili ianzo kazi vizuri maeneo matatu yafuatayo yatekelezwe.

(1) Sheria itakayohuishwa iipe Tume fursa ya kujenga uwezo wake wa kiutendaji (*capacity building*);

(2) Kwa vile Tume ni lazima ijikite katika masuala ya utafiti. Ni lazima itengewe fedha za kutosha ili ifanye kazi zake kufuatana na mazingira halisi ya sasa yanayotawaliwa na *TEHAMA*; na

(3) Kwa sababu Tume ni Kituo cha Mawazo Rejea na Ushauri katika Masuala ya Kiuchumi na Kijamii ni lazima ipate wataalamu wenye ujuzi na stadi za kutosha, pamoja na uwezo wa kujenga mtandao wa kitaalamu kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ina jukumu kubwa la kusimamia raslimali ya Taifa na kuishauri Serikali kuhusu matumizi bora ya raslimali, kusimamia na kutoa miongozo kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii, kusimamia mipango ya Serikali, na kuchambua sera za kiuchumi. Kamati imeona kuwa kutokana na majukumu haya mazito ya Tume hii, maeneo yafuatayo yaangaliwe ili itekelezaji kikamilifu wajibu wake kama *think tank* na isukume utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo

(1) Fedha zinazotengwa kwa ajili utekelezaji wa majukumu ya Tume hazitoshi. Hii inaashiria haja ya kuongeza uwezo wa kifedha kwa Tume ya Mipango;

(2) Idadi ya wafanyakazi bado ni ndogo ukilinganisha na majukumu ya Tume ya Mipango. Kwa vile sasa tayari tumeshaandaa Mpango wa Miaka Mitano, upungufu huu hauna budi kurekebishiwa;

(3) Tume itafsiri Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025 kwa lugha ya Kiswahili ili ueleweke kwa wananchi wote. Izingatiwe kuwa ufuatiliaji na utekelezaji wa Mipango hii itafanyika zaidi kwenye ngazi za Halmashauri waliko wananchi wengi;

(4) Tafiti zinazofanywa na Tume ya Mipango zichapishwe na ziwafikie wananchi ili waelewe kwa kina masuala ya kiuchumi na kijamii, kama yalivyoainishwa katika Mipango inayopangwa; na

(5) Tume lazima iwezeshwe na ijengewe mazingira ya kuvutia akili (*attract brains*) za nchi kufanya kazi katika Tume katika fani na nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzingatia kuepukana na utaratibu wa kutokutoa maamuzi ya ushauri unaotolewa na matatizo ya urasimu, Kamati inaishauri Serikali kuwa ianzishe Idara ndani ya Tume ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopendekezwa na Tume katika ngazi ya kitaifa na kimatafa na taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo iwasilishwe Bungeni. Utekelezaji bila ya Usimamizi na Ufuatiliaji hautaleta tija.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Tume ya Mipango kuhakikisha kuwa inatimiza mambo ya msingi yafuatayo:-

(1) Tume ya Mipango ishirikiane kikamilifu na Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi za Serikali ili kusimamia na kuratibu kikamilifu Miradi ya Maendeleo ya Taifa,

Wizara, Mikoa na Halmashauri za Wilaya ili malengo na matokeo yanayotarajiwa yasimamiwe na kutekelezwa kikamilifu katika ngazi hizi husika;

(2) Tume ya Mipango ibuni mbinu mbadala za kujiiondoa katika utegemezi mkubwa kwa kutegemea vyanzo vya kodi ya ndani peke yake (*tax revenue*), badala yake iangalie vyanzo vingine visivyo vya kodi (*non tax revenue*) vitakavyosaidia kugharamia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kiwango kikubwa;

(3) Serikali ihakikishe kuwa Bajeti ya Tume inawiana na Mipango itakayopangwa kila mwaka;

(4) Tume ihakikishe kuwa wakipitisha mawasilisho ya Bajeti za Wizara zinaendana na mipango iliyokusudiwa. Mantiki ya utaratibu huu ni kuondoa pengo la utendaji (*disjoint*) kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha ili kuimarisha utendaji, ufuutiliaji na utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano ulioandaliwa.

(5) Tume ya Mipango ikishirikiana na Wizara ya Fedha zijenge mawasiliano na Wizara zote hasa zile za kipaumbele ili kufuatilia na kutathmini (*monitoring and evaluation*) kila baada ya hatua ya utekelezaji wa Mpango uliofikiwa na Wizara husika. Uimarishaji wa kutoa na kupata taarifa uboreshwe kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kamati moja ya changamoto kubwa ya Tume ni utaratibu utakaowekwa wa uelewa wa Mpango. Mipango hii ya Taifa ni lazima ieleweweke vizuri kwenye ngazi za utawala za chini ili ziweze kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mipango. Ufuutiliaji ukifanyika ngazi za juu tu tutarudia mapungufu na makosa yaliyojitokeza awali. Hali hii inahitaji kuimarishwa kwa Chuo cha Mipango Dodoma ili Taifa lipate wataalamu wa kutosha watakaofanya kazi hadi ngazi za vijijini.

Mheshimiwa Spika, programu ya mpango iendelee kuweka msisistizo wa kukidhi mahitaji ya mafunzo ya stadi za kazi pamoja na Elimu ya Juu ya Vyuo vikuu, Tume lazima iangalie namna gani Mpango wa Maendeleo utajielekeza katika mafunzo mbalimbali ya stadi za kazi ili kujenga uwezo (*capacity*) kwa wananchi, hasa tukizingatia azma ya uchumi wetu tunataka kuwekeza kuelekea kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango lazima iangalie namna itakavyofanya kazi katika ngazi mbalimbali kuanzia chini mpaka juu. Tume lazima iangalie namna gani itakavyotekeliza maelekezo kutoka ngazi za juu na kupeleka ngazi za chini (*Top-Down*), waangalie vilevile kutoka ngazi za chini kwenda ngazi za juu (*Down-Top*) ili kugundua na kuibua fursa za uchumi zilizoko katika maeneo husika kuziingiza katika mipango. Utaratibu huu itarahisisha Mpango wa Taifa kueleweka vizuri katika ngazi zote na kusaidia kufuatilia utekelezaji wake. Dhana hii lazima iandamane na mazingira bora ya miundombinu ya kuibua yale maeneo muhimu ya vipaumbele (*matching of priorities and supportive priorities*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu - Mheshimiwa Steven Masato Wassira - Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji wa Tume Bwana Philipo Mpango, Manaibu Makatibu, Watendaji pamoja na

wataalamu wa Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda - Mwenyekiti Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Makamu Mwenyekiti, na wajumbe ni Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Oseler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Amour Abdulla, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Alhaj. Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Luaga Joelson Mpina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashilillah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi - Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Rais, Fungu 66 - Tume ya Mipango, kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona bado tunawasikiliza Wenyeviti sasa tunaingia na Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani. Sasa na wenyewe wanatakiwa watumie karibu nusu saa kila mmoja, yaani Msemaji Mkuu upande Katiba, Sheria na Utawala na nusu saa kwenye Uratibu. Sasa ningependa nao waweze kutoa mchango wao wamalize halafu mchana tuanze kujadili, kuliko tukatishe halafu warudi tena mchana. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu a-move tuongeze muda wa nusu saa kufuatana na kifungu cha 28(2).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kwa kutumia kifungu 150 kutengua

kifungu namba 28(2) kinachosema Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11.00 isipokuwa kama Spika akiona inafaa, Bunge linaweza kuendelea kukutana kwa muda usiozidi dakika 30 au kusitishwa wakati wowote kabla ya saa saba mchana baada ya kuwahoji Wabunge ili wasemaji wanaofuata waweze kupata muda wa kukamilisha shughuli yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KIILMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Bunge liliafiki hoja ya Kutengua Kanuni*)

MHE. SUZAN A. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI- OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba upokee shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha, 2011/2012, kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 99 (7) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya umma wa Watanzania na kwa mema yote ambayo amekuwa akitujalia.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa natoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wetu Mkuu wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Freeman Mbewe, Naibu Kiongozi wetu - Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kwa kunitfea kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii. Aidha, nawashukuru Wabunge wenzangu wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza wajibu wangu wa kuwatumikia Watanzania kwa umakini na kwa uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee, nawashukuru Katibu Mkuu wa CHADEMA, aliyekuwa Mgombea wetu wa Urais, Dk. Willbrod Peter Slaa na makamanda wote wa CHADEMA nchi nzima kwa kazi kubwa tuliyofanya ya kunadi ilani na sera za chama chetu hata wananchi wakatuelewa na kutupa ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. (*Makofî*)

Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, naishukuru familia yangu hususan mume wangu Boney Ngowi, pamoja na watoto wangu, ndugu na jamaa wote ambao wamenivumilia sana wakati wote nikiwa katika kadhia za kisiasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili watumishi wa umma wawe wenye ufanisi wa kutosha, Serikali inapaswa kuhakikisha wanaofuata Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma zinazosisitiza tabia na mwenendo unaozingatia mambo yafuatayo:-

Kutoa Huduma Bora, Utii kwa Serikali, Bidii ya kazi, kutoa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu, kuwajibika kwa umma, kuheshimu sheria, kutumia taarifa kwa usahihi

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa bado Serikali haijaweza kusimamia maadili na kanuni hizo za utumishi wa umma kikamilifu. Matumizi mabaya ya madaraka, ufisadi, rushwa, uzembe, mishahara hewa, ni sehemu tu ya ukiukwaji wa kanuni hizo tunaoendelea kuushuhudia kila mwaka. (*Makofi*)

Kimsingi, kukosekana kwa umakini, utovu wa dhamira ya dhati ya kuboresha sekta hii, na ufuutiliaji usioridhisha wa utendaji kazi katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ndiyo unaoendelea kusababisha maadili ya kazi kukiukwa na uwajibikaji wa watumishi wa umma kuzidi kuperomoka.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo sugu la watumishi kutojali muda. Watumishi wengi hawajali muda wa kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu na zaidi hushughulika na mambo mengine yasiyoleta tija kwa Taifa.

Suala hili linasababisha kila aina ya maboresho katika sekta ya umma kushindwa kuleta tija. Waheshimiwa Wabunge, wamelalamika barua hazijibowi kwa wakati, na zinapojibowi inaweza kuchukua miezi sita hadi mwaka jibu kupatikana. Jambo hili ni kasoro mojawapo katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia tatizo kubwa sana la utunzaji kumbukumbu kiofisi pamoja na zile zinazowahusu watumishi wa umma wenyewe. Hali hii imekuwa ikisababisha kuwe na ugumu wa kushughulikia masuala tata ya kiofisi. Pia ukosefu wa kumbukumbu nzuri za watumishi umekuwa ukisababisha usumbufu mkubwa wakati wa kushughulikia taratibu za mafao na mirathi ya watumishi pindi wanapokuwa wamefariki na au wamestaafu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza, ili kuwe na uwajibikaji wa kutosha na kuepusha matatizo yote hayo, ni vyema kukaanzishwa mfumo ambao utamlazimisha kila mtumishi wa umma kila wiki au mwezi kuwa na kipimo kinachoonyesha kufikiwa au kutofikiwa kwa majukumu yake aliyopangiwa, yaani *measurable performance*.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kwamba kwa njia hii, mazoea ya Watendaji kuingia ofisini na kuzifanya ofisi kuwa vijiwe vyta kujadili matukio ya mitaani yatapungua na kila mtu atawajibika kulingana na majukumu yake na atapandishwa ngazi kwa kutumia utaratibu huu. Vinginevyo, kila siku sekta ya utumishi wa umma itaendelea kuwa na watumishi wasiotimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na kawaida ya kuwahamishia katika vituo vingine vyta kazi watumishi wa umma wanaobainika kufanya makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa kazi zao. Kambi ya Upinzani tunapinga utaratibu huu, kwani unazidi kuchocha uzembe na ukiukwaji wa maadili na kanuni za utumishi wa umma. Kwa mtindo huu, Mtumishi anajua hata akiharibu hatasimamishwa au kufukuzwa kazi, bali atabadilishiwa tu kituo cha kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuchochaea uwajibikaji wa kutosha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ianze kuchukua maamuzi magumu ya kinidhamu au/na ya kisheria dhidi ya mtumishi yeote anayekiuka maadili ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Umma wenyewe Ulemavu, Shirika la Afya Duniani linakadiria kuwa katika kila jumuia, asilimia 10 ya watu wake wana aina fulani ya ulemavu wa kimwili au kiakili. Tanzania inakadiria kuwa na watu zaidi ya milioni nne wenyewe ulemavu wa aina mbalimbali. Idadi ya watu wenyewe ulemavu katika Utumishi wa Umma bado ni ndogo. Hali hii inatokana na idadi ndogo ya watoto wenyewe ulemavu ambao wanapata elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa idadi kubwa ya watu wenyewe ulemavu, bado Sekta ya Utumishi wa Umma haina mazingira rafiki ya kazi kwa watu wenyewe ulemavu kuweza kufanya kazi bila shida.

Kambi ya Upinzani, inataka kufahamu Menejimenti ya Utumishi wa umma inachukua hatua gani za makusudi ili kuhakikisha kuwa watu wenyewe ulemavu wanapata fursa za rafiki ya kufanya kazi na kuhudumiwa ndani ya sekta ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, maslahi duni kwa watumishi wa umma bado ni changamoto kubwa katika Taifa letu. Suala la maslahi duni lina sura kuu mbili. Sura ya kwanza ni mishahara isiyokidhi mahitaji ya familia za watumishi wa umma. Walimu, wauguzi na waganga wa ngazi mbalimbali ni mionganoni mwa watumishi wanaopata mishahara isiyotosheleza mahitaji muhimu ya familia.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kama tulivyosema wakati wa kuwasilisha bajeti mbadala, tunaitaka Serikali ianze mara moja safari ya maboresho makubwa ya mishahara ya watumishi wa umma kwa kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka Sh. 135,000/= ya sasa hadi kufikia Sh. 315,000/= kwa mwezi, ili angalau watumishi waweze kukabiliana na makali ya kupanda kwa gharama za maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili linazingatia ukweli kuwa kima cha chini cha sasa cha Sh. 135,000/= kwa mwezi hakiwezi kutosheleza mahitaji ya msingi ya familia. Mathalan, kwa familia ya Kitanzania yenyewe watu sita, yaani mke, bwana na watoto wanne, mshahara wa Sh. 135,000/= ni sawa na mwanafamilia mmoja kutumia Sh. 22,500/= kwa mwezi au Sh. 750/= kwa kila mmoja kwa siku. Kiasi ambacho ni kidogo kuliko anachotengewa mfugwa kwa ajili ya chakula kwa siku ambacho ni kiasi cha Sh. 2,420. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa *formula* zinazotumika kwa sasa kuongeza mishahara ya watumishi ni za kibaguzi na upendeleo. *Formula* ya kuongeza mishahara kwa kufuata kiwango cha asilimia sawa kwa watumishi wa aina zote huwapendelea zaidi wenyewe mishahara ya juu na huongeza zaidi pengo la mapato (mishahara) kati ya watumishi wa kada za juu na chini.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, mwaka 2007/2008, nyongeza ya mishahara kwa asilimia 7.2 kwa watumishi wote ilisababisha nyongeza ya Sh. 5,420/= tu kwa watumishi waliokuwa wanapata kima cha chini cha mshahara cha Sh. 75,340/= na kufikia Sh.

80,750/=. Lakini nyongeza hiyo hiyo ya asilimia 7.2 kwa watumishi wa kada ya juu waliokuwa wanapata mshahara wa Sh. 1,795,000/= mwaka 2006/2007 ilifanya wawe wameongezewa Sh. 129,000/= na hivyo mishahara yao kufikia Sh. 1,924,000/= mwaka 2007/2008. Kiwango hiki kilichoongezwa kwa watumishi wa kada ya juu kilizidi kiwango cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, hali hii imefanya kuwepo kwa ubaguzi wa kimfumo, hivyo kuchocha kuibuka kwa matabaka na pengo kubwa zaidi baina ya walionacho na wasionacho. Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali irekebishe utaratibu wake wa kutumia kiwango kimoja (*Fixed rate*) katika kurekebisha mishahara ya wafanyakazi ili ipandishe kwanzana kima cha chini cha mshahara hadi Sh. 315,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali iweze kuongeza kima cha chini cha mshahara hadi Sh. 315,000/= kwa mwezi. Tunaishauri Serikali kupunguza posho na huduma za kuwalipa watumishi wa ngazi za juu. Kwa mfano, hakuna huduma za umeme, maji, wala simu zinazolipiwa kwa watumishi wa kima cha chini ila kima cha juu.

Watumishi wanaolipiwa huduma hizo ni wale watumishi wa ngazi za juu tu. Watumishi wa Serikali ngazi ya *TGS* hadi *TGSM* wanalipiwa *unit 1290* za umeme na *unit 450* za simu na watumishi wa Serikali ngazi ya *TGSN-Q LSSJ (1-3)* na *LSSP (1-6)* wanalipiwa *unit 1480* za umeme na *unit 650* za simu.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea pia kuishauri Serikali kupunguza misamaha ya kodi, kutumia vyanzo vya mapato vilivyoainishwa katika hotuba yetu ya bajeti mbadala na kuachana na matumizi yote yasiyo ya lazima, ili iweze kupata fedha za kutosha zitakazoiwezesha kuongeza na kupandisha kima cha chini cha mshahara hadi Sh. 315,000/= kuanzia mwaka wa fedha wa 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali na nyongeza ya mishahara, dai lingine kubwa la muda mrefu la wafanyakazi ni kupunguziwa kodi inayotozwa kwenye mishahara ya wafanyakazi (*PAYE*). Kambi ya Upinzani tunaendelea kusisitiza kuwa Sheria ya Kodi ya Mapato ifanyiwe marekebisho ili kushusha kiwango cha chini kabisa cha *PAYE* mpaka asilimia tisa na kiwango cha juu mpaka asilimia 27. Uamuvi huu utawezesha wafanyakazi kubakia na fedha na hivyo kutumia katika uchumi na kukuza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sura ya pili ya maslahi duni ni mafao duni ya uzeeni yanayoshughulikiwa na taratibu au mifuko ya pensheni (mfano, *SSSS*, *PPF*, *LAPF*, *NSSF*, *PSPF* na *GEPF*).

Mafao haya duni nayo yanachangiwa na sababu kadhaa, lakini mbili kubwa ni mishahara duni wanayolipwa watumishi wa umma wakati wakiwa kwenye utumishi wa umma, jambo linalosababisha michango yao kwenye mifuko ya pensheni kuwa duni vile vile; na tofauti ya mafao yatolewayo na mifuko mbalimbali kama nilivyoitaja hapo juu. Kuna mifuko inayotoa mafao mazuri kwa wastaafu (Mfano, *GEPF*, *PSPF LAPF*) na mingine inayotoa mafao duni (Mfano, *SSSS*, *PPF*).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwe na utaratibu wa namna moja wa kukokotoa mafao ya uezini, malipo ya mkupuo na pensheni ya kila mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatutakuwa tumetenda haki kama hatutazungumzia dhuluma iliyowakuta watumishi katika Vyuo Vikuu vya Serikali waliokuwa kwenye utaratibu wa SSSS. Utaratibu huu uliwhusu Wahadhiri na Maprofesa walioajiriwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kabla ya mwaka 1978. Kwa mujibu wa utaratibu huu, mstaafu alipata malipo ya mkupuo mmoja tu, ambayo yako chini ya yale wayapatayo watumishi wanaoshughulikiwa na *PSPF*, *GEPF* na *LAPF*. Kwa utaratibu wa SSSS, mstaafu hakulipwa Pensheni ya kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Vyuo Vikuu waliokuwa kwenye utaratibu wa SSSS wamekuwa wakijadiliana na Serikali ili waingizwe kwenye utaratibu wa pensheni ya kila mwezi kwa muda mrefu bila mafanikio. Hivi karibuni, Serikali imetoa waraka ambao unaelekeza kuwa wahadhiri/maprofesa ambao watastaafu kuanzia Machi, 2011 ndio tu wataingizwa kwenye utaratibu wa pensheni ya kila mwezi wa *PPF*. Haifahamiki Serikali ilitumia vigezo gani kufikia uamzi huu. Tatizo ni kwamba wale ambao tayari walikwishastaafu (1993 – Februari, 2011) hatima ya dai lao la pensheni ya kila mwezi haijulikani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Serikali itende haki kwa kuwaingiza wote waliokuwa kwenye utaratibu wa SSSS waliostaafu na wale ambao hawajastaafu kwenye utaratibu wa *PPF* bila kuwabagua, na wastaaafu wote ambao sio wengi sana waanze kulipwa pensheni ya kila mwezi kuanzia Machi, 2011. Serikali itafute fedha za dharura ili zoezi la kuwalipa wastaaafu hawa lianze mara moja. Kwa kuwa Serikali hii ni sikivu, basi itasikiliza kilio cha siku nyingi cha watumishi hawa ambao wamedhulumiwa haki yao ya pensheni ya kila mwezi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Kikao cha Baraza la Taifa la Chama cha Walimu Tanzania (*CWT*), walimu bado wanaidai Serikali malimbikizo ya madeni yao yanayofikia jumla ya shilingi bilioni 13. Kambi ya Upinzani imesikitishwa sana na mateso ya muda mrefu wanayopata walimu wa nchi hii. Licha ya mishahara yao kuwa midogo, bado wameendelea kunyanyasika kwa kutolipwa madai yao ya muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali hii sikivu kusikia kilio hiki cha muda mrefu cha walimu na kuwalipa fedha zote za malimbikizo ya madeni yao mapema iwezekanavyo kabla hawajaanza kufanya mgomo kama ambavyo wamekuwa wakisema, lakini wakakubali kuwa wavumilivu. Tunaitaka Serikali iache kuutumia vibaya uvumilivu huu wa walimu, iwalipe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mfumo wa utoaji pensheni kwa wafanyakazi, Kambi ya Upinzani tunaisihi Serikali itekeleze mapendekezo yafuatayo:-

Kuanzisha utaratibu utakaowawezesha wachangiaji katika mifuko hii kuwa na sauti katika uendeshaji wa mifuko husika kwa kuteua wawakilishi katika Bodi zinazosimamia mifuko hiyo. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa mifuko hii ya utoaji wa pensheni nchini na kuwa na mafao bora na yanayowiana. Kupanua wigo wa mifuko hii kwa kusajili wafanyakazi /watu wengi kutoka sekta binafsi. Kuanzisha pensheni maalum kwa ajili ya wazee wote nchini wenye umri wa miaka 65 na kuendelea bila kujali kama walikuwa wafanyakazi wa Serikali ama la.

Mheshimiwa Spika, utawala bora, uongozi bora na utawala wa sheria, pamoja na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ni nguzo ya msingi katika kukuza uchumi wa Taifa lolote duniani.

Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2010/2011, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora umeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa uwajibikaji wa utawala kwa umma, licha ya Serikali kutamba kuchukua hatua madhubuti katika kusimamia uadilifu na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa mgawanyo kamili wa madaraka mionganoni mwa mihimili ya utawala kumesababisha mfumo wetu wa utawala kuwa na mianya inayoruhusu vyombo mbalimbali vya kiutendaji Serikalini kuingiliwa na wanasiasa na kusababisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, ili kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria, ni muhimu kuweka na kudumisha uwiano thabiti katika mgawanyo wa madaraka mionganoni mwa mihimili ya utawala, yaani Dola, Bunge, Mahakama na taasisi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, suluhisho la kudumu la tatizo hili la utawala bora ni kuandikwa kwa Katiba mpya ya nchi itakayojenga misingi ya kulinda demokrasia, kulinda haki za wananchi na kutoa fursa kwa wananchi kuwawajibisha viongozi wao watakaposhindwa kutimiza wajibu wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) iliendelea kuonyesha udhaifu mkubwa katika kukabiliana na tatizo la rushwa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyosemwa katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, bado TAKUKURU hajawa na uwezo wa kutosha wa kuchunguza malalamiko yote ya rushwa yanayopokelewa. Pia ina uwezo mdogo wa kuchunguza na kufungua mashtaka ya rushwa, licha ya Serikali kutamba kuwa imeongezewa meno kupitia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya udhaifu huo wa TAKUKURU, rushwa imezidi kuota mizizi katika taasisi nyeti za utawala wa umma kama ilivyoonyeshwa na matokeo ya utafiti wa *East Africa Bribery Index*. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo,

Jeshi la Polisi lilihika nafasi ya kwanza nchini na ya tano katika Ukanda wa Nchi, Afrika Mashariki likiwa limepewa asilimia 65.1.

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyotolewa na taasisi ya *Agenda Participation* chini ya mradi unaoitwa “*Corruption Trackers*” inaonyesha kuwa TAKUKURU ina udhaifu mkubwa katika mchakato mzima wa kuchunguza na kusimamia kesi Mahakamani, jambo ambalo limesababisha Serikali kushinda asilimia moja tu ya kesi zote zilizofunguliwa Mahakamani kati ya mwaka 1995 na 2009. Aidha, jitihada za dhati hazijaonekana za kushughulikia Watumishi wa Umma waliotajwa kwenye orodha ya mafisadi waliohusika na kashfa za Kagoda, Meremeta, *Deep Green, Richmond, IPTL* na mikataba mingine inayoendelea kulitia hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, madai ya fedha za rada. Kambi ya Upinzani inatambua kuwa Bunge lako Tukufu litatenga muda maalum kwa ajili ya kujadili suala la madai ya fedha za rada kiasi cha takribani paundi za Kiingereza milioni 29.5 za faini na fidia sawa na takribani shilingi bilioni 75.2 za Kitanzania, ambazo kampuni ya uuzaji wa zana za kivita ya *BAE Systems* ya nchini Uingereza imeamriwa kutulipa baada ya kubainika kuwepo ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu katika ununuzi wa rada hiyo. Kwa kuwa suala hili linagusa misingi ya utawala bora, Kambi ya Upinzani kwa niaba ya mamilioni ya Watanzania tunaowawakilisha, tunachukua fursa hii kutoa msimamo na ushauri ufuataao.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunataka wahusika wote waliohusika na kashfa ya rada (akiwemo aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa wakati huo), wachukuliwe hatua zote za kinidhamu na kisheria kwa kufikishwa Mahakamani haraka iwezekanavyo, kwani uchunguzi uliofanywa na Idara ya Upelelezi wa Ufisadi (*SFO*) ya nchini Uingereza, umeonyesha kuwapo kwa hongo na ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu katika mchakato mzima wa ununuzi wa rada hiyo. Kambi ya Upinzani tunaona kuwa, bila watuhumiwa hawa kuchukuliwa hatua, ni dhahiri kuwa Taifa haliwezi kuwa na uhakika wa kuzilinda vizuri fedha hizo za rada pindi zikilipwa, pamoja na fedha nyingine za umma ambazo zinaweza kuendelea kupotea kwa sababu umekuwa ni utamaduni wa Serikali yetu kutokuchukua hatua kwa wahusika wa rushwa kubwakubwa za namna mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, kwa niaba ya mamilioni ya Watanzania wote tunaowawakilisha, tunapinga fedha za rada kulipwa kupitia Serikali yetu, kwani haiaminiki, hasa ikitiliwa maanani kuwa fedha hizo zilipotea mikononi mwa Serikali hiihii iliyopo madarakani na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Serikali kuwajibisha wahusika wa upotevu huu na hata wakati kesi hiyo ikiwa Mahakamani Serikali yetu haikuomba kuunganishwa kwenye kesi hiyo ila leo wako mstari wa mbele kudai fedha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunapinga nia ya kampuni ya *BAE Systems* ya kutaka kulipa fedha hizo kupitia Asasi Zisizo za Kiserikali za Uingereza, kwani hatua hiyo itakuwa ni udhalilishaji mkubwa kwa Watanzania wote, ni sawa na kutuambia kwamba sote hatuna uwezo wa kuamua na kusimamia mambo yetu. Badala yake, tunataka Bunge lako Tukufu lijadili na liazimie kuanzishwa kwa “Akaunti ya muda

ya fedha za Rada” itakayosimamiwa kwa pamoja na wawakilishi wa Asasi zisizo za Kiserikali za Tanzania na wawakilishi wa sekta binafsi na Mwakilishi wa Serikali. Kampuni ya *BAE* ilipe fedha hizo mapema iwezekanavyo kupitia akaunti hiyo.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia lichukue wajibu wa kujadili na kuamua kipaumbele cha matumizi ya fedha hizo chini ya usimamizi wa Akaunti hiyo, kwa kuzingatia zaidi maslahi ya wengi kadri fedha hizo zitakavyoonekana kutosha. Aidha, Azimio hilo limpe mamlaka Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kukagua matumizi ya fedha hizo kama kwa fedha nyingine za umma.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya fedha za umma. Moja ya majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ni kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali. Hata hivyo, ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zimeonyesha kukithiri kwa matumizi mabaya ya fedha za umma kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, kulifanyika malipo ya mishahara kwa watumishi wa Serikali kuu waliostaifu, waliokufa na watoro kazini, ya jumla ya shilingi 1,842,607,565.29. Kwa mwaka huohuo, kulifanyika malipo kwa watumishi wa Serikali za Mitaa waliostaifu, kuachishwa kazi na watoro, ya jumla ya shilingi milioni 583,221,297. Kwa mwaka huohuo, kulikuwa na mishahara ya watumishi wa Serikali za Mitaa isiyolipwa na ambayo haikurejeshwa Hazina ya jumla ya Sh bilioni 1.1. Aidha, Ripoti ya Haki za Binadamu ya “*State Department*” ya Marekani ya mwaka 2010, imethibitisha kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali ilipoteza jumla ya shilingi bilioni 26.6 kwa kulipa mishahara hewa kwa watumishi wa taasisi saba tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunataka uchunguzi wa kina ufanyike na wahusika wote wanaofanikisha wizi huu wa fedha za umma wachukuliwe hatua haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti zaidi matumizi ya fedha za Serikali na kuzielekeza zaidi kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi, Kambi ya upinzani tunasisitiza pendekezo letu tulilolitoa wakati wa kuwasilisha bajeti mbadala, kwamba tunataka mfumo mzima wa kulipana posho za vikao (*sitting allowances*) uondolewe katika utumishi wa umma bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*). Kambi ya Upinzani haturidhishwi hata kidogo na mwenendo wa utendaji wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, ulioanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kwa kuwapa mikopo na maarifa. Kwanza, haturidhishwi na utendaji wa mfuko huu kwani umekuwa ukiwzesha idadi ndogo sana ya wananchi, huku wengi wakiachwa pembezoni.

Pili, tumebaini kuwa mikopo inayotolewa na mfuko huu imekuwa na riba sawa na taasisi nyingine zinazofanya biashara ya kukopesha fedha. Kambi ya Upinzani tunahoji, je, faida ya riba inayotengenezwa na mfuko huu inakwenda wapi, mbona haionekani

katika mapato vya Serikali? Kama ni “*revolving fund*”, je ni lini mfuko huu utaanza kuijendesha wenyewe?

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, mfuko huu unakabiliwa na tuhuma za kutapeli wananchi kwa kuwapa ahadi za uongo au zisizotimizwa kwa wakati. Mathalani, Julai 15 mwaka jana, zaidi ya wanachama 200 wa Mfuko huu wa Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, walivamia ofisi za Makao Makuu ya taasisi hiyo yaliyopo Morocco Jijini Dar es Salaam wakilalamika kutapeliwa fedha zao za amana. Wanachama hao kila mmoja alikuwa ameambiwa atoe shilingi 18,000 kama kiingilio cha uanachama na amana ya shilingi 250,000 kwa ahadi ya kukopeshwa shilingi milioni moja katika kipindi cha juma moja, lakini hawakupewa mkopo huo kwa wakati. Lalamiko lingine lilikuwa ni kuongezeka kwa vipengele vya masharti ya uombaji wa mikopo hiyo. (Chanzo cha taarifa hizi ni habari iliyotoka katika Gazeti la Mwananchi la Julai 16, 2010 na mtandao wa *You Tube* unaoonesha video ya malalamiko ya wanachama hao).

Mheshimiwa Spika, wananchi wamefikia hatua ya kuufananisha Mfuko huu wa Rais na kampuni ya *DECI*, inayotuhumiwa kuendesha mchezo wa upatu kinyume cha sheria. Kwa ujumla, mfuko huu umekuwa ukichafua jina, hadhi na cheo cha rais. Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani, tunalitaka Bunge lako Tukufu kuitia Kamati zake lifanye uchunguzi maalum kuhusu uendeshwaji wa Mfuko huu na kushauri namna bora ya kuuendesha.

Mheshimiwa Spika, taasisi za wenza wa Marais. Kumeibuka mtindo wa wake za Marais kuanzisha taasisi zao binafsi zisizo za Kiserikali lakini zinazotumia magari, jina na hadhi ya Kiserikali (ya kuwa Mke wa Rais), kuvuta fedha za wafadhili kwa ajili ya kufanya kile kinachoitwa “kusaidia jamii”. Mifano ya taasisi hizi ni Taasisi ya Maendeleo ya Wanawake (WAMA) ya Mama Salma Kikwete na Mfuko wa Fursa Sawa kwa wote (*EOTF*) wa Mama Anna Mkapa.

Mheshimiwa Spika, tabia ya kila Mke wa Rais kuanzisha taasisi yake tena baada tu ya mumewe kuingia madarakani, inatoa picha mbaya kuwa taasisi hizi huanzishwa kwa maslahi binafsi zaidi kuliko kusaidia jamii; kwa kuwa Mke wa Rais ni taswira ya Rais mwenyewe ambaye ndiye Kiongozi wa Nchi. Kambi ya Upinzani tunaona ipo haja kwa Serikali kuandaa utaratibu rasmi wa kuwa na taasisi moja tu yenye nguvu itakayokuwa inaongozwa na Mke au Mume wa Rais aliye madarakani kama mlezi na kupokewa na Wake au Waume wa Marais wajao, ili kuondoa picha hii mbaya ya kila mmoja kujianzishia taasisi au mfuko wake.

Mheshimiwa Spika, nyumba za Serikali. Kambi ya Upinzani tunataka Serikali ijieleze kwa niniilitumia mabilioni ya fedha za walipa kodi kujenga nyumba za kuishi watumishi wa Serikali lakini baadaye ikaziwa.

Mheshimiwa Spika, wakati nyumba za Serikali zilijengwa na kuuzwa, baadhi ya Mawaziri wanakaa hotelini. Kwa siku gharama ya hoteli hizo huwa ni kati ya laki tano na laki sita. Tukipiga hesabu ya kiongozi mmoja aliyekaa hotelini kwa miezi saba tangu aapishwe, ni dhahiri jumla ya shilingi milioni 110.2 zitakuwa zimetumika. Je, ni viongozi

wangapi wanakaa hotelini na mpaka sasa wameliingizia Taifa hasara kiasi gani? Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya viongozi waliouza nyumba hizo?

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ni mengi na yanalenga kuhakikisha kuwa tabia na mienendo ya Viongozi wa Umma inazingatia misingi ya maadili yaliyoainishwa katika Sheria Namba 13 ya mwaka 1995. Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni vema mchakato wa Katiba Mpya uzingatie pia jinsi ya kuiondoa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma chini ya Ofisi ya Rais, ili iwe taasisi huru na iwajibike moja kwa moja kwa Bunge.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Sekretarieti hii ni kuwasilisha kwa Rais mapendekezo ya Baraza la Maadili kuhusu uchunguzi wa tuhuma za ukiukwaji wa maadili lakini kwa mfumo huu wa sasa, iwapo tuhuma zinazochunguzwa zitawahusu Viongozi Wakuu, akiwamo Rais mwenyewe, je, taarifa hizo zitapelekwa wapi? Au ndio kusema Rais wetu ni malaika, hapaswi naye kuchunguzwa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na upungufu ambao tumeutaja kuwa unasababisha taasisi hii kutokuwa huru katika utendaji wake kazi kwa mujibu wa sheria, pia kuna tatizo la sheria inayosimamiwa na taasisi hii. Sheria hii haisimamiwi kabisa kwani kuna baadhi ya watumishi walijaza taarifa za uongo na imekuja kujulikana kwa umma kuwa walitoa taarifa za uongo lakini hadi sasa hawajachukuliwa hatua zozote za kisheria. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa, Idara hii kuwa chini ya Ofisi ya Rais ni kiini macho kwa Watanzania na hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba nchi hii bado ina matatizo makubwa ya utawala bora na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tulitarajia kuwa Sekretarieti ya Maadili ya Utumishi wa Umma ingekuwa ni mfano katika suala la posho za vikao, lakini kwa bahati mbaya nayo inaomba shilingi milioni 28.6 kwa ajili ya kulipia posho katika vikao mbalimbali vyta ofisi. Jambo hili halikubaliki kabisa na ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, maadili ni jambo la msingi sana na Ofisi hii ndio kinara wa uratibu wa maadili katika nchi yetu lakini kinachosikitisha Idara ya Ukuzaji wa Maadili imetengewa shilingi 44,280,000/= tu kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa kampeni katika Wilaya na Mikoa. Tukipiga hesabu kwa Wilaya 133 nchini, ni dhahiri kuwa kila Wilaya itakuwa imetengewa shilingi 332,932/= tu kwa ajili ya shughuli za kuelimisha maadili kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka Watendaji wa Serikali waelewe maana ya maadili kama nguzo kuu ya uwajibikaji basi fedha hii ni dhahiri kuwa haitoshi kwa kampeni hiyo. Kibaya zaidi fedha hii yote inatoka nje. Katika kitabu cha mafungu ya Kitengo cha Usimamizi wa Anuai za Jamii zimetengwa shilingi 320,000,000/= kwa ajili ya kutoa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili kwa watumishi 30 wanawake na watumishi wenye ulemavu. Hili ni jambo la kupongezwa hasa kwa kuwa tukitilia maanani jinsi mfumo dume ulivyowakandamiza wanawake na kuwafanya wakose fursa ya elimu. Pamoja na pongezi hizi, Kambi ya Upinzani tunataka kujua utaratibu

utakaotumika kuwapata wanafunzi hawa, je, mwaka jana walienda wangapi na mpango huu ni endelevu? Kambi ya Upinzani inasikitika kuona kuwa Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha wanawake kielimu bado fedha yote hii inatoka kwa wafadhili na kwa maana hii wasipotoa kwa wakati wanawake hawa wanawenza kukosa fursa ya kujiendeza kitaaluma hii haipendezi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, uadilifu, uwazi na uwajibikaji wa Serikali. Uwazi na uwajibikaji ndiyo kiini na msingi wa utawala bora, sio tu katika Taasisi na Idara za Serikali bali hata katika sekta binafsi na Mashirika ya Umma. Uwazi na uwajibikaji hauwezi kusimamiwa kikamilifu na kudaiwa bila kuwepo kwa utawala wa sheria .

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba viongozi wetu wamekuwa wakizungumzia sana utawala bora na hata kuona kuwa ndiyo kibwagizo sahihi cha kuzuia migogoro, bado hali halisi inaonyesha kuwa mifumo na misingi ya uwajibikaji bado havijapewa uzito unaostahili. Muathirika mkubwa wa kutokujibika kwa Viongozi wa Umma katika utendaji wao wa kila siku, ni mwananchi wa kawaida ambaye maisha yake ya kila siku yanategemea maamuzi ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, dhana ya uwazi na uwajibikaji imekuwa ni gonjwa sugu ambalo hadi sasa halijapatiwa tiba ya kutosha licha ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali katika sekta hiyo ya utawala.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeshtushwa kuwa kuna mfuko maalum wa uadilifu, uwazi na uwajibikaji ulioanzishwa mwaka 2007 kwa lengo la kuweka msingi wa utawala bora. Kwa kuwa kila asasi inayoundwa inatakiwa kuwa na mpango kazi unaoonyesha nini kinatakiwa kutekelezeka na kwa muda gani; Kambi ya Upinzani inataka kufahamu uanzishwaji wa mfuko huu unalenga kufanikisha nini ambacho Watanzania wanawenza kukipima.

Mheshimiwa Spika, tunahoji suala hili kutokana na ukweli kwamba kila mara Ofisi ya Rais au Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikiandaa Semina Elekezi kwa Watendaji Wakuu wa Serikali kufundishwa maadili ya utawala bora. Kwa mtazamo wetu hii maana yake ni kwamba maelekezo yanayotolewa ni jinsi ya kuweka dhana nzima ya utawala bora ki-vitendo. Aidha, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa hadi mtumishi anateuliwa katika ngazi ya juu ya utumishi wa umma ni dhahiri kuwa mtendaji huyo anapaswa kuwa anaelewa misingi ya utawala bora, kinyume na hivyo, mtendaji huyo basi hana sifa ya kuwa kiongozi na kupewa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Kambi ya Upinzani tumbaini kuwa Serikali haijatenga fedha zozote za maendeleo katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 kwa ajili ya kujiendeza matumizi ya teknolojia ya mtandao katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/2011 unaonesha kuwa kituo cha mafunzo kwa njia ya mtandao kilifanya utafiti wa awali wa uanzishwaji wa vituo vishiriki katika Mikoa ya Arusha, Morogoro, Dodoma na Mwanza kwa kutumia

mkongo wa Taifa. Kinachosikitisha pamoja na kazi kubwa kufanyika, ni fedha iliyotengwa kutoendana na kasi ya TEHAMA katika dunia yetu ya sayansi na teknolojia. Tunataka fedha zitengwe kwani hali ikiendelea hivi, Tanzania tutajikuta tunabaki wasindikizaji ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge hili, kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutoa maoni yetu, naomba nikishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo – CHADEMA kwa kunteuwa kugombea Kiti cha Ubunge Jimbo la Karatu na kushinda kwa kishindo. Napenda pia kutoa shukurani za kipekee kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kunteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Nami natoa ahadi kwake kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, natumaini mambo yatakuwa mazuri na tutashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Dkt. Willibrod Peter Slaa - Katibu Mkuu wa CHADEMA na Mbunge wa miaka 15 wa Jimbo la Karatu, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuwaletaa wananchi wa Karatu maendeleo na kuifanya CHADEMA kuwa Chama kiongozi Karatu, hata nami nikapata uhalali wa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kupitia CHADEMA. Ninasema kuwa kwa baraka za Mwenyezi Mungu, viatu ulivyoniachia vinanitosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kwa wananchi wa Jimbo la Karatu kama sitawashukuru kwa imani kubwa walijonayo kwangu na kwa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), nami nawaahidi kuwa nitaitunza na kuiheshimu imani yao kwangu, kuendelea kushirikiana nao kuleta maendeleo katika Jimbo na Wilaya yetu na mwisho kukifanya CHADEMA kuwa Chama Kiongozi kwa Wilaya na kwa nchi nzima katika uchaguzi wa mwaka 2015, nasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika mchakato mzima wa kuandaa hotuba hii, nasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mahusiano ya madhehebu ya dini, asasi zisizo za kiserikali na Serikali. Kwa mujibu wa sheria inayounda Asasi Zisizokuwa za Kiserikali Namba 24 ya

mwaka 2002, asasi hizo zimetafsiriwa kuwa ni, “mkusanyiko wa hiari wa watu au shirika ambalo ni huru, usio na ushabiki wa kisiasa, usiolenga kutengeneza faida, ambao unaandalowi katika sehemu husika vijijini, kitaifa au kimataifa kwa madhumuni ya kukuza na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi, mazingira, kijamii au kitamaduni”.

Mheshimiwa Spika, watalamu wengine wamezitafsiri kama jumuia za wananchi ambazo hufanya kazi zake tofauti ya zile za kiserikali kwa madhumuni ya kutoa misaada mbalimbali ya kijamii au kisiasa. Katika Ripoti ya Hali ya Asasi za Kiraia Tanzania ya Mwaka 2009 ilioandalowi na “*The Foundation for Civil Society*” imeripoti kuwa asilimia 62.2 ya shughuli za asasi hizi zinafanyika kote vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee uendeshaji wa asasi zisizo za kiserikali, mahusiano na dola na nafasi ya asasi hizi katika kushirikiana na Serikali kuleta maendeleo na ujenzi wa demokrasia. Katika sehemu kubwa ya Afrika Mashariki, kama ilivyokuwa katika sehemu kubwa ya Afrika, suala la kujumuika nje ya dola na vyombo au asasi zake ilikuwa ni ngumu kwa sababu ya aina ya tawala zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Serikali ilisajili mashirika yasiyo ya Kiserikali yapatayo 554 na kati ya hayo 526 yalipatiwa cheti cha usajili na 28 yalipatiwa cheti cha ukubalifu. Aidha kwa mwaka huohuo, Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGO's* waliweza kutembelea mashirika 25 tu katika Mikoa ya Iringa na Tanga. Pamoja na Msajili kusajili kiasi kikubwa hivyo cha mashirika haya yasiyokuwa ya Kiserikali, swali la kujiuliza ni kuwa je, ni mangapi kati ya hayo ambayo yanaendesha shughuli zake maeneo ya vijijini ambapo wananchi wengi wamekuwa hawajui haki zao na wamekosa mahali pa kupata msaada wa kina juu ya ni hatua gani wanaweza kuchukua pale wanapoona kuwa haki zao zinakiukwa kwa njia mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, asasi za leo ndani ya mfumo wa soko huria zina sura tofauti. Nyingi zinaanzishwa na wateule (*Elite*), kitabaka hawana tofauti na wale walioshikilia dola. Ziko mijini na hazina sura za kitaifa kama ilivyo kwa vyama vya wafanyakazi na wakulima. Malengo yake ni ya ama kurekebisha mambo au mahusiano baina ya makundi ya watu sio ya kitabaka au kuwahurumia na kuwasaidia watu wenye shida kama vile watu wenye ulemavu, watoto yatima, wazee, vijana na wanawake hasa wajane wajikwamue na umaskini. Asasi zingine zinaelimisha wananchi habari juu ya demokrasia na jinsi Mfumo wa Vyama Vingi unavyofanya kazi na jinsi wananchi wanavyowenza kushiriki katika mfumo huo. Asasi nyingine zinajihusisha na masuala ya haki za binadamu, haki za watoto. Katika sura hii za asasi hizi twapaswa kujiuliza nini yatakuwa mahusiano yake na dola?

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya viongozi wanaodhani kuwa kazi ya asasi zisizo za Kiserikali ni kutoa upinzani kwa dola katika kuikosoa, kuiamsha, kuielimisha na kuiwijibisha dola tu. Kutokana na dhana hii, mahusiano ya dola yatakuwa ni yale ya kupingana na kukinzana na sio kusaidiana katika kuleta maendeleo. Kambi ya Upinzani inashauri Watendaji wa Serikali na watu wanaojihusisha na utendaji wa asasi hizi wote kwa pamoja kuondokana na dhana hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na mgongano wa asasi hizi na dola, Kambi ya Upinzani inashauri asasi hizi zikite zaidi katika kutekeleza majukumu yake mahsusini yafuatayo:-

- Kuwashauri na kuwaelimisha wananchi kuhusu sera na sheria mbalimbali kwa kutilia maanani kuwa wananchi walio wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu sera na sheria hizo, utekelezaji wake na kufanya tathmini katika ngazi zote pale walipo na hata kitaifa.
- Kufuatilia huduma na bajeti: Asasi za Kiraia zinaboresha huduma zinazotolewa na Serikali kwa kufuatilia, kudai uwazi na uwajibikaji na kwa kuhakikisha upatikanaji jumuishi wa huduma hizo na usawa wa kijinsia.
- Kukuza ufahamu wa wananchi kuhusu wajibu wao katika kujiletea maendeleo yao wenyewe.
- Asasi za Kiraia zinafanya kazi kama mlinzi wa kuangalia kile kinachofanywa na Serikali na wananchi. Madhumuni ya ulinzi huu ni kuhakikisha kuwa Serikali na watu wake wanatimiza ahadi na wajibu wao ili kupunguza umasikini na kuongeza uwazi na uwajibikaji.
- Kutoa msaada wa bure wa kibinadamu na kisheria kwa kuwapatia huduma maskini na kwa kutengeneza mbinu bunifu za kupunguza umasikini. Pia zina wajibu muhimu katika kutatta migogoro ya kibinadamu na kisheria. Hii inajidhihirisha wazi katika vikundi/mashirika mengi ya kidini yanayojenga mashule, hospitali na kuchimba visima vya maji na kadhalika.
- Kushawishi mabadiliko chanya kwani asasi hizi zinatakiwa kuwa daraja kati ya mamlaka za Serikali na jamii.

Mheshimiwa Spika, matukio kadhaa yanaonyesha kuwa mahusiano baina ya asasi za kiraia na dola si mazuri. Mfano nzuri ni tukio lililotokea Julai 2009 ambapo mamlaka ya Wilaya ya Ngorongoro iliwakamata wawakilishi wa asasi zisizo za kiserikali kwa madai kuwa walichochea wanawake wa Loliondo kuandamana na kurudisha kadi za CCM kwa kupinga kuchomewa makazi yao na mwekezaji. (*Tazama taarifa ya Tanzania Tanzania Human Right Report by State Department*). Tatizo hili bado lipo kwani hali iliyopo kwa sasa kwa asasi yoyote ambayo itafanya kazi ya kuelimisha wananchi kuhusu na haki zao.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili bado lipo kwani hali iliyopo ni kwamba asasi yoyote ambayo itafanya kazi ya kuwaelimisha wananchi kuhusiana na haki zao za msingi huchukuliwa kuwa ni adui na Serikali. Sambamba na hilo ni malalamiko ya asasi za kiraia dhidi ya asasi ya kiraia inayomilikiwa na Mke wa Rais (WAMA) namna ambavyo ilitumika wakati wa uchaguzi kufanya kampeni za CCM wakati asasi zingine za kiraia zilikatazwa kujihusisha na Vyama vya Siaya. Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa ni kasoro inayoleta mahusiano mabaya kati ya Serikali na asasi za kiraia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Ripoti ya Asasi za Kiraia Tanzania ya Mwaka 2009 ilioandaliwa na “*The Foundation for Civil Society*” imeripoti kuwa asilimia 36 ya watu waliohojiwa wangependa asasi hizi zisizokuwa za kiserikali zishirikiane na Serikali kusaidia wasiojiweza, asilimia 33 kutengeneza ajira, asilimia 25 kupunguza umaskini, asilimia 22 utetezi wa jamii pale haki za binadamu zinapokiukwa, asilimia 20 kuboresha mahusiano na kuondoa mifarakano, asilimia 15 kuanzisha miradi ya manufaa kwa jamii na asilimia 13 kupeleka ufahamu na ujuzi kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, tuziombe taasisi za kiraia na za Serikali kwa pamoja zijiulize zimesaidia vipi kusaidia makundi yasiyojiweza ya wazee, walemaavu, watoto yatima, wajane na makundi mengine ya jamii? Hapa ndipo tunapoona umuhimu wa Serikali kuanza sasa kuwalipa pensheni wazee wetu. Aidha, Serikali itoe ruzuku kwa vituo vya kulelea watoto yatima vinavyoendeshwa na asasi zisizo za kiserikali na sio utaratibu ule wa kusubiri mpaka wakati wa sikukuu ndipo vinunuliwe vitu kama vile mbuzi, mchele, sembe hivi vinatumika na vinaisha. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Ripoti imeeleza jamii inahitaji kupata utetezi, kuongezewa ufahamu na ujuzi. Tuna ukiukwaji mkubwa wa haki za raia kama mauaji ya raia wakiwa mikononi mwa Polisi, wananchi wengi kuwa na uelewa mdogo wa Katiba hata kushindwa kuchangia mchakato wa Katiba, Kambi ya Upinzani inashauri sasa asasi hizi zijikite katika kusaidia jamii na Serikali itoe ushirikiano kwa asasi hizi ikiwemo kushiriki mstari wa mbele katika mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, mahusiano mabaya kati ya dola na asasi za kiraia yanababishwa kwa kiasi kikubwa na pale inapotokea tukio ambalo asasi za kiraia inasema kuwa matendo yanayofanywa na Polisi au Jeshi au Taasisi nyingine za Serikali kuwa ni uvunjifu wa haki za msingi za kiraia na Serikali inaunda Tume Maalum ya kuchunguza kwa fedha za walipa kodi, mwishowe taarifa haziwekwi hadharani kwa wananchi kuelewa ukweli. Kama vile taarifa ya uchomaji wa nyumba huko Loliondo, Maji ya sumu yanayoingia katika Mto Tigitambao ni chanzo cha maji kwa matumizi ya wananchi nyumbani katika eneo la Nyamongo, taarifa ya uhamishaji wa wafugaji katika bonde la Ihefu, taarifa ya ujenzi holela wa maghorofa katika jiji la Dar es Salaam na kadhalika. Kambi ya Upinzani inasema jambo hili linazidisha mvutano kati ya asasi za kiraia na Serikali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mahusiano mazuri baina ya Serikali na asasi za kiraia ni jambo la msingi kwa maendeleo ya nchi yetu, Kambi ya Upinzani inasema hivyo kutokana na ukweli kwamba asasi hizi zisizo za kiserikali kama zitakuwa na mahusiano mazuri na wadau wote ikiwemo Serikali ndizo zitakazofanya kazi ya kufuatilia na kusimamia utendaji wa Serikali kwa kuwa ziko karibu sana na wananchi. Moja ya mambo yanayoifanya jamii kutotoa ushirikiano kwa asasi hizi zisizo za kiserikali ni pamoja na kutoridhika na utendaji wa baadhi ya asasi hizi na watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa ushauri ufuatao kwa asasi hizi:-

- Kuwepo uwazi katika bajeti na uwajibikaji wa asasi hizi, vyanzo vyatya mapato vijulikane, kiasi kinachopatikana, matumizi yake yawe wazi hasa kuwepo vitabu vyatya uhasibu.
- Kuwepo na ufanisi katika kutambua miradi, kuweka vipaumbele na utekelezaji hasa katika kuzingatia mahitaji ya jamii.
- Uwepo utaratibu shirikishi wa kupanga mipango ya utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.
- Uongozi wa asasi hizi usiundwe na watu wenye mahusiano ya kifamilia tu, ili kuondoa muonekano wa asasi hizi kuwa kama asasi ya familia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa mazingira yalivyo sasa nchini bado asasi zisizo za kiserikali hazina uhuru wa kutosha kufanya kazi zake kwa Sheria ya Asasi zisizo za Kiserikali Namba 24 ya mwaka 2002 inazipa mamlaka za Kiserikali nguvu kubwa ya kuingilia utendaji wa kazi mbalimbali za asasi hizo. Mathalani sheria hiyo inampa nguvu Msajili wa Asasi hizo kukataa kuisajili asasi pale ambapo anaona kazi zake hazina maslahi kwa umma, lakini maana ya neno maslahi ya uma hajaelezewa kinaga ubaga jambo ambalo linaweza kutafsiriwa kuwa ni maslahi ya kisiasa zaidi kuliko uhalisia. Wakati sheria hiyo hiyo imetoe mamlaka ya kufuta asasi yejote ile.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali, kuweka mazingira huru kwa asasi hizi kufanya kazi zake za kutoa huduma mbalimbali za kijamii, elimu, uraia na demokrasia kwa wananchi. Serikali iepuke vitendo vyatya kuingilia shughuli za asasi za kiraia na Serikali itoe ruzuku kwa asasi ambazo zinatoa elimu, afya na kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika hali nyingine isiyo ya kawaida yapo madai mengi yaliyori potiwa ya Wakuu wa Mikoa/Wilaya kuzuia kazi mbalimbali za asasi hata pale ambapo asasi hizo haziwajibiki kwao. Ripoti ya haki za binadamu Tanzania ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2010 iliripoti kuwa mtandao wa asasi zisizo za kiserikali za mijini Songea ulipokea amri kutoka kwa Mkuu wa Wilaya Bw. Thomas Ole Sabaya kuwa mikutano yao yote na wananchi inasitishwa na itafanyika tu kama kuna kibali cha ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani tunapenda kutoa rai kwa Serikali kuweka mazingira huru kwa asasi hizi kufanya kazi zake kwa pamoa na kutoa huduma mbalimbali za kijamii hutoa pia elimu ya uraia na demokrasia kwa wananchi na hivyo zinasaidia kujenga Taifa lenye watu makini na endelevu. Aidha, Kambi ya Upinzani hairidhishwi na mazingira ya sasa ya utegemezi wa asasi hizo kujiendesha kwa misaada toka nje, hivyo tunaitaka Serikali ileze ni mikakati gani inafanywa na Serikali kuziwezesha asasi kupata rasilimali za ndani ili kuepusha utegemezi.

Mheshimiwa Spika, mahusiano na madhehebu ya dini. Naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru vingozi mbalimbali wa madhehebu ya dini kwa kuendelea kuhubiri amani na upendo mionganoni mwa Watanzania. Kwani sote

tunatambua kuwa amani na utulivu katika nchi yetu ni jambo muhimu sana katika kufanikisha maendeleo ya nchi yetu. Sote tunashuhudia nchi zisizo na amani na utulivu huporomoka katika maendeleo ya kiuchumi. Makundi maalum ya watoto, walemavu, wazee, wanawake ndiyo wanaoathirika zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda pia kuwapongeza viongozi wa dini mbalimbali kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni kuamua kutimiza wajibu wao kikamilifu wa kuhubiri uwajibikaji wa watawala kwa watawaliwa. Hii inatokana na ukweli kuwa viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikristo waliamua kuunda umoja wao na kutembelea maeneo mbalimbali yenye migodi ya madini na kuona uhalisia wa jinsi ambavyo wananchi wanaoishi maeneo hayo wamekuwa wakiishi kwa tabu pamoja na kuwa wapo katika maeneo ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunawataka viongozi wa dini wasiishie tu kwenye maeneo yenye migodi ya madini na dhahabu ila waende na maeneo mengine ambayo yana migogoro mbalimbali kama ile ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima. Maeneo yenye mbuga za wanyama, migogoro kwenye maeneo ya viwanda mbalimbali na maeneo ya maliasili na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa dini ni watu ambao jamii ya Watanzania walio wengi imekuwa ikiwaamini na wana uwezo mkubwa wa kuvuta usikivu kwa waumini wao na wananchi kwa ujumla. Napenda kuwaomba viongozi wa dini kuendelea kutukumbusha sisi viongozi wa kisiasa umuhimu wa amani na tena pale inapotokea kuwakemea, kuwaonya, kuwakaripia wale wote wanaohubiri siasa zenye mwelekeo wa kutugawa Watanzania katika misingi ya udini, ukabila na itikadi za kisiasa, ili kuepusha Taifa letu katika mifarakano isiyo ya lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kwetu kumeibuka matukio mengi yanayoenda kinyume na maadili mema ya Kitanzania kama vile vitendo vya rushwa, mauaji yanayosababishwa na watu kujichukulia sheria mkononi na katika siku za karibuni yametokea mauaji mikononi mwa Jeshi la Polisi ambalo ndio mlinzi wa amani. Kambi ya Upinzani inawaomba viongozi wa madhehebu ya dini kuhubiri upendo mionganoni mwetu, mshikamano, utamanduni wa kuvumiliana na maadili mema na uwajibikaji kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, licha ya taasisi za dini kutujenga kiroho, zimekuwa zikisaidia serikali katika kutoa huduma kwa jamii, kama vile huduma za afya, maji na taasisi za kutoa elimu kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu. Kambi ya Upinzani inaziomba taasisi hizi zisaidie Serikali kukabiliana na ongezeko la vijana wanaofeli mitihani Kidato cha Nne na kuwasaidia kujenga vyuo vya ufundi na vituo vya ujasiriamali hasa maeneo ya vijijini ambako ndiko waliko vijana wengi waliofeli Kidato cha Nne hasa katika Sekondari za Kata. Kambi ya Upinzani, tunaishauri Serikali iweze kuanzisha utaratibu maalum wa kuzipatia ruzuku taasisi za dini ambazo zitajikita katika kujenga vyuo vya ufundi maeneo mbalimbali nchini na Wizara ihusike moja kwa moja katika kuratibu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wajibu wa kushirikiana na madhehebu ya dini katika kila hali kutokana na mchango wao mkubwa katika kuharakisha huduma za msingi kwa raia wake. Sambamba na hilo ni ushirikishwaji wa taasisi hizi katika kupendekeza mwelekeo bora wa matumizi ya rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, taasisi za dini zimekuwa na mchango mkubwa sana katika kuendeleza nyanja za ufundi hapa nchini na haswa kutokana na kujenga vyuo mbalimbali vya ufundi kwa ajili ya vijana kuweza kujiendeleza na haswa wale ambao wanakosa fursa za kuendelea na Elimu ya Juu. Kambi ya Upinzani, inapenda kufahamu je, kuna mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha kuwa taasisi za dini zinawezeshwa na haswa kipindi hiki ambacho vijana wengi walifeli Kidato cha Nne kwa matokeo ya mwaka jana ili kuweza kujenga vyuo vingi zaidi vya ufundi na kuweza kuwapatia fursa vijana hawa ili waweze kujiendeleza kwenye nyanja hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu wa Kambi ya Upinzani unatokana na ukweli kuwa taasisi na au mashirika ya dini Tanzania yanamilikia au kuendesha asilimia 40% ya hospitali na wastani wa asilimia 26% ya miundombinu ya huduma za afya na kutoa huduma za afya kwa asilimia 50% maeneo ya vijiji hapa nchini mwetu. Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Ulimwenguni ya mwaka 2006 ilionyesha kuwa mashirika ya kidini yalishiriki kwa kiasi kikubwa sana katika kuzuia kuenea kwa magonjwa mbalimbali Barani Afrika, zaidi ya asilimia 70 ya huduma za afya hutolewa na mashirika ya kidini. Hivyo ni rai yetu kwamba tukijielekeza katika mashirika ya kidini katika kujenga vyuo vya ufundi hakika inawezekana kuweza kuwapatia vijana wetu waliokosa nafasi za kuendelea na vyuo vya elimu ya juu kujiendeleza kwenye sekta ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu wamejitokeza baadhi ya watu na wengine viongozi kwenye maeneo mbalimbali ambao wamekuwa na tabia ya kuanza kupandikiza mbegu za udini na mifarakano ya kidini miongoni mwa Watanzania ambao wamekuwa na utamaduni ya kuishi kama ndugu huku kila mmoja akiheshimu dini ya mwenzake na wakishirikiana katika mambo mbalimbali ya kijamii katika Taifa letu. Kambi ya Upinzani tunachukua fursa hii kulaani na kukemea wale wote ambao wamekuwa wakianzisha chokochoko hizi na tunaitaka Serikali iwachukulie hatua za kisheria wale wote ambao wanapandikiza chokochoko za kidini miongoni mwa Watanzania kwani tusipochukua hatua tutaligawa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mahusiano na siasa. Kama ambavyo jina la Wizara hii inavyoonekana na majukumu yake kuwa ni pamoja na kuratibu mahusiano ya kisiasa hapa nchini, Kambi ya Upinzani tunapata tatizo kuweza kuainisha majukumu ya Wizara hii na haswa kwenye kuratibu masuala ya kisiasa kwani kwa mujibu wa *Instrument* ya tarehe 17 Disemba 2010, Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la kusimamia Vyama vya Siasa kuitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Utata nilioueleza hapo juu ni kuhusiana na ni nani haswa anasimamia masuala ya Vyama vya Siasa kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Wizara hii ya Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa baada ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Namba 7 ya mwaka 2009 sasa limeanzishwa Baraza la Vyama vya Siasa mnamo mwezi Mei 2010 ambalo linatajwa kuwa kiungo kati ya Vyama vya Siasa na Serikali na kati ya majukumu ya Baraza hili ni kutatua migogoro mbalimbali ya kisiasa ambayo inaweza kujitokeza baina ya Vyama na hata Vyama na Serikali. Kambi ya Upinzani inajiliza, je, Baraza hili linawajibika kwa nani kwa msingi kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndio inasimamia majukumu ya Vyama vya Siasa na wakati huohuo Ofisi ya Rais ina Wizara ambayo mionganoni mwa majukumu yake ni kuratibu mahusiano na Vyama vya Siasa. Suala hili ni muhimu likawekwa wazi kwani linaweza kusababisha mgongano katika utendaji kazi baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ile ya Rais na haswa katika kuratibu Vyama vya Siasa. Aidha Kambi ya Upinzani inatambua kwamba Baraza hilo ni chombo kilicho chini ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa ajili ya kumshauri. Hivyo mabadiliko ya kisheria na kanuni yanahitajika kuunda chombo cha kuunganisha Vyama vya Siasa chenyeh malengo ya ushirikiano wa Vyama.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Wizara hii ilihuksika moja kwa moja wakati wa mgogoro wa kisiasa uliokuwa umeibuka katika Jiji la Arusha hususani baada ya uchaguzi wa Meya ambaa ulikuwa umekiuka misingi ya kisheria na kanuni zote za kidemokrasia. Umma ultangaziwa kuwa Waziri alienda Arusha kulishughulikia suala hili. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu, je, katika mgogoro ule Waziri alihuksisha Vyama vya Siasa? Je, ripoti yake itawasilishwa Bungeni ili umma uweze kufahamu ni nani alihuksika katika kusababisha mgogoro huo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango. Majukumu ya msingi ya Tume ya Mipango ni kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa na kubuni sera za uchumi na mikakati ya mipango ya maendeleo ya Taifa pamoja na usimamizi wa uchumi na utafiti. Haya ni majukumu makubwa sana na ambayo yanahitaji ushirikishwaji mkubwa wa wananchi katika ngazi zote, ikiwemo na taasisi za kiraia sambamba na kuwa na rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa lingekuwa ni jambo la busara mipango yetu ya kuinua uchumi na kupangia matumizi rasilimali zetu tulizonazo ingelianzia ngazi ya chini ya utawala badala ya kuanzia ngazi ya juu. Kama ambavyo tulieleza katika hotuba zetu za Bajeti kuu na Kiongozi wa Upinzani – Waziri Mkuu kuwa Halimashauri zinatakiwa zipewe uwezo wa kuweza kupanga kulingana na fursa walizonazo ili kutengeneza ajira kwa kiwango kitakachopangwa kila mwaka na kuwezesha maendeleo kuanzia ngazi ya chini. Ili kutimiza azma hiyo ni lazima mipango ianzie katika ngazi ya chini kabisa, kwani huko ndiko rasilimali za nchi hii ziliko na sio katika ngazi ya juu. Ushauri huu ni katika kuoanisha dhana au sera nzima ya ugatuaji wa madaraka ambayo kwa miaka kumi na mitano Serikali imekuwa ikihimiza ili iwezekane.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasema kitendo cha kurudisha majukumu makubwa na ya msingi katika ngazi ya juu ni kinyume kabisa na uanzishwaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka. Hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali isigatue tu majukumu bali igatue pia na upangaji wa rasilimali zetu. Mathalani ni aibu kwa Mikoa ya Pwani kukosa Kiwanda cha Samaki au Halmashauri zinazozunguka mwambao wa

Bahari ya Hindi kukosa mipango endelevu ya jinsi ya kutumia rasilimali hiyo kwa maendeleo ya wananchi wake. Hii ni kasumba mbaya kwani kila kitu cha kuiendeleza jamii ni lazima wapange Watendaji walioko juu, Serikali Kuu. Halmashauri haziwezi kuingia ubia na wawekezaji mpaka ruhusa itoke Kituo cha Uwekezaji. Hii ni kuwafanya Watendaji wetu kuwa hawawezi kufikiri na kupanga kulingana na fursa zinazowazunguka katika kuwaletaa wananchi wao maendeleo. Hali hii pia iko kwenye maeneo yenye rasilimali na maliasili nyingine kama misitu, madini, gesi asilia, ardhi yenye rutuba na kadhalika. Ni lazima tukubali kuwa kwa sasa wananchi wako mbele ya Serikali kwa mambo mengi na ndiyo sababu kubwa kila jambo ambalo linapangwa na Serikali linashindwa kutekelezeka, lakini kama wananchi wakishirikishwa katika kupanga ni dhahiri tutakwenda mbele na mipango itakuwa na maana zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kutokana na kazi mahsus za Tume kuwa ni kupima hali ya rasilimali za Taifa na kuishauri Serikali juu ya matumizi bora ya rasilimali na kuharakisha maendeleo, hii ni dhihaka hasa kwenye sekta ya madini ambapo kwa sasa watu wamekwishamilikishwa rasilimali hizo na wananchi wengi wameshakuwa majeruhi kwa kuhamishwa bila kulipwa fidia stahiki wengi wamebaki ni masikini. Sasa Serikali ilikuwa wapi? Je, watu ambao wamekwishamilikishwa, watarudisha au ndio tunaweka chandarua ya kuzuia mbu wakati kumekwisha pambazuka?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kutokana na majukumu ya msingi ambayo yapo kwenye Tume hii na yale ambayo tunaona ni muhimu ya ushirikishaji wa umma katika kuandaa sera za maendeleo kwa sekta mbalimbali, ili yatekelezeze na tija ioneckane kwa Watanzania, bajeti iliyopangwa ya shilingi bilioni 7.4 ni kama mzaha, haitoshi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupanga bajeti ya kutosha vinginevyo Tume hii itashindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi na haswa ikizingatiwa kuwa Tume hii ina wajibu wa kusimamia kikamilifu mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi yetu kwa mwaka 2010 ilishuka kwa asilimia 8.5 kulinganisha na dola ya Kimarekani. Ili kutekeleza mpango huu na kufikia lengo la kutumia shilingi trilioni 8.2 kwa mwaka wa kwanza, tutajikuta katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa mpango huu unafika kiasi cha fedha kinachotarajiwa kitakuwa sio shilingi trilioni 9.1 tena kama kilivypangwa sasa. Hii itavuruga kabisa utekelezaji wa mpango wa Maendeleo wa Taifa. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ielete kwa kina ina mikakati gani ya kukabiliana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya nchi ili kuhakikisha kuwa mpango huu unatekelezwa kikamilifu ndani ya miaka mitano kwa makadirio ya fedha yaliyowekwa sasa? Vinginevyo, mpango huu utakuwa hautekelezeki na tutajikuta tukilazimika kuufanyia duruso/mapitio (*review*) ili kuweza kukabiliana na kushuka kwa thamani ya shilingi. Vilevile, kiasi cha pesa kilichotengwa kwa utekelezaji wa mpango huu si kiasi halisi kinachoweza kutegemewa katika kuutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa, ikiwa anguko hili la thamani ya shilingi litaendelea kutokea bila kudhibitiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, usalama wa Taifa, hapa Tanzania tuna sheria mbili zainazohusu usalama, moja ni Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 (*National*

Security Act, 1970) naomba kunukuu maudhui ya sheria hiyo “An Act to make better provision relating to state security; to deal with espionage, sabotage and other activities prejudicial to the interests of the United Republic; and for purposes incidental thereto or connected therewith”. Sheria ya pili ni ile ilioanzisha Idara ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996 (*Tanzania Intelligence and Security Service Act, 1996*), naomba ninukuu maudhui yake “An Act to establish the Tanzania Intelligence and Security Service and make provision for other matters relating to it”. Hizi sheria zote bado zipo, japokuwa kuna upungufu wa hapa na pale kutokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii, yanayotokea nchini. Kwa kuwa lengo kuu la sheria hizo ni kulinda maslahi ya nchi yetu, si rahisi kuwa na mlolongo wa vyombo vyaya usalama kwa usalama wa nchi kwani kuna hatari kuna wakati tutafikisha nchi katika hali mbaya kwa kukosa chombo sahihi kinachotoa ushauri wa mwisho kuhusu maslahi na usalama wa nchi na mambo ya usalama yanahitaji maamuzi kufanya kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyaya usalama ni vya muhimu sana katika ulimwengu wa sasa hasa katika kutazama kwa makini masuala yote ya uwekezaji unaokuja kuwekezwa Tanzania, (wawekezaji kufanyiwa *background work before investing in our country*), Kambi ya Upinzani, tunaishauri Serikali kuwa baada ya kuzihisha sheria hizo mbili na kuwa na sheria moja, hivyo kiundwe chombo kimoja kwa ajili ya kusimamia maslahi na usalama wa Taifa letu na kijulikane kama Wakala wa Usalama wa Taifa (*National Intelligence Agency*) na chombo hiki kiratibu ukusanyaji, uchambuzi, ugawaji na ufuatiliaji wa taarifa mbalimbali zinazohusiana na maslahi pamoja na usalama wa Taifa letu. Hii inatokana na ukweli kuwa changamoto za kiusalama zimeongezeka sana na zinahitaji kila mara tuweze kujipanga upya ili kuweza kukabiliana nazo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kuwa sheria zilizounda usalama wa Taifa hazitoi fursa kwa chombo hiki kufanya “ujasusi wa kiuchumi” (*Economic Espionage*) kama vile kuweza kufanya tafiti na kuingiza nchini mbinu na teknolojia mbalimbali ambazo zinatumika kwenye nchi nyingine ulimwenguni, ambazo hutumia katika kukuza uchumi wao ili na sisi kama Taifa tuweze kuzitumia mbinu hizo na teknolojia hiyo katika kukuza uchumi wetu, Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa huu sasa ni wakati muafaka kwa ajili ya kuifanya marekebisho sheria iliyouna chombo hiki na kuhakikisha kuwa kinapewa mamlaka na jukumu la kufanya ujasusi wa kiuchumi (*economic espionage*) na kuweza kuingiza mbinu na teknolojia mbalimbali za kukuza uchumi wetu kutoka mataifa ya nje kama ambavyo nchi nyingine ulimwenguni hutumia vyombo kama hivi kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Nashukuru sana. Kwanza, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kutuwezesha tumalize hotuba hizi kusudi mchana tukiingia tuanze kujadili, vinginevyo ingekuwa ngumu sana. Nashukuru sana kwa hilo.

Kwa hiyo, mchana tukirudi watakaoanza kuzungumza ni wale ambao hawajaongea hata mara moja katika hotuba ya bajeti na ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama hawajajitokeza ambao hawajazungumza hata mara moja basi tutaingia na wale

waliochangia mara moja. Kwa hiyo, orodha niliyo nayo kwa sasa hivi kwa wale walioomba watakaoanza ni Mheshimiwa David Malole, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani.

Waheshimiwa Wabunge, kuna suala lingine pia, katika siku za *weekend* au siku zingine, Waheshimiwa Wabunge mnakuwa labda mmepewa safari, mimi mwenyewe nimewahi kumpeleka mmoja mahali, basi unakuta huna mahali pa usalama pa kuweka gari lako labda wengine bado mko kwenye *guest*, kwa hiyo, unaweza kuacha gari hapa, lakini ukiacha gari hapa, naomba upeleke taarifa kwa Idara yetu ya *Sergent at Arms*. Ofisi yao iko katika Ukumbi wa Msekwa pale, unaacha ufunguo na unatoa taarifa, gari yako itaandikwa vizuri kwamba umeacha gari hii na ufunguo uko hapa kwa sababu ukiacha tu hivihivi nayo si sahihi, hutajua nani kaacha, nani kafanya nini. Ndiyo maana juzi siku ya tafrija magari *yali-pack* eneo lile kushindania *twist*, wenyewe wakawa wameondoka, hayakuweza kuondoka, basi ikabidi iwe ilivyokuwa. Kwa hiyo, naomba hili tulizingatie kwa sababu huu uwanja unaangaliwa. Kama unaiacha gari yako sawa lakini nenda kwa *Sergent at Arms*, Ofisi iko jengo la Msekwa pale, wataandikisha gari yako na wewe mwenyewe na utaacha na ufunguo wako, hapo utakuwa na uhakika kwamba usalama upo.

Baada ya hapo, sina taarifa nyingine yoyote, napenda nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.25 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaziwa mchana na Mheshimiwa Spika, wachangiaji wa mwanzo watakuwa ni Mheshimiwa David Mallole, Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Dokta Titus Kamani, wajiandae. Tunaanza na Mheshimiwa Malole.

MHE. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mawazo yangu katika hotuba ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa upendo mkubwa walionipatia kwa kunichagua kwa kura nyingi sana za ndio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kutoa pole sana kwa wananchi hasa wa Tarafa ya Kikombo kwa kuondokewa na mlezi wa Tarafa hiyo, ndugu yetu mpendwa Peter Chiwanga. Nilikuwepo wakati wa msiba na ninaahidi kwamba hata siku ya kumaliza msiba nitakuwepo. Kama nilivyowaambia, naomba wasijisikie upweke

wala ukiwa mkubwa mimi nitakuwa pamoja nao na nitakuwa karibu sana na Tarafa ya Kikombo, ili tuweze kusaidiana vizuri katika matatizo mbalimbali yanakayowasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa kifupi na kwa kutumia maneno machache ya Kilatini kwamba “*Veni, Vidi, Vici*” kwamba nimefika hapa Bungeni, nimeona taratibu zinazoendelea na kwa hakika sasa nitatekeleza wajibu wangu vizuri na bila ya shaka mtaona matokeo ya kazi yangu kwa kipindi cha miaka mitano mliyonipatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana mke wangu, Mama Mallole na *staff* yote ya *X-Ray* na Hospitali Kuu ya Mkoa, kwa ukarimu mzuri amba walinitendea wakati wa kura zangu. Nawashukuru sana watoto wangu, Waafrika tuna watoto wengi sana katika upana wa mila na desturi zetu, tunakaa na watoto wa kaka, dada, shemeji, mjomba, nawashukuru wote lakini niwashukuru kwa namna ya pekee Deprima na Silvanus Mkanda pamoja na mjukuu wangu Lucy, ambaye ameshaanza kujifunza kuzungumza, mara nyingi akiniona kwenye TV anasema, “*Aona Babu Mallole*” na mimi nikisikia lugha hiyo, inanifariji na kuendelea kunipa nguvu sana. Niwashukuru Deserina na Doni Mkubulo pamoja na familia yao yote lakini pia wanangu George, Steve, John na Desteria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi mkubwa wa fadhila kama sitawenza kuyashukuru mashirika mbalimbali ya dini. Nayashukuru sana kwa mikesha mbalimbali walijonifanyia na kuniombea hadi nipite. Nazishukuru kwa namna ya pekee Taasisi mbalimbali za Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu vyote vilivyoko hapa Dodoma; nasema ahsanteni sana kwa msaada wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nitoe pongezi kwa Spika, Baraza la Mawaziri, Wabunge na Wenyeviti wote amba mmechaguliwa kuweza kuliongoza Bunge hili. Nasema hongereni sana, Mungu awabariki na kazi yenu izidi kuendelea kuwa nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee sasa na ya mwisho lakini ya muhimu zaidi, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kura nyingi sana za ndio alizozipata katika uchaguzi wake wa mwaka jana, mwaka 2010. Namshukuru mimi kwa namna ya pekee kwa namna mbili, kwanza kabisa tulikuwa wengi; kama mnavyojua mara nyingi fitna ziko nyingi mtu unapokuwa umepata kura nyingi sana za maoni. Aliniibua yeze na kunipitisha na kwamba mimi ndio niwe mgombea pekee na bado alisimamia yeze kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kuweza kuona kwamba napita. Pia naomba nimshukuru kwa namna ya pekee, maana hata baada ya kupita kulikuwa na matatizo mengi lakini tarehe 5/02/2011 wakati tunasherehekea sherehe za CCM hapa Mkoani Dodoma, ameweza kuwatangazia wananchi wazi kabisa kwamba yeze anatambua kwamba David Mallole, ndio Mbunge pekee wa Jimbo la Dodoma Mjini, kuitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi, namshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie kuhusu masuala ya utawala bora. Katika hili, napenda kupongeza sana tena sana juu ya mpango wa *Master Plan* Mpya ya Mji wa Dodoma na nakiri kabisa kwamba *Master Plan* iliyokuwepo hapo zamani, kwa kweli ilikuwa na upungufu mwingi sana ambao ulisababisha mtasfaruku mkubwa na kupelekeea Serikali kutolewana na wananchi. Nashukuru, hasa kwa uwezo wa pekee kabisa wa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ameweza kubaini upungufu wa *Master Plan* hiyo na kuagiza *Master Plan* Mpya itengenezewa, ambayo sasa itaelekeza Mji Mkuu Mpya wa Dodoma ujengwe maeneo yanayoanzia kule Chamwino na Vijiji vya jirani. Hali hii, nina uhakika kabisa kwamba itaondosha matatizo mengi ambayo yameleta usumbufu mkubwa sana, hasa kwa wakazi wa eneo la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Master Plan* iliyopita, ililenga kubomoa maeneo ambayo yalikuwa yamejengwa ili mji ujengwe. Hali hiyo imeondoa kabisa amani na utulivu katika eneo hili. Naomba sasa *Master Plan* Mpya itakayokuja iangaliwe kwa karibu sana kwamba watakapokuwa wameitengeneza, basi ilenge maeneo ambayo bado hayajajengwa. Dodoma ina ardhi kubwa sana, *we have got a lot of unused land here in Dodoma just as you have got a lot of unused land here in Tanzania*. Kwa hiyo, waangalie kwamba ni maeneo gani wanaweza wakaweka mji na si vema wakati wote mji ukawa unalenga maeneo ambayo tayari watu wamekaa. Si vema kubomoa kwanza halafu baadaye ukajenga. Maeneo ambayo yamejengwa yaboreshwe kwa utaratibu wa aina yake, lakini ramani mpya itakayokuja iweze kuangalia kwa karibu sana kuweza kuona kwamba wanaweka kwenye maeneo ambayo bado hayajaguswa na mtu yejote. Wakifanya hivyo, nina uhakika kabisa kwamba hata maeneo ambayo bado ni ardhi pana, tambarare, maeneo ya milima na maeneo ya mapori ambayo yamejaa hapa Dodoma, bado hata mji wa Dodoma wakisema waujenge kwa miaka 200, hiyo ardhi hawataimaliza. Sasa kama ardhi ni kubwa, uko umuhimu gani wa kujaribu kulenga wakati wote ni maeneo gani wananchi wamekaa ili waweze kubomoa ndio wajenge? Nina imani kwamba watazingatia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa upande wa Serikali, kwamba maadamu Mji Mkuu sasa unaelekea Chamwino na vitongoji vyake, basi utaratibu mzuri uweze kuwekwa watu hawa wakae karibu na maeneo ambako kunatakiwa sasa kuuendeleza Mji Mkuu. Tunaomba sasa watu wa *CDA* wahamishe Ofisi zao kutoka katikati ya mji, waende maeneo ya Chamwino. Wagogo wanasema, “*Mgunda alimika, winamu ya mgunda*” ukitaka shamba lako liweze kulimika vizuri, mwenye shamba uwe jirani vinginevyo watu watakata mtama, watakata mahindi na utashtukia hupati chochote. Wakae karibu, wasimamie *Master Plan* Mpya na wasimamie ujenzi mpya wakiwa karibu na maeneo ambako mji mpya sasa unaelekezwa, yaani upande wa Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba sisi wenyeji wa hapa huwa tunashukuru katika kila jambo. Tunawashukuru kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya, lakini tunashukuru hata kwa bahati mbaya juu ya makovu mbalimbali ambayo wametusababishia na hatuwalaumu sana. Hayo yalijitokeza kwa sababu ya *Master Plan* ya wenzetu Wazungu ambayo waliitengeneza ikiwa na malengo ya kuwagonganisha wananchi na Serikali yao. Bado nataka kusema kwamba sisi tutawaaga

na kuwasindikiza kwa nyimbo nzuri na nderemo na kwa kutumia vifaa vya kisasa tulivyonavyo sisi wenyeji wa asili, yaani ngoma za Muheme, Marimba, Mazeze pamoja na Ndulele, tukijua kwamba wameyafanya mengi kadri Mwenyezi Mungu alivyowajalia, lakini tutaendelea kuwaombea kwamba huko walikoenda wakaendelee kuujenga mji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, mwisho kabisa, ninaomba nimalizie pia kwa maneno haya mafupi ya Kilatini, “*In Omnibus Resipicethinemu*”, kwamba katika kila jambo ambalo mtu unafanya ni lazima mtu utahadhari sana. Dakika za mwishoni wanapokuwa hawa wanaagaaga kuelekea kwenye *Master Plan* Mpya iliyoko huko Chamwino, sasa kunawenza kutokea uharibifu ambaو haujapata kutokea kwa kipindi cha miaka 37 iliyopita. Tunaomba sasa, moja, wasimamishe bomoabomoa zote kwenye maeneo ambayo tayari walikuwa wameshayaweka maeneo ya Mkonze, Michese, Ipagala, Swaswa, Msalato na Nhungu, hasa maeneo ya Ntube, kule kwa John Masaka, maarufu kwa jina la Kisagara Ndeo, hata katika miji mingine kama Mji Mwema pamoja na Chinyoya.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni maajabu ndugu zangu kuona kwamba hata maeneo ambayo makaburi yanatakiwa yawekwe ni lazima kwanza mji eti uondoke pale ndipo makaburi yawekwe! Nadhani huko Marekani, walioweka *Master Plan* ya namna hii wanacheka na walikuwa wanasuburi sana kama kuna uwezekano kuona kwamba hata majengo yote ya Bunge hata labda Chuo Kikuu cha *UDOM*, kinafyekwa na kuondolewa ili makaburi yawekwe! Hivi ni vichekesho, bado tuna ardhi kubwa, bado watu wanafyeka mapori kuelekea maeneo ya Nala, kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na maeneo makubwa sana ya kuzikia watu kuliko kuendelea kufikiri kwamba wakati wote ni lazima kwanza tufyeke mji ndipo kitu fulani kisimame.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ndugu zangu *CDA* wana mambo mengi. Naomba sasa hivi masuala ya maji wakabidhi *DUWASA* kwa upande wa Dodoma Mjini na Halmashauri kwa upande wa vijijini. Umeme wakabidhi *TANESCO*, barabara wakabidhi *TANROADS*, ardhi wakabidhi Manispaa. Miaka ya nyuma...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITU: Ndio.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, naomba ninukuu Kanuni ya 64(1)(b) ambayo inasema:-

“Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifdhii uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani jambo ambalo liko kwenye mjadala ni hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mahusiano, Uratibu; Hotuba ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kadhalika. Sasa sikuwa nimejua kwamba makadirio ya Ofisi hizi mbili yanahusu *Master Plan* ya CDA! Huyu Mheshimiwa Mbunge, inaelekea anazungumza vitu ambavyo haviko kwenye mjadala. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, kwanza ninakupongeza kwa kuliona hilo lakini mimi mwanzo nilipitiwa na zile salamu zilikuwa nyingi sana. Salamu za watu wote, wajukuu, nini, nilipitiwa kwa kweli. Basi, tuseme tu kwamba Msemaji aliyekuwa akiongea amesikia na kwa bahati mbaya muda wake umeshakwisha. Kwa hiyo, tumuachie amalize kutoa shukrani. (*Makofî*)

MHE. DAVID M. MALOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuendelea kunilinda, lakini ninapozungumzia katika hili hata kidogo mimi sifikiri kama napotosha. Suala la CDA liko kwenye Sera, suala la CDA liko kwenye mahusiano, sasa ninachozungumzia ni mahusiano yaliyoharibika ambayo yamejitokeza kutokana na chombo hiki kuwepo hapa. Kama hiyo haina mahusiano na utawala bora au kama watu wanagongana na Serikali inaonekana sio utawala bora au sio kitu kinachohusiana na Sera na Utawala Bora, basi itabidi labda eneo hilo niliache, lakini mimi sikufikiri kwamba nimekosea kitu chochote kile. Nilikuwa ninajaribu kuimarissha masuala ya uhusiano na utawala bora, yaweze kuibuka hapo. Mara nyingi ni vizuri kuvielewa vitu *philosophically and not superficially*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kudumisha utawala bora na kwa kuzingatia kwamba kwa muda mrefu watu wa CDA wamekuwa hawawezi kudumisha mahusiano bora, basi nilikuwa ninafikiri kwamba hata ardhi ambayo wanayo, ili waweze kuleta mahusiano bora ni vema sasa wakawaachia watu wa Halmashauri ya Manispaa maana ndio wamiliki wa ardhi kisheria. Hawa walipewa tu kwa muda wakifikiriwa kwamba labda wanaweza wakajenga Mji Mkuu kwa kipindi ambacho hakitazidi miaka 37, lakini muda umeenda na sasa hivi Halmashauri ya Dodoma Mjini, imeshindwa hata kuitwa Jiji kwa sababu mapato yao hayatoshi, kwamba wangeweza wakakusanya pesa kutoka kwenye ardhi yao. Tayari Arusha ni Jiji, Mwanza ni Jiji, Mbeya ni Jiji, Iringa ni Jiji, kwa sababu wao hii ardhi ni ya kwao ni mali yao wamekusanya mapato yameshawenza kukamilika na yameshatamkwa kuwa majiji. Sisi mojawapo ya sababu inayotufanya tusiwe jiji, ni kwamba ardhi ipo chini ya CDA na Halmashauri yetu haipati mapato ya kutosha kwa sababu ardhi sio yao. Mimi nilikuwa nafikiri mambo haya yanaharibu sana mahusiano na kufanya sera tulizonazo zionekane kwamba ni ngumu, utawala bora uonekane kwamba haupo, kwa sababu kila wakati kuna ugomvi kati ya Serikali na wananchi. Naomba suala hili liangaliwe kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ya kuwashukuru wote wanaohusika, nafikiri ni wajibu wangu, ni sawasawa kumshukuru mke wangu kwa kazi nzuri ambayo aliifanya. Kuwashukuru watoto, hata huyo ambaye anayesema “*Aona Babu Malole*”, ni malaika

ambaye ananipenda na anaendelea kunipa nguvu. Kama wengine hamjapata hata mjukuu mmoja, angalau mie ninaye mmoja, msinionee wivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini ili kurekebisha utawala bora yote haya niliyozungumza naomba yazingatiwe na *CDA* wahamie sasa Chamwino na kuicha Dodoma kama Mji Mkongwe, tuendelee kama tutakavyoweza. Waende wakajenge maeneo ambako hakuna watu sio kubomoa nyumba za watu na kusema eti wanabomoa yawe makaburi. Hivi ni vichekesho kabisa ambavyo havipo na vinaharibu kabisa mahusiano kati ya Serikali na watu; wanafanya watu waione Serikali mbaya wakati kumbe Serikali ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, mjadala wetu unalenga Wizara tatu. Kwa hiyo, tuwasikilize kwa makini wanaochangia, inawezekana akafika mahali, mwanzo alianza vibaya, kweli shukrani zilikuwa nyingi na sisi tumesema hizi salamu za mjukuu na nani tunaziache ili *tu-focus* kwenye *key issues* lakini sasa tuna *limitation* ya *time*, yeye ame-opt kutumia muda wake kwa salamu, lakini mwisho amemaliza kwa kuzungumzia haya masuala ya uhusiano. Naomba tuwe makini kwenye Wizara hizi tatu, ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na ya Uhusiano na Uratibu. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Sara Msafiri.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafsi na mimi niweze kuchangia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, *exchange Mic* yako.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafsi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Ofisi ya Utawala Bora. Napenda nizipongeze Wizara zote hizi kwa kutoa hotuba nzuri ambayo inaonesha mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali, kipindi cha mwaka 2011/2012, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye Wizara ya Utumishi, hasa kwenye Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Nakipongeza hiki Kitengo kwa kazi zake ilizofanya hasa kwa kuhakikisha kwamba wamekusanya orodha ya wahitimu na wataalamu mbalimbali ambao wamemaliza masomo yao na kuwa na data kamili. Pamoja na pongezi hizi, napenda tu niongelee kwenye suala la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira iandae utaratibu mzuri wa kushughulikia mfumo mpya wa kuratibu ajira kwenye Utumishi wa Umma kwa sababu ajira nyingi sana za Utumishi wa Umma tumeona zinahitaji usoefu kuanzia miaka 10 na

kuendelea, zina-entertain mikataba kwa watumishi ambao wameshamaliza muda wao wa ajira, wamefikia umri wa kustaaafu, lakini wanaongezewa mikataba pasipo sababu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu moja, wapo watumishi ambao wamesomea fani ambazo ni nyingi, wapo wataalamu wengi tu kwa mfano, *Human Resource, Sociology* na fani nyingi ambazo wahitimu wako wengi na Sekretarieti imekiri kwamba kuna mlundikano wa watu wanahitaji ajira, lakini Serikali inaendelea kuwapa mikataba ya ajira. Nashauri kwamba ifike hatua sasa tuwe *serious* kwamba tunataka kutatua tatizo la ajira hasa kwa vijana kwa kuhakikisha kwamba watumishi wanaofikia umri wao wa kustaaafu, wastaafu, ili vijana waliokuwa nje nao wapate kuajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kijana ana malengo yake mwengine ameshalenga kutumikia utumishi wa umma, sasa tukitumia uzoefu wa miaka tisa na kwenda juu, kuongeza mikataba kwa watumishi waliomaliza muda wao, hawa vijana wataajiriwa lini? Kwa hiyo, naomba sasa Mheshimiwa Waziri anapojobu hoja ahakikishe kwamba anatuambia kuna fursa gani kwenye ajira za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yanasemwa kuhusu vijana, kwamba vijana hatuna uwezo lakini mimi nasema mtu amejiriwa toka akiwa na miaka ya 23, amefanya kazi mpaka anafikisha miaka 60, hivi leo Serikali inataka kutuambia nini vijana wa Tanzania kwamba huyu kijana ametumikia sekta ya umma kwa miaka 40, lakini ameendelea kupewa mikataba ataleta mabadiliko gani kwenye taasisi anayoiogoza? Tunayo mifano hai, mashirika ya simu, taasisi za fedha, mashirika ya dini, wapo vijana ni ma-CO, wanafanya kazi zao vizuri, lakini Serikali imeendelea na urasimu wa kuhakikisha vijana hawapati fursa kwenye sekta ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kwenye Sheria ya Gharama za Uchaguzi hasa TAKUKURU ilivyosaidia kuhakikisha mapambano dhidi ya rushwa yanatekelezwa na kuhakikisha rushwa inapungua na kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Nasema hivyo kwa sababu moja, sheria hii imeleta mabadiliko makubwa katika mfumo mzima wa uchaguzi uliopita, mabadiliko ya kwanza sisi ni mashahidi, Madiwani wengi huko kwenye ngazi ya Kata ni vijana, hawa vijana hawana rasilimali fedha, hawana rasilimali watu lakini wameshiriki uchaguzi na wameshinda, leo vijana ni Madiwani na wengine ni Wenyeviti wa Halmashauri. Mfano mzuri ni kwenye Mkoa wangu wa Morogoro, tuna wilaya sita, Wilaya tatu ya Kilombero, Kilosa na Mvomero wanaongoza Wenyeviti wa Halmashauri wenye umri chini ya miaka 35, haya ni mafanikio yaliyoletwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi na mapambano dhidi ya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwengine Bungeni hapa, sasa hivi tuna Wabunge vijana 140 na Bunge lako lina Wabunge 350, ni sawasawa na asilimia 40 ya Wabunge wote, haya ni matokeo ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, vijana hatuna rasilimali lakini kuitia sheria hii, kuitia usimamizi mzuri wa TAKUKURU, vijana tumeweza kufika Bungeni na vijana tutaendelea kutetea Sheria hii ya Gharama za

Uchaguzi, tutaitetea TAKUKURU kuhakikisha maboresho yanafanyika ili iweze kutumika vizuri mwaka 2015 na tuweke mabadiliko katika jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee ofisi ya TAKUKURU kwa ujumla, TAKUKURU hii tunesomewa hapa asubuhi kilianza kitengo, *Task Force* tangu mwaka 1975 baada ya uhuru lakini iliyokuwa sasa hivi mwenye macho haambiwi ona, TAKUKURU imejiimarisha kwenye elimu kwa umma, hakuna mtu ambaye hajui mapambano dhidi ya rushwa, hakuna mtu ambaye hajui madhara ya rushwa, TAKUKURU imejenga ofisi kila Wilaya. Kujenga ofisi huku siyo kwamba wanajipendekeza waonekane wanafanya kazi nzuri kwenye macho ya Wabunge na Wanasiasia, ni ili kuhakikisha mkulima kule kijiji, mwananchi kule Ulanga, kule Kilombero, kule Mvomero anaweza kulinda na kutetea haki zake na kuhakikisha huduma zinazotolewa na Serikali ambazo ni haki ya kila mwananchi kupata anazipata. Kwa hiyo, mimi napenda kukipongeza kitengo hiki cha TAKUKURU. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda ukurasa wa 84 kwenye hotuba aliowasilisha, kitabu cha Mheshimiwa Hawa Ghasia, utaona kazi za TAKUKURU, kwenye kipengele cha 8, tunaambiwa kwamba TAKUKURU kwa sasa ina jumla ya kesi 466, kesi hizi ziko Mahakamani na tunajua Mahakama ndiyo chombo kinachotoa haki ulimwenguni, Watanzania tunaamini kwamba hizi kesi zimeshafika sehemu yake, rasilimali zilizoibwa na wachache zitarudi mikononi kwa wananchi. Kwa hiyo, mimi nimesukumwa kabisa kwenye nafsi ya moyo wangu kusimama kuipongeza TAKUKURU. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye aya ya 10, tunaona kiasi cha fedha kilichorejeshwa, fedha zilizoibwa, mabilioni ya hela, zaidi ya bilioni 13 TAKUKURU wamepambana kuhakikisha rasilimali zinarudi mikononi mwa wananchi. Hii ni kazi kubwa lazima Watanzania tuipongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kesi hizo 466, tuna kesi za *grand corruption* kesi 24 ziko Mahakamani, kesi hizi ndiyo kulikuwa na malalamiko mengi ya wananchi, maana hizi ni rushwa kubwa, rushwa ya mikataba, rushwa ya viongozi wakubwa tulio wapa dhamana leo zipo Mahakamani. Mimi nasema tuwaombee TAKUKURU wapewe afya njema, waweze kusimamia haki na misingi ya watendaji wao wa kazi ili hatimaye hizi mali zirudi mikononi mwa wananchi, kwa mkulima wa chini ambaye ni mlipa kodi. Kwa hiyo, mimi nimesukumwa kabisa kwenye nafsi yangu kuwapongeza TAKUKURU. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwenye ukurusa wa 83, kipengele cha tano, tunaona majalada yaliyopelekwa kwa DPP kuanzia mwaka 2005, 2006, 2007 mpaka 2010 mpaka Mei, 2011. Majalada haya mwaka 2005 yalikuwa 20 lakini mpaka sasa majalada yaliyokuwa kwa DPP, yameshazidi 200 hapa kuna walakini tukubali, zipo nchi za Jumuiya za Madola, tumeona kwamba TAKURURU au taasisi zao za rushwa zimepewa mamlaka ya ku-*prosecute* kesi, tuwape mamlaka hayo TAKUKURU, tunaogopa nini? Ghana wamefanya, Uganda wamefanya, Sierra Leon wamefanya na Kenya kwenye Katiba yao Mpya wameingiza kwamba Taasisi zao za Kupambana na

Rushwa zimepewa wajibu, mamlaka ya kuchunguza na kusimamia kesi zao Mahakamani na sisi hatuishi kama kisiwa lazima tufanya maamuzi ya busara hapa ili kuhakikisha rasilimali za watu zinarudi kwa wananchi wenyewe na siyo kufaidisha wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hiyo, napenda tena niongelee TAKUKURU ilivyotusaidia Tanzania kujenga heshima yetu katika nyanda za kimataifa. Tunajua kwamba jambo lolote linapotokea haliji tu *by chance* linakuja kutokana na historia ya mtu, linakuja kutokana na historia ya taasisi. Leo hii Watanzania tuko hapa, Mkurugenzi wa TAKUKURU ni Rais wa *SADC* kwenye *Anti Corruption Authorities*, kipindi cha nyuma alikuwa Rais wa *East African Anti Corruption Authorities*, bado ni *board member* wa AU, bado ni *board member* wa dunia, haya ni mafanikio, haya mambo hayaji hivihivi. Watanzania tumezoea mpaka tusifiwe na watu wa nchi za nje ndiyo tunakuja na sisi kusifia, tujivunie hizi ndiyo sifa za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda pia nitoe ushauri mchache kuhusu TAKUKURU na Serikali kwa ujumla. Kwanza nashauri Serikali sasa ifike wakati kazi ya *ku-prosecute* iwe kwenye mamlaka ya TAKUKURU ili haki zipatikane kwa urahisi.

Mbili, Serikali iandae mpango maalum sasa wa kutathimini Sheria ya Gharama za Uchaguzi, ishirikishe wadau mbalimbali wa Vyama vya Siasa, ishirikishe sekta binafsi, ishirikishe *NGOs*, tuiboreshe, ili mwaka 2015 tunapoelekea nchi yetu kuwa na Katiba Mpya, tuhakikishe sheria haina upungufu mdogomdogo uliojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nianze kwa kumshukuru Mungu kwa sababu ndiye aliyetuwezesha wote kuwepo hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki moja iliyopita niliokoka kwenye ajali ambayo ingeweza kuwa mbaya, kwa hiyo nina kila sababu za kumshukuru Mungu na kuwashukuru wote walionitakia heri wakati nilivyokuwa narejesha afya na mawazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa sababu ndiyo mara ya kwanza nachangia kwenye bajeti ya nchi hii katika Bunge hili, niwashukuru wapigakura wa Jimbo la Busega, kwa imani kubwa waliyonipatia kuweza kuingia hapa kuwakilisha. Napenda kuwaahidi kwamba kama mwakilishi wa Chama cha Mapinduzi, nitashirikiana vyema na wenzangu wote hata wa Upinzani kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele kwa bajeti iliyopitishwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za karibuni, jina langu limekuwa maarufu sana kwenye vyombo vya habari, nilitaka nitumie nafasi hii kusema waliokuwa wanasikia Dkt. Kamani ndiyo huyu. Nafahamu kuna Waandishi wa Habari walikuwa wanaandika tu Kamani, hawamfahamu, lakini ni kwa sababu ya siasa za watu ambao hawataki kukubali matokeo ya demokrasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatoa hofu kabisa wananchi wa Jimbo la Busega kwamba Mbunge wao yuko imara na ataendelea kuwawakilisha kwa umakini mkubwa kuhakikisha kwamba keki ile ndogo ya Taifa na wao wanaipata kwa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze vilevile kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kitu kimoja, karibuni alikutana na uongozi wa Vyama vya Wafanyakazi TUCTA, mwaka juzi kulikuwa na mvutano mkubwa kati ya Serikali na Vyama vya Wafanyakazi kuhusiana na madai mbalimbali ya wafanyakazi, kitu ambacho kilipelekea Rais kwa mara ya kwanza au kwa mara chache akaacha kualikwa kwenye shughuli muhimu za Vyama vya Wafanyakazi na wafanyakazi wa nchi hii. Napenda kumpongeza kwamba alitambua umuhimu ule na akaweza kukutana na kuondoa tofauti zile za msingi zilizokuwa zinasumbua na kukera wafanyakazi wa nchi hii na kwa kufanya hivyo imeleta utulivu, hata kama siyo kwa asilimia 100, lakini utulivu mzuri kati ya Serikali na Vyama vya Wafanyakazi. Tunategemea Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kuwa na usikivu wa namna hiyo kuhakikisha Watanzania wote wanachangia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuwapongeza sana Mawaziri wa Nchi waliowasilisha hotuba za bajeti leo hii asubuhi. Kwa kweli bajeti zile zimesimama na mimi napenda kusema mapema kabisa kwamba naziunga mkono lakini tu nitachangia ili kuisaidia Serikali ijaribu kuweka marekebisho ya hapa na pale kuhakikisha kwamba utekelezaji wa bajeti zile unakwenda kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka nizungumzie suala hili la mfumo wa kutathimini wafanyakazi, *OPRAS*. Mfumo huu una nia njema sana na ni mfumo mzuri sana kama ungetumika vizuri lakini tatizo ninalolibaini katika sehemu nyingi za kazi, hakuna mipango mikakati ya kazi. Kwa hiyo, tathimini inakuwa ni ngumu kwa sababu hakuna malengo yanayolewaka, malengo yanayopimika kwenye taasisi zetu. Kwa hiyo, nafikiri ili mfumo huu ufanye kazi vizuri, nashauri Waziri, nashauri Serikali iangalie namna ya kuhakikisha kwamba sehemu zote za taasisi za umma, lakini vilevile hata za binafsi, kwa sababu ni mpango ambao unalenga kumfanya kila mfanyakazi awajibike na uwajibikaji siyo kwenye taasisi za umma tu hata za watu binafsi, kuwekwe mipango mkakati. Vilevile kuwe na hii mikataba ya wataje, *customer service charter*. Mikataba hii ni muhimu kwa sababu inawafunga wenye taasisi au wafanyakazi kuhakikisha kwamba wanatimiza yale malengo yaliyokusudiwa kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kuzungumzia habari hii ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko hii ni muhimu sana na nakumbuka imekuwa ikizungumziwa mara nyingi sana katika Bunge hili. Tatizo la mifuko hii kwa muda mrefu imekuwa ni

utofauti wa mafao kati ya mfuko na mfuko pale mtumishi anapomaliza muda wake wa kutumikia nchi. Sasa hii inaleta kero, kwa sababu unakuta watu wa taaluma moja, kiwango kilekile cha ngazi ya mshahara lakini wanapostaafu unakuta mwengine anapata chini kabisa hawezi kujimudu na mwengine anapata auheni. Bunge hili lilishapitisha sheria ya ku-*rationalize* mifuko hii na ilikuwa anatakiwa sasa kuajiriwa Msajili wa Mifuko ili mifuko hii iwe na uwiano unaofanana. Sasa nashangaa kwa nini kuna kigugumizi katika kutekeleza hili. Nitaomba Waziri wakati anafanya majumuisho atoe maelezo kwa nini *rationalization* ya hii mifuko haijafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuna kundi kubwa muhimu sana katika jamii yetu la wazee, watu ambao wametumikia nchi hii kwa namna mbalimbali aidha, katika kazi ya kuajiriwa au katika kilimo, hata WACHUNGAJI wa Makanisa nao wamechangia katika nchi kwa namna mbalimbali na Mashehe katika kuweka jamii katika misingi ya maadili mema na kujenga Taifa. Sasa watu hawa wanapozeeka, mazingira yao yanakuwa magumu sana, kwa nini kusiwe na mfuko ili watu hao nao wapate mafao? Nafahamu kuna stadi ambayo ilishafanyika na ikazinduliwa mwaka juzi na aliyekuwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Prof. Kabuya, wakisema kwamba utaratibu ule wa mafao ya wazee ulianza. Kitu ambacho kinachangia kuongeza umaskini katika jamii yetu ni kuwaacha wakiwa katika hali hohehahe. Takwimu zinaonyesha kwamba katika nchi yetu, asilimia 40 ya watoto yatima wanalelewa na wazee. Sasa wazee wale wanapokuwa ni maskini ina maana umaskini unasambaa katika jamii yetu kwa kiwango kikubwa sana. Utafiti ule uliofanywa ukaonyesha tu kwamba kama wangeweza kulipwa shilingi 16,000.50 tu wangeweza kuondoa kabisa hilo tatizo la umaskini. Naomba Serikali ije na majibu mazuri ya lini utaratibu huu wa mafao ya wazee utaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nataka kuzungumzia suala ambalo naliona linaendelea kujitokeza na limekuwa likijitokeza la utunzaji wa nyaraka za Serikali. Tumeona mara nyingi hapa Bungeni watu wanatumia vielelezo za nyaraka za Serikali ambazo ni za siri, zinatumika hadharani, itakuwa ni Serikali ya aina gani hata madokezo ya ndani, hata leo asubuhi hapa mtu anasema ameona dokezo sabili, hii ni nyaraka ya ndani ya mawasiliano hata uamuzi haujafanyika lakini inatumika kama kielelezo cha hadhara. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Na Serikali imekaa kimya.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Na Serikali haijazungumza kitu, tunaomba maelezo kwa nini hatuwezi kushughulikia mambo haya hata ndani ya nyumba kwanza mama na baba mnapanga mambo kabla hamjayatoa kwa vijana, kwa watoto, sasa mambo bado yangali kwenye chumba, yameshatoka hadharani, hii ni Serikali? Tunahitaji maelezo kwa nini utaratibu huu unaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda na mimi niungane na dada yangu Msafiri kupongeza kidogo kazi ya Taasisi hii ya TAKUKURU, aisifuaye mvua imemnyea. Mimi nilikuwa na kimbembe sana kwenye maeneo yangu ya shughuli ya uchaguzi, lakini nawahakikishia ndugu zangu Wabunge, kama taasisi hii isingekuwepo, wengi wetu

wasingeweza kuingia hapa kama siyo wale matajiri wakubwa, watu wa pesa za kawaida ilikuwa vigumu kuingia hapa hata kama wananchi wangekuwa wanakupenda namna gani. Kwa hiyo, lazima tukiri kwamba taasisi hii inafanya kazi nzuri lakini tuelewe tatizo la rushwa ni tatizo gumu hata marehemu Baba wa Taifa alikuwa anasema walikuwa wanatoa adhabu kali, wanawachapa viboko wakati wanaingia gerezani na viboko vingine wakati wanatoka wakawaonyeshe wake zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi hatuwezi tukarudi huko kwenye *corporal punishment*, lakini lazima tukiri kwamba tuwasaidie hao watu waweze kufanya kazi vizuri. Tusiwalinganishe mara moja kama nchi zilizoendelea zilizokuwa na taasisi hizi kwa miaka mingi, hiki chombo kimeanza karibuni lazima kisaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nataka nizungumzie habari hii ya *TASAF*, mfuko huu muhimu sana wa kusaidia juhudhi za wananchi. Kwa muda mrefu umekuwa ukijielekeza zaidi na shughuli za jamii, maendeleo ya jamii, zahanati, shule na madarasa.

Lakini nafikiri kwa mwelekeo huu ambapo nchi yetu tunajipanga tushindane Kikanda, Kimataifa, tushindane pia kwa utaalam wa *TASAF* na nguvu ielekezwe kwenye kuwawezesha wananchi kiuchumi yaani *economic empowerment* kwa sababu ni muhimu sana. Kule vijijini akinamama na vijana kupitia vikundi vyao wakipewa elimu, naamini kabisa *TASAF* itakuwa na mchango mkubwa na hapo itaimarishwa zaidi na mpango huu wa MKURABITA ambao kwa sasa bado unakwenda polepole. Hizi Wilaya chache zilizoteuliwa kwa mfano, kurasimisha mali, ardhi na kadhalika ili wananchi waweze ku-access mikopo bado ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba, angalau basi waangalie kwa kila Kanda kuwe na uwakilishi, siyo Wilaya zote zinakuwa upande mmoja. Tuhakikishe kwamba maarifa haya yanaweza kusambaa sehemu nydingi na kwa haraka zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusiana na masuala ya Tume ya Mipango. Nafikiri kwamba pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo sasa bado huduma zake zinapatikana katika Benki ya Raslimali. Jamani, hili eneo bado ni dogo sana kwani benki hii iko Dar es Salaam peke yake. Sasa wananchi wa Busega viyi wataifika hii Benki ya Kilimo ambayo iko Dar es Salaam wakati wakulima wote wako vijijini hawako mijini? Hebu mzisambaze hizi benki na kama haiwezekani basi mfungue madirisha kwenye benki za makabwela kama *NMB*, *CRDB* na kadhalika ili wananchi wengi waweze kuzifikia huduma hizi. Uzoefu wa nchi hii umeonyesha kwamba hata Mifuko mingine iliyokuwa inatolewa na Serikali, watu waliokuwa wanaweza kuifikia ni wale tu viongozi wa juu, watu wanaoishi mijini au wafanyabiashara wakubwa. Sasa matokeo yake ni kwamba mwananchi wa kawaida anaendelea kuachwa nyuma na mfumo wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimevutiwa sana na utafiti ambao unafanywa na Tume ya Mipango, ili kuifanya Tanzania iweze kutumia fursa za kiuchumi na kijiografia kwa ukanda wetu wa Maziwa Makuu wa Afrika Mashariki, lakini hata nchi za Kusini

mwa Afrika. Utafiti huo ni wa muhimu sana naomba sana Mheshimiwa Waziri asukume hii Tume ikamilishe kazi ili tuweze kuona matokeo ya utafiti huo na yafikishwe hapa na sisi tuweze kuwaeleza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tutaendelea kuimba Tanzania imekaa vizuri na ina fursa tele, kule kwangu kuna Ziwa Victoria pia kuna barabara kuu inayounganisha nchi yetu na nchi jirani. Kwa hiyo, tuitumie fursa hii.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbunge na muda wako umekwisha.

MHE. DR. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge na sasa napenda kuwataja wafuatao: Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa David E. Silinde na Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay. Lakini tutaanza na Mheshimiwa Joseph R. Selasini na waliotajwa wajiandae.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka kulichangia ni suala ambalo limekuwa likizungumzwa mara nyingi na viongozi wetu ambalo sasa linaludiwa mara kwa mara na naona lisipozungumzwa na hatua zikachukuliwa linaweza likatuletea sintofahamu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kuzungumza ni suala la udini, ila kabla sijaendelea kuzungumza naomba niseme kwamba mimi ni kiongozi katika Kanisa Katoliki. Nasema hili kwa sababu inawezekana katika kuchangia hili nikaambiwa nitangaze maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za karibuni tumekuwa tukiwasikia viongozi wetu wakikemea kuhusu kuibuka kwa udini katika nchi yetu na tumekuwa tukisikia viongozi wanaozungumza jambo hili wakituhumu baadhi ya Vyama vyा Siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishangaa viongozi wanayo mamlaka kwa mujibu wa Katiba na viapo vyा uongozi. Sasa nashindwa kujua ni kwa sababu gani hawachukui hatua dhidi ya jambo hili ambalo ni hatari sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunaelekea kwenye uchaguzi, baadhi ya magazeti na wananchi walikuwa wanatuhumu chama kimojawapo katika vyama vilivyoshiriki uchaguzi kwamba kinaungwa mkono na dini mojawapo kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa likirudiwa bila kuwekwa wazi wala bila mhusika kuhusishwa moja kwa moja na jambo hili. Nachelea kusema kwamba linaamsha hisia za wananchi na kwa sababu hiyo, badala ya kujenga nafikiria tunaendelea kubomoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu Ibara ya 19 inampa kila raia uhuru wa kuabudu katika dini anayoitaka bila kuingiliwa. Ibara ya 19(3) inaweka masharti kwamba bila kuathiri Ibara ya kwanza na ya pili utaratibu utawekwa. Katika nchi yetu upo utaratibu wa kuhubiri dini bila kuingilia dini za wengine. Lakini niseme kwamba suala hili ambalo limekuwa likianza kuibuka katika nchi yetu, halishughulikiwi kikamilifu. Huko tunakokwenda likiendelea tutatazamana vyama vyetu kwa mujibu wa dini zetu jambo litakalofuata tutawatazama Viongozi wetu kwa mujibu wa dini zetu. Tukiendelea hivyo tutaanza kutazama hata Viongozi wa Taasisi nyeti kwa mujibu wa dini zao na matokeo yake sasa Taifa litalikuwa vipande vipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba jambo hili ni bay a kuliko hata maandamano ya CHADEMA. Kwa hiyo, naitaka Serikali, *seriously*, jambo hili ilishughulikie. Haitoshi tu kiongozi kusimama jukwaani na kusema kuna udini akaishia hapo hapo. Serikali yetu ina vyombo kwa nini isitumie vyombo vyake kuhakikisha kwamba wanaoingiza jambo hili katika nchi yetu wanashughulikiwa hata kama ni vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Namba 5 ya mwaka 1992 iliyoanzisha Vyama vya Siasa, inakataza vyama kuundwa kwa misingi ya dini na inaonyesha waziwazi kwamba chama kitakachoshiriki katika jambo hilo hatua ambayo ni muafaka kwa chama hicho ni kufutwa. Sasa inakuwaje wasimamiaji wa Sheria, watu ambao tumewapa Mamlaka ya kutunza amani katika nchi yetu wanabaki kulalamika tu kwenye majukwaa bila kuchukua hatua inayostahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaudhi hasa kama muumini wa dini fulani unasilia chama fulani kinahusishwa na dini yako na wakati wewe huhusiki, inaudhi! Naishauri Serikali ichukue hatua inayostahili katika jambo hili kwa sababu ni ukweli usiopingika kwa sababu hata kwa nyakati tofauti Rais wetu amekuwa akilizungumza hili sasa imefikia hatua lishughulikiwe. Nasema kati ya mambo mazuri ambayo yalisimamiwa vizuri ni pamoja na utulivu ambao unatokana na kila mtu kuabudu dini anayotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, sasa nizungumze kuhusu rushwa na TAKUKURU. Sitazungumza kuhusu rushwa kubwa kubwa ambazo zimekuwa zikitajwa mara kwa mara. Sitazungumza kuhusu EPA wala Meremeta wala sitazungumza kuhusu rushwa zile ambazo sasa hivi zinashughulikiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba rushwa imekithiri ndani ya Mahakama zetu kwa sababu tafiti zinaonyesha hivyo na hakuna sababu ya mtu yeoyote kukataa hizo tafiti. Lakini ni ukweli usiopingika rushwa imekithiri katika Jeshi la Polisi

na inafanywa waziwazi kabisa. Kila mara ninapokuwa nasema kuhusu hawa ndugu zangu wanania na kama nawasema vibaya. Lakini nimekuwa nikisema na hii narudia tena, pale Himo sasa hivi tunavyozungumza na wiki zilizopita Polisi wanasindikiza malori ya mahindi kuyavusha kwenda Kenya kwa Pikipiki moja mbele na nyiningine nyuma na *SMG* mgongoni. Sasa swali langu ni kwamba je, Serikali haipo? kwani TAKUKURU hawapo? Nilishasema tena hapa Bungeni ni shilingi 50,000/= zinatolewa mchana kweupe kabisa watu wanaona. Sasa ukiniambia TAKUKURU ilifanya kazi kubwa katika uchaguzi tukaingia hapa, sawa ilitusaidia sisi tukaingia hapa lakini wanaoumia na rushwa ni watu wetu wa kawaida kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tunazungumza habari ya *DOWANS* kulipwa nilikuwa naunga mkono kutolipwa, tuangalie kwanza Sheria inasemaje na kesi imekwendaje. Lakini nilikuwa na hoja yangu kwamba kuna *DOWANS* nyangi sana huku chini, wananchi wanateswa sana na rushwa kuanzia kwenye vijiji, Kata na Wilaya. Watu hawapati haki zao tena haki zilizotajwa kwa mujibu wa Sheria, haki ambazo Serikali inapaswa izisimamie. Sasa kwa kuwa TAKUKURU wamefanya kazi nzuri hiyo ya kujenga Ofisi mpaka kwenye Wilaya, majengo tu hayatoshi, sisi tunachotaka ni kuangalia kwamba watu wametendewa haki. Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere alikwishesha wakati fulani kwamba kama rushwa ikiendelea kuwa Mahakamani au ikiendelea kuwa Polisi Taifa letu liko katika mgogoro mkubwa sana. Kwa hiyo, nawasihi ndugu zangu wa TAKUKURU kwamba hii ni *challenge* ambayo wanapaswa kuiangalia na naisihi Serikali yetu kwamba hii ni *challenge* ambayo wanapaswa kuiangalia kwa sababu ni kilio cha wananchi. Serikali inapeleka fedha za kutosha ili watu wahudumiwe lakini fedha zinaishia kwenye mifuko ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo napenda kulijadili ni mishahara hewa. Takwimu zimeshatolewa na *CAG* na wazungumzaji wengine pia wamezungumza. Inakuwaje ukienda kwenye Halmashauri wanakwambia kwamba sisi hatulipi bali Hazina ndiyo inayolipa. Sisi tukipeleka Hazina majina ya watu amba wamekufa au wameacha kazi au hawajaripoti kazini Hazina *hai-respond*. Ukiwa uliza Hazina wanasma Utumishi *hai-respond* na matokeo yake ni kwamba mabilioni ya fedha yamekuwa yakipotea kwa sababu ya mishahara hewa. Sasa tunamwomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ya hoja yake alete mkakati ni namna gani tutaondokana na aibu hii kwa sababu namna ya kupata takwimu ni ya kawaida kabisa, Maafisa Utumishi wako Wilayani na kila sehemu, inakuwaje jambo hili lisishe? Fedha ambazo zilikusudiwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi zinalipwa tu hovyo hovyo na hizi zinazolipwa ni watu wanakula? Je, zinarejeshwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo napenda kuchangia ni kuhusu uwajibikaji. Ni dhahiri kabisa Watanzania wengi wanaibbia Serikali kwa njia ya kutofanya kazi. Nenda kwenye Ofisi, ikicheza Simba na Yanga ni mjadala kutwa nzima, ikicheza *Manchester* na *Barcelona* ni mjadala kutwa nzima, yakiingia masuala ya uchaguzi sijui CCM imesema nini na CHADEMA imesema nini, ni mjadala kutwa nzima wakati Taifa hili ni maskini na mijadala inaendelea katika Ofisi mbalimbali wakati tuna Viongozi wanaosimamia hizi kazi. Mwisho wa mwezi watu wanapata pesa na wanadai nyongeza za mishahara. Sasa sikatai nyongeza za mishahara lakini tufanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui Serikali katika hilo ina nini la kusema. Watu wanachukua pesa wanakwenda tu na kinachoumiza zaidi unaingia kwenye Ofisi unamkuta anayepaswa kusimamia utendaji yeze ndiye anaanzisha hoja au mijadala ya *Barcelona* na *Manchester* na watu wanajadili tu. Au mtu anafunga Ofisi saa saba mchana anakwenda kula anarudi saa tisa au mtu anaingia na mayai au maziwa na kadhalika ofisini anauza. Mambo haya yanaitia aibu Serikali na yanatutia aibu kama Taifa, lazima tufike mahali tuseme ni mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tufanye kazi kwa sababu hapa tunahimiza wakulima wafanye kazi, lakini wakulima hakuna mtu anayewasimamia kwa sababu ile ni Ofisi yao wasipolima hawapati chakula na sisi tunawahimiza waende kwenye kilimo, lakini sisi hakuna anayetuhimiza. Hatufanyi kazi basi imekwisha hivi hivi. Ninaposema watumishi ni pamoja na sisi pia Wabunge, hata sisi Wabunge lazima tuwajibike kama Wabunge, tumekuja hapa Dodoma kufanya kazi na kuishauri Serikali sasa kama Mbunge yuko nje ya Bunge halafu mwisho wa mwezi anataka mshahara, posho na kadhalika hilo nalo lazima liangaliwe. Lazima Watanzania tufanye kazi, kama ni Wabunge tufanye kazi, kama ni Maofisa tufanye kazi ili tustahili kupata hicho ambacho tunakitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sitaki kugongewa kengele naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph R. Selasini na sasa nimwite Mheshimiwa David E. Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kutoa maoni yangu juu ya hotuba ya Ofisi ya Rais kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningeanza nalo ni suala la urasimishaji wa ardhi mijini na vijijini. Lengo kubwa la kuanza na eneo hili ni kwa sababu kwenye hotuba iliyosomwa na Waheshimiwa Mawaziri imegusa katika eneo langu la Mji wa Tunduma katika Jimbo la Mbozi Magharibi hususan eneo la maporomoko. Kimantiki suala zima la urasimishaji wa ardhi ni jambo bora na la msingi kabisa kwa nia moja tu ya kutaka kusaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo linakuja wapi? ni kwamba je, tumewaandaaje wananchi juu ya kupokea huu mkakati, yaani huu urasimishaji wa ardhi unaambatana zaidi ya MKURABITA. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho Mheshimiwa Waziri ajiandae kwa sababu wamejaribu *ku-pilot* kwa mwaka wa fedha unaokuja watafanya Tunduma pamoja na Kimara Baruti Dar es Salaam. Lakini je, tumewaandaaje Watanzania? Wanaelewaje kuhusiana na suala la MKURABITA? Wanaelewaje vilevile kuhusu urasimishaji wa ardhi vijijini na mijini? Kwa hiyo, hili ni lazima tutoe maelezo ili angalau wananchi waweze kunufaika na huu mkakati. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri naomba alichukue na alitilie maanani ili mwisho wa siku aweze kutoa majibu ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuja kwenye jambo la msingi na nizungumzie hasa Sekta ya TAKUKURU. Naweza kusema kitu kimoja kwamba TAKUKURU ndani ya Taifa hili imeshindwa kazi. Nasema nikiwa na ushahidi wa kutosha na Watanzania wote wanajua. TAKUKURU inafanya kazi kwa mashinikizo zaidi, yaani magazeti yakinyanyuka yakazungumza kitu fulani ndiyo TAKUKURU inaelekea huko, lakini haiwezi ikaenda ikafanya kitu kulingana na ushahidi uliopo. Kwa miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2005-2010, Taifa liligubikwa na kashfa kubwa kama za *EPA*, *RICHMOND*, Rada na kashfa nyingine makubwa lakini bado TAKUKURU wameshindwa kuchukua hatua dhidi ya hizi kashfa kubwa zilizoligharimu Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima sasa kitengo cha TAKUKURU kifanyiwe kazi kwa sababu ukienda TAKUKURU hususan Wilayani kama Jimboni kwangu Mbozi Magharibi kuna kesi ndogo ndogo za mtu kumpa Polisi shilingi 1,000/=, mtu kumpatia Mtendaji wa Kata kuku ndizo ambazo zinachukuliwa hatua, lakini hizi kesi kubwa zinazoliangamiza Taifa hazichukuliwi hatua. Kwa hiyo, hili ni lazima muwe mnaliona na najua kabisa Mheshimiwa Mkuu wa Kitengo cha TAKUKURU analijua hili. Alijaribu kutuelezea kwenye semina Dar es Salaam na alitueleza changamoto zinazoikabili Idara yake lakini mpaka leo tumeendelea kuwa ni watu wa maneno, ni watu ambao tumeshindwa kutekeleza wajibu lakini Taifa halihitaji kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajaribu kuzuia rushwa, lakini Marehemu Mwalimu Nyerere alishasema rushwa ni adui wa haki. Mahali popote palipo na rushwa hapawezi kupatikana maendeleo. Asilimia kubwa ya watu wanaotoa rushwa ukiacha watu wakubwa lakini wananchi wa hali ya chini ndiyo ambao wanakabiliwa zaidi na hizi rushwa kwa sababu mahali popote sasa hivi wataambiwa huwezi kupata huduma Hospitalini mpaka utoe rushwa, huwezi kupata huduma ya kupata faili lako Mahakamani mpaka utoe rushwa na huwezi kupata huduma ya elimu mpaka utoe rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mazingira yote haya yanajengwa kwa sababu TAKUKURU imeshindwa kuchukua hatua madhubuti kwa maana ya kushughulikia zile kashfa kubwa ambazo zimelikabiri Taifa hili. Kwa hiyo, katika hili nafikiri wananchi sasa wanataka majibu, tunataka tuone kweli TAKUKURU yenyе meno siyo TAKUKURU ya maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala haya haya ya TAKUKURU maana yake lazima turudi na nahitaji nilizungumzie kwa undani zaidi, kwa Mfano, kashfa za *Richmond* na *EPA* kwa hali ya kawaida viongozi wakubwa waliokuwa wanahusika na masuala haya na Bunge hili ambalo lilijadili, walijaribu kuchukua hatua wao wenyewe. Wengine walijiuzulu nafasi zao na ninyi wenyewe mnawajua lakini mpaka leo TAKUKURU inasema haina ushahidi wakati ushahidi wa awali kabisa wa hizi kesi ulianzia ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la *EPA*. Ule upoteaji wa zile fedha TAKUKURU inaeleza kwamba haina ushahidi, lakini Watanzania wanajua

ushahidi, mazingira ya ushahidi ni pamoja na aliyejewa Gavana kuondoka na kufa katika mazingira ya kutatanisha. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanaonesha kabisa kwamba pana walakini juu ya Taifa hili. Sasa bado tunaendelea kuyumba kwa sababu hizi fedha zote zingeweza kupatikana zingepeleka maji katika Kata yangu ya Ndarambo, Kata yangu ya Kamsamba, zingepeleka hospitali katika Tarafa ya Msangano na Kata nyingine ya Chitete pale, wote wangeweza kupata huduma hizo kwa sababu fedha hizi zinapotea na ndiyo maana kila mwaka ripoti za CAG zinakuja na mapungufu yale yale kwa sababu TAKUKURU wanashindwa kuchukua hatua katika kashfa kubwa ambazo zinapelekea Taifa hili kupoteza mwelekeo katika maeneo madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika jambo la tatu, suala la maslahi ya Watumishi wa Umma. Kimantiki Watumishi wa Umma wamekuwa wakilalamikia kiwango cha chini cha mshahara. Ukiangalia pale kwenye *TGS* zinavyoandikwa kwa mfano *TGS A* ambacho ni kiwango cha chini kabisa kinakuwa *graded* kuanzia Namba 1-8 lakini kinachoelezwa kwenye Taifa ni kile kiwango cha juu kabisa cha shilingi karibu 124, 000/= kile kiwango cha chini cha *TGS A* ambacho mtumishi anaanzia huwa hakiwekwi hadharani, ni kama shilingi 80,000/= au kitu kama hicho. Watanzania sasa wanasema hivi, ukiachia suala tu la kuongeza mishahara kwa watumishi tunahitaji sasa thamani ya fedha iweze kutiliwa maanani, kwa sababu hata Zimbabwe pale watu wanalipwa mabilioni ya shilingi lakini hayana thamani yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kila wakati mmekuwa mnasema hatuna hifadhi ya kutosha ya fedha za kigeni katika Benki Kuu, sasa nani apeleke pale hifadhi ya kutosha kama siyo Serikali inayohusika? Maana yake mnahitaji sasa wakati uliopo kutafuta namna ya kupata hivyo vyanzo vya fedha ambavyo vitaweka fedha za kigeni zikiwemo hizo dola ambazo mnasema ndiyo zinaweza ku-*balance* na kuifanya thamani yetu ya fedha isiyumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maslahi ya umma ni lazima yazingatiwe. Ukianza katika ngazi ya mshahara uongezwe lakini pia ni lazima mfanye *real restructuring* ya taasisi nzima kwenye suala zima la mshahara na menejementi ya utawala wa umma. Kwa hiyo, suala la maslahi vilevile liambatane na kitu kinachoitwa ujenzi wa nyumba kwa maana ya makazi kwa watumishi. Makazi ndiyo ambayo yanaongeza motisha (*morale*) kwa wafanyakazi. Sasa mtu anakwenda Mbozi ambako ndiyo anakuta zile nyumba za Serikali zilishauzwa, anakwenda kuanza kazi anafikia gesti ya ajabu, maana hata mantiki yenyewe ya kufanya kazi inapotea, hata heshima yake ya kazi inapotea kwa sababu anategemea mwisho wa mwezi ndiyo aje kulipa na ninyi wenyewe mnajua katika masuala ya utumishi, mtu anapoajiriwa analipwa fedha ya awali kama ya mwezi mmoja tu ili aweze kujikimu baada ya hapo atafute makazi ya kuishi. Sasa kwa Serikali hii ambayo kiwango chake cha mshahara bado ni kidogo na wananchi hawapati fedha za kutosha, kamwe hawawezi kufikia yale malengo ambayo wanayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ambayo ningependa niizungumzie ni kwenye ajira za kada ya chini. Serikali yetu kwa sasa hivi pamoja na kwamba walijaribu

kuleta mfumo wa *decentralisation* kwamba inatakiwa sasa tushushe mambo mengi ya kiutawala kwenda chini, lakini ajira za kada ya chini mpaka leo hii bado zinatolewa vibali au kufanyika kutoka ofisi kuu (*central office*) kwa maana ya Wizara husika. Sasa watu wa Mbozi wakiwemo wa Jimbo langu wanalamika, wanasesma hivi sasa Mheshimiwa tunaomba utusaidie kupata ajira za udereva, uhudumu ofisini, ulinzi, maana yake kila Wilaya ina madereva wa kutosha, watu wenye ujuzi wa ulinzi wa kutosha, kila Wilaya na kila Jimbo lina watu wenye ujuzi wa uhudumu wa ofisi kama masekretari, lakini leo wanashindwa kuajiriwa kwa sababu tu ajira zinaanza sehemu fulani ambako ni Makao Mmakuu, Wizarani, Dar es Salaam. Watanzania wachache watu wa Mbozi ambao hawana taarifa, wala hawana uwezo wa kupata hata fedha ya nauli ambayo itawafikisha Wizarani kwenda kufanyiwa usaili, mwisho wa siku wanakosa ajira. Kwa hiyo, mnatuletea watu wa Dar es Salaam wanakuja Mbozi kufanya,kazi, wakifika pale wanaondoka kwa sababu ya mazingira ya pale kuwa magumu kwa wao kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni lazima Serikali mkubali kwamba lazima mtuachie Halmashauri zetu husika ziajiri watu wa kada ya chini wa aina zote na wala siyo sasa ofisi za juu kwa maana ya Wizara, Mawaziri na watu wengineo waendelee kuajiri hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tano ni kuhusiana na *issue* ya udini, hili na mimi siwezi nikaliacha. Taifa sasa hivi limegubikwa na simanzi ambayo watu wote wanajua wakati wowote lolote linaweza likatokea, lakini udini una tafsiri pana zaidi kuliko watu wanavyofikiria. Udini ni hisia, kitu ambacho mtu unakiamini, hujawahi kukiona, humjui huyo Mungu, humjui huyo Muhammad, humjui huyo Yesu, yaani ni vitu ambavyo huwijui lakini umezaliwa navyo, umekuwa navyo, umeishi navyo na kuvishika, ni hatari zaidi kuliko kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia kitu kimoja maana yake *issue* ya udini imeanza wakati wa uchaguzi mkuu hususan wa mwaka 2010. Vongozi hao hao ambao mwaka 2005 waliambiwa ni chaguo la Mungu ilipofika mwaka 2010 watu waliposema hapana wewe leo siyo chaguo la Mungu, mwingine ndiye chaguo la Mungu ndipo udini ulipoanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Taifa linaweza likaenda namna hii? Tuzungumze ukweli maana yake hata sisi Majimboni watu watasema huyu ni chaguo la Mungu, unakwenda mwaka 2015 hujatekeleza yale ambayo Mwenyezi Mungu alitaka uyafanye, maana yake siyo tena chaguo la Mungu, maana yake unawenza ukachaguliwa na Mungu usipotekeleza yale baadaye Mungu anakutema, anakuacha. Kwa hiyo, Mungu huwa ana chaguo ndiyo maana tunasema kuna Manabii wa kizazi na kizazi, kuna viongozi wa kizazi na kizazi na ndiyo maana leo katoka Siame anakuja Silinde ndiyo wakati wangu, atatoka Silinde atakuja mtu mwingine ndiyo wakati wake, sasa kwa nini kulishikilia hili suala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uwafikishie taarifa maana yake Mawaziri, hata Rais naye alijue kwa sababu amekuwa akilizungumza mara kwa mara kwamba udini, udini lakini viongozi tumekuwa tukilikataa hili na ni lazima tuelimishe Taifa kwamba

jamani umoja na mshikamano ambao walijenga mababu zetu akina Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, unashikwa kwa nguvu kwa sababu itakapoanza vita ya udini hapatakuwepo na suala la CHADEMA wala CCM, tutaanza Wakatoliki tuko wapi? Uwe CCM *uwe* CHADEMA, *uwe* NCCR - Mageuzi, *uwe* TLP, tutakuwa pamoja. Waislamu mko wapi? Nendeni kule, vita yake haiwezi kuisha leo itaendelea mpaka msuluhishi mwenyewe ambaye ni Mungu atakapoamua, ndiyo suala la imani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri husika ni lazima sasa ukiachia kulikemea, tuache mara moja kulizungumzia hili suala na ni lazima tuchukue dhamana kwa maana kwamba kila kiongozi anayehusika na hili jambo aweze kukaa kimya na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sita, ni kuhusu utawala bora. Neno utawala tu maana yake ni ufalme, hapa lazima tuanze kubadilisha mantiki, nchi siyo ya kidikteta, tupeleke sasa badala ya kuwa utawala bora, iwe uongozi bora. Kiongozi ni mtu anayesikiliza, mtu anayechukua ushauri lakini mtawala ni mtu ambaye ana-*dictate*, ni mtu ambaye hana maamuzi, atakachoamua ye ye ndiyo sahihi. Sasa mantiki ya utawala bora lazima iendane na kitu kinachoitwa maamuzi magumu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda umekwisha.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Namwita Mheshimiwa Mustapha Akunaay na wafuatao wajiandae; Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa Zainab Kawawa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa ufupi naanza walipoachia wenzangu kuhusu suala la udini kwa sababu hii ni *time bomb*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nchi hii imelifumbia macho kwa muda fulani. Hili suala lilianza mwaka wa 1992 baada ya Vyama vingi kuanza. Kwa bahati mbaya watu walioanza kuhubiri siasa hawakujua siasa ni nini, badala yake ili wakubalike katika jamii wakawa wanatumia vikundi. Kwa mfano, mwaka wa 1995 wakati wa uchaguzi vilitokeza vibendera vingi baadaye watu wakatambuana kupitia vibendera (vitambaa vidogo) na baadaye watu wa TRA wakawa wanatoza watu kutokana na vibendera vilivyokuwa vimewekwa kwenye maduka yao. Hali hiyo ikaendelea mpaka mwaka wa 2000, hapo ikawa baridi kidogo, sasa mwaka 2005 ikaanza lakini mwaka 2010 ndipo ilifikia kilele chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la udini ni bay a kiasi kwamba sasa hivi pamoja na udini nchini watu wanatambuana pia kwa vyama. Imefika hatua mpaka kuna mtindo wa kutambuana kwamba mtu aliyeavaa nguo hii ni CCM, aliyeavaa nguo hii ni chama fulani, huyu ni CHADEMA na huyu ni CUF. Kitu ninachofahamu ni kwamba duniani

kote chama kinajulikana wakati wa uchaguzi na kinachaguliwa kwa sababu ya ubora wa sera zake na uchaguzi ukiisha mambo yamekwisha na siasa inakuwa ni Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushabiki tunaoufahamu sisi ni wa mpira. Duniani kuna mchezo wa mpira katika bara la Ulaya, Amerika na hata hapa Tanzania zinajulikana timu kama Yanga na Simba, Ulaya *Manchester, Leeds*, na kadhalika, lakini sasa tukiendeleza hivi vitu vidogo vidogo kesho vitakuwa vikubwa. Tumefika mahali sasa watu kwa imani zao wana salamu zao. Sasa hivi imefikia hatua mpaka watu wameogopa kusalimiana *Assalam Alaykum* mpaka mtu anachanganya na salamu tatu, *Assalam Alaykum*, Bwana asifiwe, Tumsifu Yesu Kristu, yote hayo ni kujaribu kuua ile itikadi kwamba tunakwenda wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kutumia Ofisi ya Rais kudhibiti hili jambo, watu warudi katika misingi yao ya zamani, kwanza inatakiwa iwe kinyume cha sheria kama kuna mahali ambapo bendera imewekwa kama siyo ofisi, iko njiani kwenye vijiwe, hivi ndiyo vya kuanza navyo kwanza, bendera ni kitu cha heshima, ikae ofisini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguo za chama kama inavyokatazwa hapa Bungeni pia ofisini zikatazwe. Unakwenda ofisini unakuta mtu amevaa *T-shirt* imeandikwa chama fulani, anajulikana huyu ni wa chama fulani. Hicho kitu kitakuwa ni hatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wenzangu wamesema sana juu ya hili jambo nasogea kwenye suala la utawala bora. Katika utawala bora labda nianze na maadili ya wafanyakazi wetu. Maofisini wafanyakazi wamekosa nidhamu, wanakuja ofisini kama ilivyosemwa *time* wanayotaka, wanavaa nguo ambazo siyo za heshima, wanazungumza lugha ambazo siyo za heshima. Ofisi za Serikali sasa hivi zimetoa kitu kinaitwa *customer charter*, mteja ameingia ofisini mhudumu au anayekutwa labda ni Sekretari anazungumza na simu, *computer* yake ina muziki, maskini wa Mungu mkulima ambaye ametoka kijijini ana shida ya kumuona labda ni *DC* au Mkurugenzi, anakaa pale masaa matatu lakini wao wanapiga simu, wanasikiliza muziki kwenye *TV*. Sasa inatakiwa *computer* zote ofisini, muziki ufungwe maana masekretari wanasikiliza muziki mpaka wana-type vitu ambavyo havieleweki. Sasa ukikuta barua imetoka Serikalini ina makosa milioni moja kwa sababu hakuna umakini, hakuna umahiri na watu wakubwa wanaweka sahihi makaratasi ambayo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/2008, Serikali ilitoa nafikiri ni waraka siyo sheria kwamba nyumba za Serikali ziuzwe kwa wafanyakazi wa Serikali. Nyumba zingine katika Taasisi za Serikali kama hospitali ziliuzwa mpaka sasa hivi imefikia mahali kwamba hospitali hauwezi ukaiongeza au kama kulikuwa na chuo hakiwezi kikaongezwa kwa sababu wakuu wa pale walikuwa wameuziwa nyumba kuanzia Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Polisi wa Wilaya, Afisa Usalama, wamechukua maeneo makubwa katika miji. Mijini kuna maeneo yamepangiwa majina, *low density, high density, medium density* sasa mpaka watu wengine wanakuwa na heka tatu, au nne mjini wanazuia *expansion* ya mahospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Mbulu kulikuwa na eneo la hospitali, wafanyakazi na Wakuu wa Serikali wakauziwa eneo mpaka hospitali ya *MSH*, Mheshimiwa Rais alikuja kuitembelea akasema mtaongeza kutoka wapi? Limechukuliwa eneo la takriban heka za mraba 250, sasa wananchi wamekwama na Serikali kwa sababu wale ambao wameuziana wote ni mtandao, kwa hiyo, inashindikana. Sasa tunaishauri Serikali itazame kama ilikuwa ni tatizo wakati ule wale watu walikuwa Serikalini walishindwa kujenga, sasa wamejenga wabaki na zile nyumba, lile eneo lingine lifanyiwe shughuli za Serikali au sivyo basi eneo lile liwe *revoked* ili maendeleo ya nchi yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunazungumzia *EPA* lakini *EPA* zetu ziko Vijijini na Wilayani. Watendaji wa Vijiji wanachukua hela za wananchi kwa michango wanazila, Mkurugenzi hachukui hatua, wao wanahamishwa. Kwa hiyo, katika utawala bora tunataka kusema ufile mpaka kwa *Ward Executive Officers (WEO)* na *Village Executive Officers (VEO)* hili liambatane na watendaji ambao wanakaa mahali pamoja maana yake wakizoeana basi wengine wanaanza tena mtindo wa kuwakomoa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi akichangishwa mchango wa maendeleo kama hajalipa kwa *by-laws* anakamatiwa mali yake inauzwa, lakini Mtendaji hakamatwi, hapelekwi mahali popote, Mkurugenzi akizembea hafanyiwi chochote na Sheria imetungwa tena sasa hivi akisimamishwa kazi mshahara ni *full*, siyo nusu, kesi inachukua miaka sita, kama ni kesi ya TAKUKURU ianze Wilayani, iende Mkoani, iende mpaka kwa *Director* wa TAKUKURU, iende kwa *DPP*, sasa miaka sita kesi haijawkisha inakuja kwisha mashahidi wamekufa, karatasi zimepotea, anaachiwa anakuja kurudishwa kazini. Tunataka kuishauri Serikali kwamba hawa *Village Executive Officers* na *Ward Executive Officers* wadhibitiwe fika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna mgongano wa madaraka baina ya Serikali Kuu na Halmashauri. Mpaka sasa hivi hatujaelewa kati ya Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya mipaka ni wapi, maana Mkurugenzi anatoa amri, Mkuu wa Wilaya anatoa amri. Tuna mifano mingi lakini kwa sababu ya muda Wabunge hili tutawasiliana kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mshahara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa nikuombe usisome, jitahidi ku-*focus*.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, *no nina- refer*, mimi siyo msomaji kama wengine uliowasikia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafanya *reference* kwamba pointi namba fulani, namba fulani, sasa *nili-refer* nimeona natakiwa nizungumzie juu ya mshahara. Mshahara tunaouzungumzia ni *minimum wage*, tumesikia *speech* ya Waziri hatujaelewa kama umepandishwa maana yake wakati Waziri wa Fedha akitoa hotuba yake alisema Waziri

anayehusika na Utumishi atatoa kauli juu ya mshahara, lakini tunapata mshangao kwamba hatujaona mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kuzingatia wakati mishahara inapangwa ni kuangalia hali ya fedha zetu inavyokwenda, kama mtiririko wa fedha ni hivyo basi mshahara usiwe unaombwa kupandishwa ila Serikali itambue kwamba mshahara fulani haufikii kile kitu kinachoitwa *living wage*. Kwa hiyo, iwe ni *automatic* siyo mpakaafanyakazi wawe wanalamika. Hata leo kwa mfano, wafanyakazi wanapolilia kwamba mshahara wa chini ufile shilingi 315,000/=, pengine hata hiyo ni *wrong assumption* kwa sababu sio *living wage*. Kwa hiyo mishahara ya wafanyakazi wa umma upangwe kwa uwezo wa huyu mfanyakazi kuishi, wale wengine tunajua kwamba wamepangiwa kila mwaka anapanda kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linasikitisha juu ya utumishi wa umma ni kwamba mara mtumishi wa umma anapostaifu, lake limekwisha na anakuwa hata akienda ofisini hatambuliwi na ndiyo maana kuna malalamiko mengi ya kwamba watumishi wengi hawajalipwa haki zao za uezemi na wanaishi katika hali ambayo ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nianze kwa kusema kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo nilishapata nafasi ya kutoa mawazo yangu au ushauri wangu kwa hizi Idara mbalimbali ambazo zinazohusika. Nilikuwa sikupanga kuchangia, lakini baada ya kusikia kwamba nyaraka za Serikali zinachukuliwa kama makaratasi yoyote ikaniuma sana. Nyakati zangu kama Katibu Mkuu Utumishi au wakati nikiwa kwenye Utumishi wa Umma jambo hilo lisingewezekana kabisa. Sasa nasikitika kuona linawezekana wakati tuna teknolojia ambayo ni *advanced*. Ndiyo maana leo nimeamua kuongezea ushauri kwa ule ushauri ambao nilishatoa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na utawala bora. Utawala bora ninavyouelewa una vipengele vingi, kuna uwajibikaji, utawala wa sheria, demokrasia, kutokuwepo na rushwa *absence of corruption*, mifumo mizuri ya uendeshaji, miundo mizuri ya Taasisi mbalimbali, ushirikishwaji wa wananchi na ulinzi na usalama na nitazungumzia uwajibikaji. Uwajibikaji Serikalini unaanza na kiapo cha Rais. Rais anapokula kiapo cha kuilinda Katiba na kuwatumikia wananchi bila ubaguzi wowote basi hapo uwajibikaji ndipo unapoanza Serikalini. Kwa sababu baada ya hapo anaunda Serikali, Wizara mbalimbali na Idara mbalimbali na hao Wakuu wa Idara hizo na Wizara hizo wanakula kiapo mbele ya Mungu na mbele ya wananchi, kwamba watawatumikia bila ubaguzi na kwa uaminifu mkubwa sana. Kwa hiyo, nasikitika sana ninapoona Watendaji wa Serikali siku hizi hawajibiki wakati wanatumia madaraka na mamlaka walijopewa na Rais ambayo yeeye alikula kiapo cha uaminifu kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali matatu huwa yanaulizwa kuhusu uwajibikaji. Swalii la kwanza wanasema Watendaji wanawajibika kwa ajili ya nini, bila shaka kwa ajili ya majukumu ambayo wamepewa. Swalii la pili, wanawajibika kwa nani? Serikalini lazima wawajibike kwa Rais pamoja na kwa wananchi. Lakini swalii gumu zaidi wanawajibishwaje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba usisome.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Ni *points* tu. Labda katika kuchangia hilo niseme mambo fulani fulani kwamba Afisa Utumishi na Utawala ni mtu muhimu sana katika sehemu za kazi. Ni tatizo kubwa sana tangu nichaguliwe kuwa Mbunge ninapokuwa kule Wilayani naona kwamba Watendaji hawawajibiki ipasavyo. Lakini kuna Afisa Utumishi na Utawala ambaye anatakiwa yeye sehemu za kazi aangalie kwamba kuna utekelezaji wa utawala bora. Kwa hiyo ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, Watendaji Wakuu kama Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wanapoteuliwa mara nyingi wanakuwa hawana *the habits of management*, wanatakiwa wapewe *the habits of managements* peke yake lakini *the habits of humans resources management*. Kwa sababu unapokuwa Kiongozi sehemu za kazi na unapokuwa na watumishi chini yako inabidi ujue na mahitaji yao, ujue matatizo yao na uweze kusimamia maslahi yao na utafanya hivyo kama umepewaa *the habits of human resources management*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala katika miaka 1980 na bahati nzuri Katibu Mkuu wangu *he was a very good economist*. Alikuwa mchumi mzuri sana amesoma Ujerumani, lakini hakuwa na *idea* yoyote ya utawala. Kwa hiyo akaniambia Bwana Ntukamazina wewe shughulika na utawala, mimi nitashughulika na uchumi. Sasa nikapata shida ikabidi ndiyo niwe nawaelimisha Wakurugenzi wenzangu na Viongozi mbalimbali kuhusu umuhimu wa kusimamia maslahi ya Watumishi. Sasa nafurahi kwamba kuna *institute* imeanzishwa pamoja na kile Chuo cha Magogoni cha Utumishi wa Umma, naomba vyuo hivi vitumike vizuri kwamba Viongozi mbalimbali wanapoteuliwa waende kupewaa *the habits of management*, wajue maana ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika pia Chuo hicho kitaweza kujenga uzalendo na Utaifa baina ya watu hao, Viongozi watakaokwenda kwenye chuo hicho. Niliwahi kuwa Mwalimu wa Kivukoni kwa miaka mitano. Kivukoni Viongozi walikuwa wanakuja kusoma siasa ya ujamaa na kujitegemea. Lakini *at the same time* tulikuwa na *military training* kuhakikisha kwamba wanapata ukakamavu, lakini *military training* ilikuwa ni kama *military training* ya vijana. Kwa hiyo, ilikuwa inajenga uzalendo, inajenga nidhamu ya kazi. Kwa hiyo, nashukuru kwamba Rais ana mpango wa kuirudisha *National Service* ambayo itasaidia. Lakini kama ikiwezekana kwenye uongozi *institute* kama Viongozi wanakwenda kwa miezi mitatu, basi wapate na *military training* huko huko kama tulivyokuwa tunafanya Kivukoni ili wawe wakakamavu, waweze kujenga nidhamu. Ningependa jambo hilo lifikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *neutrality* na *confidentiality* katika Serikali ambayo ndiyo imenifanya leo niweze kuchangia. *Neutrality* na *confidentiality* katika Serikali ni uhai wa Serikali na kama *neutrality* inakosekana kwa Watumishi wa Umma pamoja na *confidentiality* basi Serikali iko matatani. Kwa hiyo nawaomba Viongozi wa Wizara mbalimbali wahakikishe kwamba tunajenga maadili, tunahakikisha kwamba tunatumia teknolojia ya kisasa kwamba siri za Serikali zisiendelee kuvuja. Nitoe mfano wa *White House* ya Marekani. *White House* ya Marekani iko *accessible* kwa umma, wanasema ni *National Monument* ambayo ni *open to the people* na watu wanaitembelea na mimi niliwahi kuitembelea unatembezwa kila mahali. *But at the same time* wakati unatembezwa kuna ulinzi mkali na usalama wa *White House*. Naomba sasa hivi nisome *quotation* kuhusu *White House* utaniruhusu nisome Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema “*The White House is the residence of the Chief Executive, President ni Chief of Executive. At the same time is an office building where the affairs of state are conducted and a national monument open to the public, so far are the secret service is concerned. A basic conflict exist from the start. The need from maximum access kwenye White House watu waitembelee on the one hand at the same time the need for maximum security*”. Sasa wao wana uwezo mkubwa sana wa kuwaruhusu watu kutembelea *White House* but at the same time wana gadgets zao, wana system zao za kuhakikisha hakuna siri kuvuja, kwamba *the White House remains secure despite* ya watu kuitembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulisisitiza ni kwamba, tujenge *allegiance* na uaminifu kati ya watumishi wetu kuhakikisha kwamba Serikali inaishi kwa siri. Hizi *reform za public service* ambazo tulizianzisha ambazo zinaendelea lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaondoa urasimu, Serikali inafanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuhakikisha kwamba wananchi hawakwamishi katika utoaji wa huduma, lakini pia wawekezaji hawakwamishwi. Jambo la kuzingatia kwa watendaji Serikalini ni kwamba, *government is in business*. Inafanya *business* na *Private sector* na kwa hiyo, watumishi naomba tuwe na *change of mindset*, watumishi wajue kwamba Serikali iko kwenye *business* na kazi yao ni kutowakwamisha wananchi, ni kutowakwamisha wawekezaji, kuhakikisha kwamba sheria zinapitiwa, hazikwamishi *business* za Serikali, tuondoe urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa *TASAF* na *MKURABITA*. *TASAF* na *MKURABITA* ni Idara zinazofanya kazi vizuri sana. *MKURABITA* kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza lengo lake ni kurasimisha mali na biashara za wanyonge na ndio tegemeo la wanyonge. Kwa hiyo, bajeti zao nimezungie ni ndogo sana, bajeti ya *TASAF* na *MKURABITA* ningeomba miaka ijayo ziongezewe uwezo kwa sababu zinalenga kuwasaidia wananchi wa kawaida, vile vile zinalenga kuondoa umaskini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Mfuko wa Rais. Huu Mfuko wa Rais kuna Mbunge ambaye amechangia asubuhi akaufananisha na *DECI* kwamba ni utapeli. Hapana, ulipoanzishwa Mfuko huu nilikuwepo, ulianzishwa mwaka 1984 na ulianzishwa

na Marehemu Sokoine alipokuwa Waziri Mkuu, alikuwa ni mtu anayependa wananchi wake, akawa anatoa fedha kutoka kwenye mshahara wake kuhudumia Mfuko huu aliouanzisha, mshahara wakati ule ulikuwa mdogo, shilingi 3,000/= lakini alijitolea sana. Baadaye baada ya kufariki dunia Rais Nyerere akaona kwamba lazima aendelee kumuenzi na huu Mfuko ukaanzishwa rasmi mwaka 1988 kwa Sheria Namba 375 na lengo lake ni kuwasaidia akinamama, vijana na wale wote ambao ni *disadvantaged*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa miaka 20 iliyopita tangu Baba wa Taifa hawakupata msaada wowote kutoka Serikalini, ikabidi sasa wakope kutoka Benki na mnajua riba za Benki zilivyo kubwa. Ni mwaka jana nafikiri ambapo Rais Kikwete amewapa shilingi bilioni tatu kama mchango wa Serikali. Sasa katika kukopa kwenye Benki wanapata shida sana na ndiyo maana bado wako kwenye mikoa michache sana. Ningependa waende Ngara waweze kuwasaidia wananchi ambao wana matatizo, vijana na akinamama lakini hawawezi kwa sababu ya hii mikopo wanayoipata Benki ambayo ina riba kubwa sana. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali wausaidie Mfuko huu kama vile Baba wa Taifa alivyokuwa anausaidia na jinsi Rais Kikwete ambavyo ameanza kuisaidia ili waweze kupata *seed money* aweze kuwasaidia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishatoa ushauri wangu kwa Idara hizi lakini kilichonifanya nisimame leo ni ule uvujaji wa siri za Serikali, hiyo imeniuma sana kwa sababu nyakati zetu hilo jambo lilikuwa halifanyiki kabisa. Kwa hiyo, nawaomba viongozi Serikalini pamoja na watendaji turudi kwenye maadili, najua kuna matatizo, kwa mfano, wafanyakazi wetu sasa nadhani wameanza kujilingiza sana kwenye itikadi za vyama. Ukishajiingiza kwenye itikadi za vyama unapata matatizo kama mtendaji. Unaweza ukavujisha siri za Serikali kwa sababu ya itikadi yako au kwa sababu umepewa rushwa. Kwa kweli watendaji wanatakiwa kuwa waaminifu *to the government of the day, they have to be faithfully to the government of the day*. Nina mifano, Rais Kennedy alipoingia madarakani mwaka 1961 viongozi wake wa kisiasa, Mawaziri, walikuja kuona kwamba, watendaji wa Serikali hawakuwa waaminifu sana, wakafikiri kwamba bado wako kwenye *izen hour take over from izen hour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba, hata Marekani inakuwa *concerned* na uaminifu wa watendaji ingawa ni nchi yenye *system* zilizoimarika. Sasa sisi wa kwetu wasipokuwa waaminifu kwa *the government of the day* inakuwa matatizo makubwa. Naomba viongozi kuhakikisha kwamba, wanatumia teknolojia ya sasa lakini pia tujenge maadili katika Vyuo vyetu vya Uongozi pamoja na hiki Chuo chetu cha Utumishi wa Umma tuanze kuhakikisha kwamba tuna-*instil* haya maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Zainab Kawawa na wafuatao wajiandae; Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Fakharia Shomari na Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. ZAINAB M. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Napenda kuanza kwa kuunga mkono hotuba hii. Naipongeza sana Serikali kwa kuwa imezingatia yale mahitaji muhimu yanayohitajika kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa ombi maalum kutoka kwa wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria. Katika hili naomba nitumie kanuni ya 61 ya Bunge *ku-declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria. Wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria baadhi yao mpaka leo hawajalipwa mishahara na Serikali na moja ya sababu wanazozitoa ni kwamba Wizara ya Fedha inasubiri Ofisi ya Rais kupeleka orodha ya majina. Kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Rais, Utumishi iharakishe kupeleka majina ya wafanyakazi hao ili waanze kulipwa mishahara yao. Chuo Kikuu Huria ni chuo ambacho kwa kweli hakina *income* kubwa sana, kimekuwa kikitumia *sources* zake mbalimbali za *income* kuwalipa mishahara wafanyakazi kwa zaidi ya miezi 10 na hii imepelekea kutumia takriban zaidi ya shilingi milioni 800 kiasi ambacho kingeweza kutumika kufanya shughuli zake nyingine za maendeleo. Kwa hiyo, ningiomba sana Serikali ione umuhimu wa kuwalipa mishahara yao wafanyakazi hawa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha Sekretariat ya Ajira. Chombo hiki kama kitafanya kazi ipasavyo ni matarajio ya Watanzania wengi kwamba hakutokuwa tena na yale malalamiko ya eti fulani aliajiriwa kwa upendeleo. *In fact* sisi tumechelewa, wenzetu India walanzisha mfumo huu tangu mwaka 1956. Nitaomba nitumie kanuni ya 60 kufanya *reference* ya majukumu gani ambayo Sekretariat ya ajira katika Serikali ya India inayafanya ili na sisi tuone namna ambavyo tunaweza tukajifunza kutoka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kazi za Sekretariat ya Ajira katika Serikali ya India ni kukusanya taarifa ya soko la ajira, kutoa msaada wa watu kujiajiri wenye, kutoa mafunzo mbalimbali kwa wanaotafuta ajira, kusajili vijana ambao hawana ajira, kupeleka maombi ya kazi kwa wale ambao wanahitaji ajira, lakini kubwa zaidi wenzetu wanayo *scheme* ya kuwasaidia kutafuta ajira watu ambao ni *disadvantaged* yaani watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini tunajifunza hapa. Ninavyoona Sekretarieti ya Ajira inaweza kuwa na changamoto kuu mbili. Changamoto ya kwanza ni namna ambavyo Sekretarieti hii inaendesha usaili katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hii inamaanisha nini? Mathalani kama Mtanzania anaishi Kagera anatakiwa kwenda kufanya usaili Mkoani Dar es Salaam, mtu huyo ambaye anatafuta ajira wote tunafahamu anakuwa kwenye mazingira ambayo si ajabu hata nauli atahitaji kukopa.

Sasa mazingira ya namna hii yanampa ugumu Mtanzania ambaye anaishi pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam na wakati huo huo atafute angalau nauli ili aweze kufika Dar es Salaam, kuweza kufanyiwa *interview*. Huku ni kumkwaza Mtanzania ambaye ni mnyonge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali kwa kuwa Sekretarieti hii imekwishaanza kazi na ninaipongeza sana maana sasa ipo kwenye awamu ya pili iongeze Bajeti ya kutosha kwenye sekretarieti hii ili iweze kufungua *centres* zingine za kuwafanya *interview* Watanzania. *Either* ziwe *centres* za Kikanda au *centres* za Mikoa ili wale wanaotoka kwenye Mikoa yao waweze kufanyiwa *interviews* wakiwa huko huko kwenye Mikoa yao. Lakini pili changamoto ya *interview* katika nchi za wenzetu wamekuwa wakiwawezesha raia wao kuwa na *skills* za kufanyiwa *interview*.

Mimi ninaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ione umuhimu sasa wa kuhakikisha wanafunzi waliopo vyuoni wanawezeshwa kuwa na *interview skills*. Ni hatari sana mtu anayekwenda *interview* kama ana ujuzi mwingine wowote na kuwa na CV nzuri lakini kwa sababu ameshindwa kujibu, ameshindwa kufaulu kwenye *interview*, huyu mtu akapoteza kazi. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na watu ambao wana-*skills* za *interview* ili kuwawezesha kuingia katika ushindani kwa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira bado hajajitangaza vya kutosha, napenda kuipa changamoto Wizara ihakikishe kwamba inawafikia wadau mbalimbali na haswa wanafunzi wa vyuoni waweze kuilewa maana kule ndiko kwenye *pool* ya watu ambao wanavyo vigezo vya kuweza kuajiriwa Serikalini. Kwa hiyo, ni muhimu sana Sekretarieti hii ikawafikia wanafunzi wale waliopo vyuoni na wadau wengine wote. Lakini vilevile ni vizuri Sekretarieti ya Ajira ikawa na *website* yaani tovuti. Utaratibu wa *website* ni mzuri sana hata katika nchi za wenzetu wanautumia utaratibu huu, unawasaidia kupata *information* za ajira za nafasi za kazi lakini pia hata hili wazo la kufundisha *skills* za *job interview* mnawenza mkaweka *notice* kwenye hii *website* watu wakawa na uelewa wa kufanya *interview*. *Lets make use of the websites* ili watu waweze ku-*apply* na hii itawezesha hata Watanzania ambao wako nje ya Tanzania kuweza ku-*apply* kazi kwa kutumia hii sekretarieti ya ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kero ya wafanyakazi. Wafanyakazi ambao wameajiriwa wamekuwa wakicheleweshwa kuingizwa kwenye *payrolls* na hii inawasababishia kukosa mishahara yao kwa wakati. Kama vile haitoshi hata kama wafanyakazi hawa watakuja kuingizwa kwenye *payrolls* bado malimbikizo yao ya mishahara wanachelewa kuyapata. Inaweza ikawachukua takribani mwaka mzima kwa mtu kama mwalimu ambaye ameajiriwa huko kwenye shule za Kata inampa taabu kudai malimbikizo ya mishahara *say* ya miezi mitatu ndani ya mwaka mmoja. Gharama za kudai malimbikizo hayo kwa muda wa mwaka mzima inaweza ikazidi hata kiasi cha ile mishahara ya miezi mitatu. Kwa hiyo, mimi naiomba Wizara husika ione umuhimu wa kuharakisha watumishi kwenye *payrolls* ili waweze kupata misharaha yao kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie vikwazo katika Mifuko ya Pensheni. Kazi kubwa ya mifuko hii ni kulipa mafao kwa watumishi wanaostaafu. Lakini vilevile kulipa mafao ya mirathi na mafao mengine madogo madogo kama vile mafao ya ugonjwa na kadhalika. Mtumishi anapostaafu wapo baadhi yao wamekuwa wakicheleweshwa kulipwa mafao yao na moja ya sababu ni kwamba mwajiri anakuwa hajapeleka michango ya kila mwezi katika hii mifuko ya pensheni. Sasa ni vizuri kuiomba Wizara husika kuhakikisha kwamba inapeleka michango kwa wakati ili kuondoa hivi vikwazo. Lakini pia sababu nytingine ni upotevu wa nyaraka za ajira na hii inawapata sana wale ambao wanafutilia mirathi ya watumishi ambao wamefariki. Mimi naiomba Serikali husika ione umuhimu na itoe ushirikiano wa kutosha kabisa kwa hawa watoto ambao wanatakiwa kufutilia mirathi katika hii mifuko ya pensheni ili waweze kupewa mafao yao kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa rai. Nimeguswa sana hapa leo baadhi ya Waheshimiwa walipokuwa wanazungumzia suala la udini. Mimi nadhani tunapojadili hili suala la udini tusi-*generalize* sana mambo. Zipo taarifa hapa katika Wilaya ya Sumbawanga Mjini kuna Watanzania 400 wametengwa na makanisa kwa sababu tu walikuwa wanakiunga mkono Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninatoa rai kwa Waheshimiwa wezangu tunapoyazungumza haya masuala ya udini ni kweli wote tunaguswa lakini tusi-*generalize* mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba zilizopo mbele yetu. Naomba nianze na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa sana Tanzania la Serikali yetu kutokuthamini na kutambua ujuzi na utaalam walionao wataalam wetu. Mara nydingi tumekuwa tunalalamika kwamba hatuna wataalam wa fani mbalimbali lakini ukiangalia kwamba Serikali kwa kutumia fedha za walipakodi inawasomesha wataalam wengi wa fani mbalimbali lakini kwa kushindwa kuwawekea mazingira mazuri, kushindwa kuthamini ule ujuzi waliokuwa nao wengi wanaishia kwenda kufanya kazi nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Canada tunasema kwamba Tanzania tunashindwa kunufaika na madini yetu kutokana na kwamba hatuna wataalam kwa hiyo madini yetu yanakwenda kuchambuliwa nje na kila kitu kinafanyika nje. Lakini ukienda Canada kwenye viwanda vya madini wanaofanya kazi kule baadhi ni Watanzania. Kwa hiyo, kwa sababu tu Serikali yetu imeshindwa kuwathamini na kuwawekea hapa, wanakwenda kutafuta *green pasture* nje. Lakini pia sekta mbalimbali kama sekta ya afya hatuna madaktari wa kutosha wa fani mbalimbali. Ukienda Zimbabwe unakuta madaktari wa Kitanzania unakuta ni wengi kweli kwa sababu wameshindwa kutambulika nyumbani wamekwenda kutafuta *green pasture* nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali ije na utaratibu, lazima tuweke utaratibu wa kutambua kwamba kila mtaalam anayesomeshwa kwa namna yoyote tunamtumia ipasavyo hapa ndani ya nchi. Mara nyingi Serikali imekuwa inasema kwamba ni suala la soko huria lakini mimi ninashangaa huwezi ukasema ni soko huria wakati wananchi wapo na ndiyo wanaoathirika. Tunaokosa huduma ya madaktari, huduma ya wataalam waliobobeza ni Watanzania lakini wanaenda kuhudumia wenzetu huko nje. Huu ni udhaifu mkubwa wa Taifa letu, ni udhaifu mkubwa wa Serikali, tunaomba sana Serikali ihakikishe kwa namna yoyote ikiwezekana waweke kitu *incentives* anayesomeshwa, mtaalam apewe kitu ambacho kitamfanya hata huko anakokwenda aone hakuna umuhimu kama kubaki nyumbani kuhudumia Watanzania. Kama ni *engineer* tunatambua masomo yako ya miaka fulani kwamba umesomea uinjinia, kama ni daktari tunatambua miaka sita ya kuwa chuoni kama daktari. Kwa njia hiyo tutaweza kabisa kuhakikisha kwamba wataalam wetu ambao tunawasomesha kwa fedha nyingi sana wanafanya kazi ya kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la malipo ya wastaafu wa Jumuiya iliyokuwa ya Afrika Mashariki, kwa kweli hii inasikitisha. Jamani ni aibu, ni aibu watu ambao wametumikia Taifa hili, wameshiriki kikamilifu kuhakikisha wanaleta maendeleo ya Taifa hili, wametumika hadi wameishiwa nguvu sasa wamebaki ni watu wa kutegemea watoto na watu wa kutokujiveza, leo Serikali tunashindwa kuwalipa haki zao. Hakuna kitu kinatia uchungu kama unapowakuta wamekusanyika kule *Salender Bridge* wamelala barabarani, hakuna kinachotutia aibu unakuta wamekusanyika pale Mahakama Kuu wameungana msururu wengine wamekaa chini ni wazee ambao wamekwisha, hawana nguvu, unakuta wamekusanyika nyuma ya Bunge wanatafuta jinsi ya kusaidiwa, lakini Serikali haioni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuondoe hii aibu. Serikali iondoe hii aibu, iamue mwaka mmoja iseme hatutaki tena suala la wazee wa *East African*, tunatenga fedha hizi tuondokane na hili na tuwape haki zao waendelee kutafuta maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine walishafariki watoto wanafuatilia hakuna matumaini lakini pia wanadhalilika kule barabarani. Tulishuhudia *Salender Bridge* wamepigwa, akinamama wamelala barabarani mpaka wanatamani kumwaga radhi barabarani. Badala ya Serikali kuwaonea huruma polisi hao hao wanawapiga na wanawamwagia maji ya kuwasha. Naomba sana hebu Serikali iwe na huruma, itambue kwamba hawa watu walitumia nguvu zao, walitumia akili zao, walitumia ujasiri wao kuweza kusaidia maendeleo ya Taifa hili. Tusiendelee kuwanyanyasa kama vile hawakuwahi kutumika. Mbona wanalipwa wafanyakazi wengine ambao wanatumika muda kidogo, mbona tunalipwa wafanyakazi wengine wanakaa ofisini saa tatu, nne, kwa nini hawa waliokaa zaidi ya miaka 30 au 40 tunashindwa kuwalipa haki zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa Taifa, Serikali iondoe aibu hii kwa kuhakikisha kwamba watumishi hawa walitumikia Taifa hili wanalipwa stahili zao, waendelee na maisha yao ya kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Utawala Bora. Utawala bora ni lazima utokane na Utawala wa Sheria. Taifa letu, nchi yetu, maeneo mengi sana hakuna Utawala wa Sheria na kukosekana Utawala wa Sheria kumefanya Watanzania wengi kukosa haki zao za msingi. Kumesababisha Watanzania kushindwa kutimiza wajibu wao, kukidhi malengo yao na kuwasababishia Watanzania uchumi kuendelea kushuka na kuendelea kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukosekana kwa Utawala Bora, kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kiongozi ambaye anashindwa kutumia nafasi yake kwa ajili ya kuhudumia watu aliopewa awaongoze, anatumia nafasi yake kwa kufanya yale ambayo hakutakiwa kuyafanya, anasababisha maumivu makubwa kwa Watanzania, anasababisha maumivu makubwa kwa wale anaowahudumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu kwa kiongozi aliyepewa dhamana, mfano ni *DC* ana uwezo kwa kutumia u-*DC* wake, anakwenda kwenye boma la ng'ombe la wafugaji anakwenda kuchagua ndafu huyu, huyu na huyu, namchukua kwa ajili ya kwenda kula. Huo sio utawala bora, huo sio utawala bora. Utawala bora ni kuwasaidia wale wananchi uliopewa kuwaongoza waweze kujiongoza vizuri, waweze kutafuta maendeleo na waweze kutumia rasilimali kwa ajili ya kujiletea maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukosekana utawala bora, nichukulie mfano mdogo, maeneo ya rumande zetu kumekuwa ni maeneo ya kuwatesa wananchi kutokana na kwamba hakuna Utawala wa Sheria. Rumande za polisi za hapa Tanzania ni za kuleta mateso. Watu wanaopelekwa pale wanakwenda kuteswa na hawaendi kwa ajili ya kutafutiwa haki zao. Unapomweka mtu rumande, yule mwananchi hajahukumiwa na wala hajulikani kama ana hatia, pale ni mtuhumiwa. Lakini mwananchi kama yule unavyokwenda kumuweka kwenye chumba ambacho hakifai hata kumuweka mnyama mimi namshukuru Mungu kwamba nimebahatika kwa maisha yangu kukaa rumande ambako nilikuwa sijapita kukaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ni bahati kubwa sana Mungu aliyonionyesha niweze kujua wananchi maskini, wanyonge na wasiokuwa na hatia wanafanywaje wakiwa rumande. Kwangu nimejivunia kwa sababu nisingekwenda pale nisingeweza kuona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu ambaye anastahili haki zote hajahukumiwa kifungo, hajaiba, hajaua, unamuweka chumba ambacho ni sawasawa na chooni kwa muda wa zaidi ya siku kumi. Mimi nashukuru sikukaa siku kumi, nimekuta mwanamke amekaa kule siku kumi, chumba kina mifuko ya kinyesi pale pembeni, mifuko ya kinyesi imejaa, chumba kimetapaka mikojo, kina wadudu, mende na wadudu wa kila aina, mbu wanazaliwa pale pale, hivi kweli tunajivuna kwamba hii ni nchi ya amani? *Are we serious?* Huyu mtu tunamtesa pale rumande amekosa nini? Hajasimama Mahakamani, mwananchi amewekwa rumande siku nane, Sheria gani inasema mwananchi awekwe rumande siku nane? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusikitisha nimekuta mtoto rumande amekaa siku sita, mtoto wa miezi tisa. Nikajaribu kujiuliza mimi nimekaa siku mbili hapa nime-*feel pitch*, nimeumia, nimeshindwa kulala kwa muda karibu saa sitini, huyu mtoto amekaa siku sita rumande ni mateso gani amepata? Kwa sababu ya kukosa utawala bora tunathubutu hata kumtesa mtoto? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani sana *OCD* wa Wilaya ya Urambo na yeye aingie ndani pale rumande akae japo siku mbili tu, asingekubali mtoto akae pale siku sita, angeona huruma. Yote haya ni machache tu ambayo tunayaona, tusioyaona ni mangapi. Tanzania haina Utawala Bora, Tanzania haina Utawala wa Sheria. Tunaitaka Serikali yetu ihakikishe tunakuwa na Utawala wa Sheria, tumeandaa Sheria zetu, zisibaki vitabuni, tunawatendea wananchi unyama. Wale ni binadamu na wanastahili haki zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni rushwa. Rushwa ni adui wa haki. Rushwa inatutafuna kweli kweli na hata sasa hivi rushwa imeendelea kututawala. Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2009 imezungumzia masuala mengi sana ni jinsi gani rushwa inaathiri Watanzania. Mauaji tunayoshuhudia maeneo mbalimbali yamezingirwa na rushwa. Wananchi kujichukulia sheria mikononi ni matatizo ya rushwa, polisi hawatimizi wajibu wao. Wanachukua rushwa wanaachia watu, wananchi wanasesma kwa nini tumpeleke, tunamshughulikia wenyewe. Rushwa inasababisha ajali barabarani. *Traffic* hawafanyi wajibu wao, magari yakipita mabovu wanayaachia, wanachukua rushwa watu wanaenda kufa mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia suala la rada. Limezingirwa na rushwa, sitaki kulizungumzia leo, tutapa muda na ninaimani Ofisi yako itatoa nafasi tujadili vizuri hapa Bungeni tuweze kujua mbichi na mbivu. Lakini Serikali yetu ilinunua rada kwa fedha nyingi sana karibu shilingi bilioni 40 za Kitanzania. Kwa sababu wakubwa walichukua rushwa. Leo tunakaa hapa wenzetu kule kwa hisani tu mimi nasema ni hisani kwa sababu waliamua kusaidia Watanzania fedha zao zinarudi kwao. Leo badala ya kuona furaha tuwashukuru na tena tuwaambie tafuteni njia mradi fedha hizo zitumike Tanzania, tunakuja juu tunataka pesa zetu. Mlizishughulikia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichonisikitisha sana kwenye suala hili, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje amesimama kwenye vyombo vyahabari Tanzania anasema kwamba tunataka Uingereza warudishe pesa zetu, wametuibia. Wametuibia? Tuliwapa, hawakutuobia na cha kusikitisha wale waliohusika na masuala hayo wote wapo na wengine ni viongozi. Tunasema walituibia? Wamevunja wapi wakatuibia, hawajavunja benki? Kwanza tunaharibu mahusiano ya Kimataifa kwa kauli kama hizo kwa sababu ni hisani yao, tuombe zile pesa zije tuzitumie, tusianze kutoa kauli ambazo zitawaudhi watu ambao wametusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uwajibikaji. Suala la uwajibikaji ni tatizo na ugonjwa mkubwa kwa Tanzania. Hivi sasa tuna tatizo kubwa la umeme ambalo linaendelea. Waziri mwenye dhamana amesimama mara nyingi hapa Bungeni anatuambia kwamba mgao wa umeme utakuwa ni historia, lakini

tunachoshuhudia Watanzania ni kuongezeka kwa makali ya umeme siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tupo hapa sasa hivi Serikali nzima ipo Dodoma lakini utashangaa umeme unakatika saa kumi na mbili. Kwa nini Waziri asiwajibike kwa nafasi yake? Tunamtaka Waziri awajibike, badala ya kuonea Watanzania huruma, Wabunge wanalamika, wananchi wanalamika, ye ye anakuja kwenye vyombo vyahabari anasema wabezeni wanasiwa wanajitafutia umaarufu. Kweli! Huo ni uwajibikaji wa Waziri gani kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamtaka Waziri Mheshimiwa William Ngeleja kwa nafasi yake, kama ameshindwa aachie Wizara kwa watu wenye uwezo. Tunataka Watanzania wapate huduma, uchumi unashuka, maisha yanakuwa magumu na *production* imeshuka. Tunamuomba Waziri Ngeleja ajiuzuru kwa heshima yake na kwa heshima ya Taifa, Rais atafute mtu mwingine mwenye uwezo, aweze kutumikia Watanzania na kuleta umeme ambao utakuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliye maliza kuzungumza, kwanza nampa pole kwamba ye ye *justice over peace*, badala ya kwenda kukagua magekera kujua ikoje, imembidi akae siku saba akawa *graduate* ye ye mwenyewe, suali la msingi hapa liko, amesema nchi haina utawala bora... (*Makofi*)

MWENYEKIDI: Mheshimiwa Waziri, kaa chini.

WABUNGE FULANI: Kaa chini.

MWENYEKIDI: Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza tuwe na ustaarabu wa kuvumiliana, Waziri bila shaka alikuwa anataka kutaja kifungu kipi ambacho *an-base* kuhusu mse maji aliye pita, lakini kauli ya kumwambia kaa chini ni kauli ya Mwenyekidi peke yake. Naomba tuwe na ustaarabu wa kuvumiliana, sisi tuliookaa hatuna sauti, nguvu ya kumnyamazisha mwenzetu, ni amri ya Spika na wasaidizi wake mezani tu. Waziri endelea. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekidi, nakushukuru kwa kutoa darasa, ninataka nizungumze, Kifungu namba 64(a) na (b). Katika mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Inasema kwamba; “Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatotoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.” Kifungu (g) kinasema kwamba; “Hatotumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangaji aliyemaliza kusema ameeleza kwamba nchi yetu haina utawala bora, Mkuu wa Wilaya anaweza kwenda katika zizi la mtu, akasema ninamtaka ndama huyu au mbuzi huyu akaenda kumla bila lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naratibu utawala wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya nikimsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ofisi yangu hajapokea malalamiko ya aina hiyo wala hakuna hata *DC* aliyepelekwa Mahakamani kwa hilo, naomba Mwongozo wako Msemaji athibitishe hilo hapa ndani ya Bunge au atupatie jina hilo TAMISEMI tumshughulikie kwa sababu hapa wananchi wametusikia wengi, hakuna *DC* hata mmoja kwa taarifa ya Serikali, aliyeckwenda akadhulumu mbuzi katika zizi la mtu akamchinja na akamla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nitatoa Mwongozo mwisho wa kipindi chetu. (*Makofi*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(6) kwamba kitendo cha kuthibisha ikiwa msemaji aliyeppita amesema kitu ambacho siyo kweli, huyu anayetaka kutoa ukweli basi atuthibitishie katika Bunge hili ukweli wenyewe yeze na siyo aliyeppita, athibitishe yeze. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimesema Mwongozo uliotakiwa ni kwamba Msemaji aliyeppita ametamka suala ambalo atatakiwa kulithibitisha kwa sababu Waziri mwenye dhamana taarifa hii hana na wala haipo, kwa vile nimesema mwisho wa kipindi chetu hapa nitatoa Mwongozo wangu, naomba tuendelee. (*Makofi*)

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia kuwashukuru akinamama wa Mkoa wa Mjini Magharibi, vile vile kuwapa pongezi Mawaziri kwa hotuba zao walizotusomea hapa, ni nzuri, zimeeleweka na tumefahamu ndiyo maana sasa hivi tunachangia kwa hamasa kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningetaka kuzungumzia kuhusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi. Kwanza naipongeza Sekretarieti hii, lakini pia nawapa pole kwa sababu kumfuatilia binadamu mwenzio na ukaupata ukweli ni kazi ngumu na anatakiwa afanye kazi hii kubwa hadi afike katika ufanisi, ni lazima nimpe pole na kumpongeza kwa kazi yake nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kwamba wakati wanapokuwa wanatoa fomu za viongozi, ina maana zinafika mpaka Zanzibar kwa sababu wapo wafanyakazi wa Muungano na viongozi. Lakini nina masikitiko makubwa wakati fomu zikifika Zanzibar wanasarifisha kwa njia ya posta, fomu zinachukua muda mrefu utakapoifuata haina mfuatiliaji, fomu utaichukua, utaangalia na utaweka pembeni, hujazi

na wala hakuna atakayekufuutilia, wala hakuna matokeo mengine yatakayotokea dhidi yako. Hilo ni tatizo kwa upande wao kwa sababu hawana Kitengo Zanzibar au ofisi itakayowafanya watu wao wawe na harakati za kufuutilia kwamba kiongozi gani amepata na kiongozi gani amejibu na kiongozi gani anazishughulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najua Zanzibar ipo Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na ni jengo kubwa, ningeshauri wangeomba wapate ofisi pale ikawa kuna Afisa wao anayekuja na kufuutilia na kupata mwongozo kwa wale ambao tayari wamepelekewa zile fomu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba hizi fomu tukishajaza usahihi wake ukoje, kwa sababu mimi ndiye ninayejaza hizo fomu, ninakuletea wewe, mimi hunifuatilii kwamba kile kitu nilichokijaza ni sahihi au siyo sahihi, wala hakuna tathmini inayofanya mwisho angalau mimi mwenyewe nikajua japo kwa siri kwamba kile kitu nilichokifanya kimefuutiliwa na kiko sahihi au hakipo sahihi. Ningombwa hata hilo waliangalie kwa sababu baadhi yetu tunaweza tukawa tunadanganya tukijua kwamba hatufuutiliwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la *TASAF*. *TASAF I* imefanya kazi nzuri sana, lakini *TASAF II* bado ilikuwa inasuasua, miaka minne ya *TASAF I* mwaka 2000 mpaka 2004 wamefanya kazi nzuri. *TASAF I* ilifanya vizuri kwa sababu ilikuwa bado inasimamiwa na Wizara yenyewe, Wahasibu wa Wizara ndiyo waliokuwa wanasmamia, fedha zikitoka zinakuwa na usimamizi na ufatiliaji, lakini *TASAF II* moja kwa moja imekwenda kwenye Halmashauri, Halmashauri wanafanya kazi nzuri tu, lakini kwa sababu pesa ile ipo kwao na wao ndiyo watendaji, miradi hii inaibuliwa matokeo yake miradi hii inakuwa haina uhakika, miradi haimaliziki, fedha zinakwenda nydingi, lakini kinachotekeliza hakioneekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningombwa Wizara waangalie tena suala hili na nashauri wangefuata mfumo ule wa mwanzo wa *TASAF I* badala ya huu wa sasa hivi wa *TASAF II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekretarieti ya Ajira, inafanya kazi nzuri ya utumishi, na kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya mwaka 2007 wanaitekeleza ipasavyo, lakini kinachoshangaza ni kwamba sekretarieti hii kule Zanzibar haipo na sekretarieti hii ni ya Muungano na Zanzibar wapo watu wa Muungano, japo haijaingia katika kitengo cha Muungano *as such*, lakini inafanya shughuli za Muungano. Zanzibar wapo wafanyakazi wa Muungano na wanaajiriwa kufanya kazi sehemu za Muungano, inabidi wakati inapotoka taarifa kwenye magazeti au kwenye redio mtu atoke Zanzibar aje Bara afanye *interview* lakini kitengo kile kingekuwa kipo pale Zanzibar angeweza kufanya *interview* pale pale Zanzibar, waajiri wake wapo pale Zanzibar na Ofisi za Muungano zingine ziko Zanzibar, ingekuwa ni rahisi kuliko kutoka Zanzibar akaenda Bara akafanye *interview*, akakubaliwa na kurudi tena Zanzibar kufanya kazi katika ofisi za Muungano zilizopo Zanzibar. Nafikiri ingekuwa ni rahisi afanye *interview* pale Zanzibar. Naomba jambo hili vile vile waliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni wafanyakazi wa SMZ Zanzibar lakini anapata mkataba kufanya kazi SMT kwa bahati amefanyakazi SMT kwa muda wa miaka kumi, baada ya ile miaka kumi tayari mtu yule amefikia muda wa kustaafu, sasa kama atarejea SMZ kwa kima cha mshahara alichokiacha kwa muda wa miaka kumi ni kidogo, lakini huku SMT mshahara wake ulishakuwa mkubwa, naomba jambo hili mliangalie, badala ya mtu huyu kupata mkataba muweze kumwaangalia huyu mtu angalau na yeye apate *pension*, kwa sababu muda wake ameshaupoteza kafanya kazi nzuri Muungano na alikuwa mtendaji mzuri, amefikia kustaafu, yupo Muungano. Ninaomba mtu kama huyu afikiriwe na aweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Menejimenti ya Utumishi wa Umma, mimi najua Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatoa mafunzo elekevu kwa viongozi wa juu, lakini ningeomba wafanyakazi wa chini pia wanastahili pia na wao kupata elimu elekevu au mafunzo elekevu. Mfanyakazi wa chini anapoajiriwa wengi wanakuwa hawaijui *GO* haijui, *staff circular* haijui, yeye anakuwa yupo kazini ameajiriwa, na hawa ndio tuliozungumzia hapa kwamba wanakuwa wanapiga *story*, wanazunguka kwa sababu hana utaratibu wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunesema kwamba wafanyakazi wanachukua rushwa, tunasema kwamba wafanyakazi hawakai kazini, tunesema wafanyakazi wanavujisha siri za Serikali, hawa hawapati elimu ya kuwaongoza, wamepata elimu ya shule (digrii yake) kutoka shule mpaka ofisini hakupata mafunzo ya ofisi unategemea mtu huyo atakuwaje, ni lazima pawe na mandhari nzuri ya kumfanya yeye aweze pia kama mfanyakazi apate elimu pale ofisini kwake itakayomongoza ili kuzuia mianya ya rushwa, kuzuia uvujaji wa siri na kujua rika lake anatakiwa azungumze vipi na wakubwa wake na viongozi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, mfuko huu ni mzuri kwa sababu unafaidisha walengwa, unafaidisha wajasiriamali baadhi yao, lakini pia utagundua hawa wajasiriamali hawafanikiwi kuliko wafanyakazi wa maofisini, kwa sababu mjasiriamali hana elimu itakayomfanya ule mfuko aweze kupata vipi. Apite njia gani, aende ofisi gani ili aweze kufanikiwa. Huyu aliyepo ofisini anajua hali halisi, afanye vipi na apate vipi pesa hizi ili aweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji kutoa elimu kwa wajasiriamali ili huu mfuko uweze kuwasaidia na uwape matumaini kwa shughuli zao za kila siku. Kwa sababu akitegemea kupata pesa kwa mauzo yake itakuwa ni shida kwa sababu mjasiriamali kama alivyo hana kitu ambacho kitamfanya yeye aweze kufanya kitu kionekane. (*Makofi*)

Mheheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la samani, kumezuka mtindo katika Wizara zetu sasa hivi, kama hujanunua *furniture* zinazotoka nje ya nchi hujaona kama umekaa katika ofisi, wakati *furniture* zile siyo madhubuti, *furniture* zetu za miti ya mininga utakapotengenezwa mpaka unastaifu ofisi ile lakini *furniture* zitakuwa bado nzuri, na kama ina matatizo ni ya *vanish* tu au hata pengine umeichoka unaweza kuuza

ukapata hela tena tena. Lakini *furniture* tunazonunua njeni unga wa mbao ule uliochanganywa na kemikali wakatengeneza zikawa ndiyo *furniture*, lile ni tatizo, kwanza tunaitia hasara Serikali, inabidi kila mwaka ibadilishe *furniture*, maana leo ukisema kitu cha bosi unakisafisha unakivuta, ulishaharibu *furniture*, ina maana hakifai tena. Sasa tutakwenda kweli hivi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutakapokuwa na *furniture* zetu za miti yetu ya asili kwanza tutatengeneza ajira, ajira zitakuwepo za kutosha, iwe katika vyuo vyetu, iwe kwa watu binafsi. Ninaiomba Serikali izingatie tena kuangalia kwamba samani za ofisini na majumbani kwa viongozi ziwe ni samani kutoka katika miti yetu ya asili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliyozungumza yanatosha naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, katika muda mdogo nilionao naomba nizungumzie hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na ninaomba nizungumzie kuhusiana na Tume ya Mipango ambayo imechukua nafasi kubwa sana ya Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa sana ambacho katika nchi nyingi za Kiafrika na kwingineko, kimesababisha vurugu za kisiasa, vita vya wenyewe kwa wenyewe na matatizo ya aina hiyo siyo maandamano, bali ni kutokuwa na ulinganifu wa maendeleo katika nchi husika. Chanzo kikubwa cha Mataifa kuparaganyika ni Mataifa hayo au Serikali zake kufanya upendeleo katika mgawanyo wa rasilimali za Taifa. Wale wanaojiona kwamba wamesahauliwa wanasubiri, wanachoka, uvumilivu unaisha wanaanza kutumia njia zingine ambazo si njia za amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kwamba Tume ya Taifa ya Mipango inalo jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba Tanzania yetu tunayoipenda haifiki huko. Tume ya Taifa ya Mipango ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba tunakuwa na ulinganifu katika mipango yetu ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hili siyo jukumu la kupeana katika majukwaa ya kisiasa, ni jukumu la Kikatiba kwa sababu Ibara ya 9(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha kwamba maendeleo ya uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza kuwa na tatizo la upendeleo katika kupanga mipango ya maendeleo ya nchi, tunaanza kuwa na upendeleo katika kugawanya rasilimali za nchi yetu na hili jambo ni la hatari sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu kuna Mikoa ambayo iko pembezoni katika maendeleo iko nyuma kimaendeleo. (*Makofi*)

MWENYEKITU: Mheshimiwa Mbunge, naona kama kuna mwangwi hiyo naomba ubadilishe *microphone*. (*Makofî*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nasema kwamba kuna Mikoa ambayo iko nyuma kwa maendeleo kwa *indicator* mbalimbali ambazo zinatambuliwa Kitaifa na Kimataifa. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba Mikoa hii haiko nyuma kwa sababu tu haina rasilimali, bali vilevile ipo nyuma kwa sababu imekuwa inatengewa rasilimali kidogo na Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano michache ya kuelezea hatari hii. Katika orodha ya majedwali yanayoambatana na hotuba ya wiki iliyopita ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka huu wa fedha ukiangalia mgawanyo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mikoa na Halmashauri utaona yafuatayo; Mikoa ambayo imepewa fedha pungufu kuliko Mikoa mingine ni Mikoa mitatu, Mkoa wa Lindi shilingi bilioni 56, Mkoa wa Singida shilingi bilioni 63.8 na Mkoa wa Rukwa shilingi bilioni 63.9. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ambayo imepewa fedha nyingi kuliko mingine ni Mikoa mitatu ya juu, Mkoa wa Dar es Salaam shilingi bilioni 213.8, Mkoa wa Mwanza shilingi bilioni 156.6, Mkoa wa Mbeya shilingi bilioni 163.4. Wastani wa kila mkoa ni kuwa wastani wa mikoa yote ni shilingi bilioni 110.5 hiyo ni *national average* ya mikoa yote 21. Kwa maneno mengine ni kwamba Mkoa wa Lindi umepata asilimia 50.7 ya *national average*, Mkoa wa Singida umepata asilimia 57.7 ya *national average* na mkoa wa Rukwa umepata asilimia 57.8 ya *national average*. Wakati Mkoa wa Dar es Salaam, hiyo mikoa mitatu ya juu, mkoa wa Dar es Salaam umepata asilimia 193.4 ya *national average*, mkoa wa Mwanza una asilimia 158.8 ya *national average* na mkoa wa Mbeya una asilimia 147.8 ya *national average*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo siyo katika matumizi ya kawaida tu, tatizo hilo lipo vilevile katika fedha za maendeleo. Takwimu zinasema za Waziri Mkuu, mikoa mitatu ya mwisho kwa kupewa fedha za maendeleo mkoa wa Lindi shilingi bilioni 20.6, mkoa wa Pwani shilingi bilioni 22.3, mkoa wa Singida shilingi bilioni 23.4. Mikoa iliyopewa fedha nyingi mitatu ya juu ni mkoa wa Mwanza shilingi bilioni 63.6, mkoa wa Mbeya shilingi bilioni 52.6 na mkoa wa Shinyanga shilingi bilioni 49.6. *National average* katika fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 36.8. (*Makofî*)

Kwa maneno mengine ni kwamba Lindi ina asilimia 56 ya *national average*, Singida ina asilimia 63.6 ya *national average* na mkoa wa Pwani una asilimia 60.6 ya *national average*. Wakati hiyo mikoa ya juu niliyoitaja *their national average* ni zaidi ya asilimia 150. Mwanza ni asilimia 172, Mbeya asilimia 142 na Shinyanga asilimia 134. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye fedha za miundombinu ya barabara na haya vilevile yako kwenye hizo takwimu. Mikoa mitatu ya mwisho kwa kupewa fedha za barabara kufuatana na takwimu za Serikali mkoa wa Kigoma shilingi bilioni 8.9, mkoa wa Singida shilingi bilioni 8.9 na mkoa wa Lindi shilingi bilioni 9.7. Mikoa ya juu kwa

kupewa fedha za barabara mkoa wa Dar es Salaam shilingi 26.5, mkoa wa Dodoma shilingi bilioni 21 na mkoa wa Iringa shilingi 18.6. *National average* katika fedha za barabara ni shilingi bilioni 14. Maana yake ni kwamba hiyo mikoa mitatu tena ipo *below the national average* katika kupewa fedha za miundombinu. (*Makofi*)

Sasa hii ni Bajeti ya mwaka huu ukiangalia takwimu hizo hizo, majedwali hayo hayo kwa mwaka jana *the story is similar*. Wapo wanaoweza kusema kwamba kuna *factors* kama *population* na vitu kama hivyo zinazotumika kuangalia huu mgawanyo wa rasilimali, jibu la hoja kama hizo ni kwamba hiyo siyo kweli. Kwa sababu kwa takwimu hizo hizo Mkoa wa Shinyanga amba kwa sensa ya mwaka 2002 ni mkoa wa pili kwa wingi wa watu, umepitwa mbali na mkoa wa Mbeya katika mgawanyo wa hizi fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili tatizo la upendeleo katika utoaji wa rasilimali za Taifa ni tatizo kubwa lisipotafutiwa dawa, linaweza likatupeleka mahali ilipo Sudan au ilipo Uganda au ilipo Nigeria au ilipo Angola kule Kabinda ambako mahali inakopatikana mali watu hawafaidiki na mali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu siyo tu katika takwimu hizi, Tanzania kila mtu anafahamu ni nchi ya nne sasa kwa uzalishaji wa dhahabu katika Afrika. Mgodi mkubwa wa dhahabu nje ya Afrika Kusini na Ghana ni mgodi wa dhahabu wa Geita. Wilaya ya Geita ni moja ya Wilaya maskini katika nchi hii. Mgodi wa Geita unafuatiwa kwa karibu na Mgodi wa Kahama. Wilaya ya Kahama ni moja ya Wilaya maskini katika nchi hii pamoja na kuwa na migodi mikubwa ya dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni viashiria kwamba mipango yetu ya maendeleo siyo linganifu. Kuna mikoa na kuna maeneo yanapewa rasilimali zaidi kuliko maeneo mengine. Huu ugonjwa usipotafutiwa dawa unaweza ukatupeleka mahali pengine ambapo kila siku tunapiga kelele hapa tunapenda amani, lazima tuangalie haya masuala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile bado nina dakika tano naomba nizungumzie tatizo la rushwa na tatizo la TAKUKURU. Nchi hii kama maneno aliyosema Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwa Maafisa wa Kibalozi wa Marekani ni kweli kwamba tatizo la rushwa kubwa linashindikana kupatiwa dawa kwa sababu uongozi wa juu wa nchi hii unazuia hatua, basi Taifa hili tumefika mahali pabovu. Haya ni maneno ambayo yako katika *diplomatic cables* za Ubalozi wa Marekani kwenda *Washington DC*, kwenda *State Department* ya Tanzania *according to* Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwamba Serikali ya Tanzania tunashindwa kuchukua hatua kwa sababu uongozi wa juu wa Kitaifa unatuzuia, hili tatizo ni kubwa. Si tatizo la kisheria tena, kwa sababu kwa Sheria ya TAKUKURU ya mwaka 2007 yale Mamlaka ya Rais, kumuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa TAKUKURU kitu gani afanye na kipi asifanye hayapo tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tuna tatizo la kwamba asipofanya wanavyotaka hata kama sheria haimsemi afuate maneno yao, asipofanya anapoteza

kazi/ataachishwa kazi. Sasa hili ni tatizo kubwa kama Taifa tuna wajibu mkubwa wa kupambana nalo. Kwa namna yoyote ile inayowezekana kama haiwezekani kwa namna hizi za kawaida wananchi watachukua namna zingine ambazo siyo za kawaida. Kwa sababu watu wakichoka, watu wanapopuuzwa kwa muda mrefu wakachoka, uvumilivu ukaisha, wanachukua hatua ambazo hatujazizoea. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Aaah!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Ndio aah nini! (*Kicheko*)

Sasa naomba nimalizie kwa kusema yafuatayo, kama Taifa, kama Wabunge, hili Bunge tuna wajibu wa kuzungumza kwa uwazi mkubwa kuhusiana na matatizo haya yanayolinyemelea Taifa letu. Ni vizuri kwamba Bunge hili limeamua kwamba suala la nani aliyesababisha tukaibiwa kama wanavyodai na Waingereza kuhusiana na rada hili suala lijadiliwe hapa ili tujue kama ni kweli maneno waliyoyasema *Serious Fraud Officer* kwamba maamuzi ya aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hayakuwa na manufaa kwenye biashara ya rada tuyazungumze hapa Bungeni. Tusipoyazungumza hapa Bungeni tutahamia mitaani hamtapenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya matukio makubwa ya ufisadi ambayo yameliangamiza Taifa tuwanyooshee vidole, tuwataje hadharani, tuwazomee, tusipofanya hivyo wananchi wa Tanzania wasije wakalaumiwa watakapochukua hatua za ki-reclaim nchi yao. Kwa sababu *ultimately* mamlaka yote yapo mtaani siyo Bungeni hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITU: Nakushukuru. Kwa mujibu wa muda wetu huyu amekuwa ni msemaji wetu wa mwisho. Lakini kuna Mwongozo natakiwa nitoe, naomba nifanye kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 63(5) na (6) naomba niwasomee; “Bila ya kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yejote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdati Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.”

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Magdalena Sakaya anachangia, ametoa tuhuma juu ya mtendaji wa Serikali (*DC*) Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ametaka uthibitisho juu ya kauli ile kwa sababu kama mtendaji wa Wizara ya TAMISEMI, yeeye suala lile ameshindwa kulitambua. (*Makofi*)

Mimi kwa mujibu wa fasili hii ya 5 na ya 6 ninamuomba Mheshimiwa Magdalena Sakaya, athibitishe juu ya tuhuma alizozitoa, ama akishindwa kuthibitisha namshauri apeleke jina la Afisa huyo kwa Waziri Mkuu ili Waziri Mkuu afanye uchunguzi na hatua

zinazopaswa aweze kuzichukua, au afute usemi. Mheshimiwa Magdalena Sakaya karibu. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kauli yangu niliyoisema, nimesema kwamba kwa sababu ya kukosekana utawala bora, viongozi hata *DC* anaweza kuamua kufanya lolote analoweza kwa mfano, *DC* anaweza kuingia kwenye boma akachagua ndafu/mbuzi huyu akaondoka naye. Hayo mambo yanafanyika na kama Waziri anataka nimthibitishie nitamletea uthibitisho. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, nashukuru umenisaidia kutoa maamuzi. Nakuomba ulete uthibitisho huo siku ya Jumatatu tarehe 11 Julai, 2011 juu ya kauli hii. (*Makofi*)

Naomba kutoa matangazo yafuatayo kabla ya kuahirisha Kikao cha Bunge. Waheshimiwa Wabunge, kufuatia Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika leo tarehe 4 Julai, 2011, yamefanyika mabadiliko katika ratiba ya jinsi Wizara zitakavyowasilisha Bajeti zao katika mkutano huu. Mabadiliko haya yanagusa tarehe zilizopangwa awali kwa kila Wizara kuwasilisha Bajeti na hayabadili tarehe ya mwisho ya kumaliza Mkutano wa Bunge. Nakala za ratiba mpya zimebekwa kwenye visanduku vya Wabunge (*pigeonholes*). Naomba mpitie kwenye hivyo visanduku mnaweza kuona ratiba mpya baada ya mabadiliko yaliyofanywa. (*Makofi*)

Baada ya maelezo haya naomba kuwashukuru kwa ushirikiano wenu na naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.35 usiku Bunge lilifungwa mpaka siku ya Jumanne,
Tarehe 5 Julai, 2011 saa tatu asubuhi*)

